ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Thalathini na Mbili - Tarehe 29 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/14 - Wizara ya Mifugo na Uvuvi

(Majadiliano yanaendelea)

KAMATI YA MATUMIZI

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe nimearifiwa kwamba tumefikia pahala ambapo tunahitaji maelezo ya ziada ya Mhe. Waziri, ninaomba basi nimkaribishe Mhe.Waziri.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:Mhe. Mwenyekiti, ni kweli juzi hapa tuliondokeana tukiwa tuna hoja kuhusu suala zima la uagizaji wa kuku kutoka nje na Serikali ilitoa maelezo lakini bado ninaomba niendelee kutoa maelezo kwa nia ile ile ya kuwataarifu wajumbe na wananchi kwa jumla kuelewa hali halisi ya mahitaji yetu katika uzalishaji wa kuku.

Mhe. Mwenyekiti, mahitaji halisi ya kuku wanaohitajika katika Zanzibar kwa mwezi ni tani 585, kwa mwaka ni sawa na tani 7020, uzalishaji wetu wa ndani kwa mwezi ni tani 163 sawa na tani 1950 kwa mwaka. Kuku tunaowapata kutoka nje kwa mwezi ni tani 54 sawa sawa na tani 648 kwa mwaka. Upungufu wa kila mwezi ni tani 369 kwa mwezi, kwa mwaka sawa sawa na tani 4422, upungufu huu tukizalisha wenyewe tani 163 pamoja na zile tunazoagiza tani 54 bado tuna mapungufu ya tani 369. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa vyovyote vile tutakapojaribu kufungia uzalishaji maana yake tuna mapungufu katika uzalishaji kwa wakati huu ya mahitaji halisi ya kuku. Kwa hivyo tukizuia uagizaji kutoka nje maana yake tunapandisha bei kubwa ya kuku ndani na vile vile tunaathiri sana sekta ya utalii ambayo inahitaji sana kuku hawa wanaotoka nje. Tumepata simu nyingi kutoka kwa wananchi wakituomba kutuambia kwamba bado tuendelee kuruhusu

wananchi waweze kununua mahitaji hayo ya kuku wanaotoka nje kwa sababu ya hali halisi za wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini wakati huo huo serikali inajali sana uzalishaji wa ndani na ndio maana tunachukua kila hatua kusaidia wazalishaji wetu waweze kuzalisha zaidi ili waweze kukidhi haja ya mahitaji ya ndani na pale ambapo wazalishaji wa ndani wataweza kufikia lengo basi hapana shaka yeyote tutazuia uagizaji kutoka nje, lakini kwa sasa tunao upungufu mkubwa tukizuia utaleta athari, athari ya bei na athari pia ya kutikisa sekta ya utalii.

Mhe. Mwenyekiti, ilikuja hoja kwa nini wenzetu Tanzania Bara wameweza kukataza kuku hawa. Mhe. Mwenyekiti, wazalishaji wa ndani wa Tanzania Bara hivi sasa wanakidhi soko lao na ndio maana wakafikia hatua hiyo. Hata hivyo ma-*super market* mbali mbali ukienda pale Dar es Salaam utakuta wapo kuku kutoka nje na tukizuia leo hawa kutoka Brazil tujue watakuja kuku kutoka Nairobi na mahala pengine kufidia pengo hili. Kwa hivyo ni lazima tuchukue hadhari kubwa na cha msingi hapa ni kuendelea kuwasaidia wazalishaji wetu waweze kuzalisha zaidi ili tuweze kujikidhi soko la ndani. Hata hivyo, serikali kama nilivyosema juzi tuko tayari kukaa na wadau wote Waheshimiwa Wawakilishi, wazalishaji wa ndani ili kuona namna gani tutaweza kusaidiana zaidi kwa nia ile ile ya kulinda uzalishaji wa ndani. Lakini kupiga marufuku Mhe. Mwenyekiti, italeta athari kubwa kwa jamii kibei na athari katika sekta ya utalii. Ahsante sana.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa:Mhe. Mwenyekiti, natumia Kanuni ya 59(3) ambayo inaelekeza kwamba;

> "Mjumbe yeyote anapokuwa akisema Barazani atawajibika kuwa na sababu za msingi kwamba maelezo anayoyatoa ni sahihi na sio mambo ya kubuni au ya kubahatisha na Spika au Mjumbe mwengine anaweza kumtaka Mjumbe huyo anayesema atoe uthibitisho wa usemi wake unaohusika".

Mimi nataka nimuombe Mhe. Waziri katika maelezo yake hapa alitoa takwimu, nataka kujua zile takwimu ambazo amezitoa amezipata wapi? Je, ni sahihi kama ambavyo anatuambia, nilikua nataka kujua kile chanzo cha kupata ile takwimu alizozitoa, hilo moja.

La pili ameeleza kwamba amepigiwa simu nyingi sana na wananchi kuambiwa kwamba kuku hawa waendelee kuletwa, mimi nilikuwa nataka uthibitisho wa hilo. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, nafikiri tusipandishie hoja, wewe kama unazo takwimu sahihi toa kama huna tuendelee.

Mhe. Hamza Hassan Juma:Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninataka nikushukuru na kwa bahati nzuri na leo asubuhi hii niliamka na *ZBC*, nilipigiwa simu nyingi za kupongezwa kwa ajili ya kuwatetea wananchi, naondoka hapo. Mhe. Mwenyikiti, nakuja katika hoja.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nashukuru kwa maelezo ya Mhe. Waziri lakini naomba vile vile Mhe. Waziri na mimi anisikilize. Mhe. Mwenyekiti, suala la kuku kuna matatizo mengi ndani ya uletaji huu wa kuku hata ukiona sisi tunazuia jambo ujue kuna athari kubwa na nitatolea ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza tulipoingiza kuku hawa hawalipiwi ushuru hivi sasa hivi isipokuwa wanalipiwa kodi ya *VAT*. Mhe. Mwenyekiti, kuku hawa walipoanza kuingizwa nchini kontena ya mwanzo ilikuwa ya futi 20 ikalipwa 30,000,000/=, uendelezaji wa kuku ulipoendelea kuletwa kontena ya futi 40 sasa hivi inalipwa 8,000,000/=. Kwa hivyo ina maana hapo kwanza kodi ya Serikali inakwepwa hailipwi au labda tuambiwe Serikali inatoa *exemption* kwa wanaoleta nyama ya kuku ili kuuwa soko la kuku kwa upande wa Zanzibar lakini jengine Mhe. Mwenyekiti, kuna ubabaishaji mkubwa sana katika huu uletaji wa kuku.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa hivi ninavyosema kuna kontena imezuiwa bandarini kuku wameharibika, wameambiwa walipe 3,000,000/= ili nyama ya kuku ile ikaangamizwe. Sasa tujiulize kuna kontena ngapi ambazo ziliwahi kupenya hazikuwahi kuonekana na wananchi kuku wale wameshakula, kontena ile ambayo imekwama mpaka sasa hivi ya hii nyama ya kuku wenyewe wanaambiwa watoe 3,000,000/= waende ikaangamizwe mpaka leo kontena ipo pale. Mhe. Mwenyekiti, mimi ninataka niseme tuwalinde zaidi wananchi wetu. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, soko la kuku, kuku walikuwa hawatoshelezi kwa sababu tulikuwa tunaagizia vifaranga tulikuwa tunaagizia vifaranga kutoka Afrika ya Kusini, wananchi baada ya kuona kuna soko kubwa la kuku katika mahoteli Zanzibar wananchi wengi wame-*invest* katika kuleta *incubator* za kuzalisha kuku. Mhe. Mwenyekiti, nimeshatembelea na mimi utafiti wangu sio wa kuletewa kwenye ripoti nimeshatembelea *plants* karibu sita za uzalishaji wa vifaranga vya kuku na kila *plant* moja ina uwezo wa kuzalisha vifaranga 3000 kwa siku. Kwa hivyo sasa hivi wakiruhusiwa wananchi waanze kuzalisha kuku mahitaji ya vifaranga vitapatikana hapa hapa Zanzibar na uzalishaji wa kuku utakuwa mkubwa na hiyo *gap* ambayo iliyokuwepo sasa hivi itaweza kuwa-*covered*. Kuku wanazalishwa mpaka wanauzwa haizidi zaidi ya mwezi mmoja. Kwa hivyo ndani ya mwezi mmoja uwezekano wa wananchi ku-*cover* soko la kuku uwezekano huo upo.

Mhe. Mwenyekiti, narejea la mwisho. Wenzetu Brazil wanaofuga kuku ambao sisi tunawapa *exemption*, kule kuku wakipata mafua wanalipwa fidia, kuku wakifa banda zima kwa maradhi wanalipwa fidia. Hapa leo wafugaji wa kuku wameachiwa peke yao utafikiri Serikali haipo, wananchi wanafuga kuku, wanakufa kwa maradhi hakuna fidia yoyote. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Said Ali Mbarouk keshawahi kuitwa na mfugaji, waliingizwa vifaranga walikuwa na maradhi, vifaranga vile vikasababisha maradhi wakafa, kampeleka Waziri kamwambia Serikali itamuangalia haikumuangalia.

Mhe. Mwenyekiti, wenzetu kule wafugaji wao wakipata athari wanafidiwa, wafugaji wetu hapa hakuna mtu anayewafidia, *still* Serikali inasamehe ushuru ili kuku wale wauzwe kwa bei rahisi. Lakini jee, tujiulize kuku wale kwa bei inayouzwa hapa tuulize kule wananunua bei gani. Mhe. Mwenyekiti, suala hili bado nitaendelea kusimama na msimamo wangu sitoruhusu fungu hili kwa hizo athari nilizozizungumza kwa sababu hata tukisema tuzidishe hiyo kodi, kodi waliwahi 30,000,000/= kwa kontena ya futi 20, leo kontena ya futi 40 inalipwa 8,000,000/=. Kwa hivyo bado hawa wataendelea kwenda kuchakachua huko sisi tutapitisha wananchi wetu waumie.

Mhe. Mwenyekiti, mwenzangu mmoja hapa Mhe. Asha jana alizungumza na nampongeza sana kweli anawawakilisha wanawake ndani ya Baraza la Wawakilishi, kuku wameshaoza maana yake ingelikuwa tunazungumza vitu vya kubabaisha lakini kuku wameoza wanashindwa na 3,000,000/= pamoja na msamaha wote waliopata kwenda kutoa pesa waende wakaangamizwe, twendeni maeneo huru tukaangalie na namshukuru sana Mkurugenzi anayeshughulikia ukaguzi wa madawa na vipodozi kuangalia nyama mbovu isiingie nchini na mpaka sasa hivi kontena lile lipo na wenyewe wako wanashindwa kwenda kuliangamiza. Mhe. Mwenyekiti, naendelea kuzuia fungu.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:Mhe. Mwenyekiti, anachosema Mhe. Hamza ndicho hicho hicho kinachosema Serikali na madhumuni ya Serikali ni kuwasaidia wazalishaji waweze kuzalisha mahitaji halisi na ni vile vile ili kuhakikisha kwamba na jamii yetu inapata mahitaji yake ya nyama ya kuku.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nieleze kwamba Wizara hii ya Kilimo na Mifugo sio yenye dhamana ya kuingiza chakula ndani ya nchi kuna bodi maalumu chini ya Wizara ya Afya inayosimamia uingizaji wa chakula ndani ya nchi. Kwa hivyo ni Bodi ya Chakula, Dawa na Vipodozi ndiyo yenye dhamana. Ukitizama wao kwenye suala zima halihusiani na fungu hili wenye dhamana hiyo ni Bodi chini ya Wizara ya Afya, sasa ingelikuwa hoja hii ya kuagiza imeletwa pale tungeweza kuizungumza lakini kwenye suala la Wizara ya

Mifugo kuzuia fungu hili si halali kabisa na tukitizama suala la kodi kama kodi inayotozwa sasa haitoshelezi, sisi tunachotoza pale ni *VAT* kwa sababu kwenye bidhaa hizi za nyama sifikiri kama ipo kodi, inachofanywa pale ni kuweka *VAT* kwa msingi wa kuona uwiano wa bei kati ya wale kuku wanaoletwa nje na uzalishaji wa ndani.

Mhe. Mwenyekiti, isitafsirike kwamba serikali haiwapendelei wazalishaji wa ndani, nia yetu ni tuzalishe tuwe na mahitaji halisi. Lakini sharti tuelewane kwamba kwa wananchi wetu walio wengi bado sasa hivi mahitaji yao wanategemea kwa kiasi kikubwa uletwaji huu wa nyama ya kuku ambayo una bei nafuu na si ruhusa kuleta kuku wabovu, si rukhsa hata kidogo na Serikali haikatazi uzalishaji wa ndani na iko tayari kushirikiana na yeyote ili kuongeza uzalishaji, pale ambapo tutaona uzalishaji umekidhi mahitaji hapana shaka yoyote tutachukua hatua za kufungia, tukifungia sasa athari yake kubwa na Serikali ina dhamana ya jambo hili juu ya wananchi wake ndio tunalolizungumza hapa Mhe. Mwenyekiti. Ahsante sana.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, nimelazimika kusimama kuweka maelezo sawa juu ya kontena lililozuiliwa ni dhamana ya Wizara ya Afya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata chakula kinachokuwa *quality* na kilicho salama na ndio maana imeshatokea mara nyingi kwa vyakula kuzuiliwa bandarini kutokuingia kwa sababu huo ni wajibu wa Bodi ya Dawa, Chakula na Vipodozi. Naomba kumsahihisha Mhe. Mwakilishi aliyekaa kitako kusema kwamba kuku wale ni wabovu, hatujawahi wala hatutoruhusu chakula kibovu kuingia ndani.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nisikilize, kuku wale si wabovu, kuku wale ni wazima kilichofanywa kuzuiliwa mfanyabiashara ka-*forge document,* kuku wale walikuwa wanatoka Afrika ya Kusini ka-*forge document* na katia *document* ya kutoka Marekani akabandika *photocopy* ambayo hiyo *counterfeit* na kuharibu *competition* ya soko, tumezuia si kwa sababu ya ubovu ka-*forge* na tutawachoma kama ni moja ya adabu hata wakiwa wazima na gharama zote atalipa, ametumia *lable* ya *Tyson. Tyson* ni kampuni ya Marekani wana *security* hawezi kutoa kuku Marekani mbovu akaruhusiwa kusafiri kwenda kokote wana *lable* na kama Mheshimiwa anataka ushahidi tunayo mpaka *box* na tumeleta na *photocopy* hizi hapa, kachukuwa ile ya Afrika ya Kusini kaichana, ka-*photocopy* ya *Tyson* ambayo alama yake ni *red color* akabandika *photocopy* pale kutaka kuona kwamba anapitisha kuku wale.

Mhe. Mwenyekiti, tumezuia si kwa sababu ya ubovu ni kwa sababu *company* ime-*forge* na kampuni hii inaitwa *Malik Ferej Company* ambayo inafanya kazi kule Amani na wanaoleta kuku hapa ni kampuni mbili; kuna hiyo ya *Malik Ferej* na *Best Import.* Sasa katika kushindana kutaka soko ameona

atumie ujanja wa ku-*forge*, hatutaruhusu chakula kibovu kuingia na ndio maana kwa miaka miwili tulikuwa tunagombana na mchele wa Bopar mpaka tumehakikisha umechomwa na umetoka. Barua hii hapa tumemuandikia tarehe 16 mwezi ya Julai kwamba ame-*forge* kuku hawa hatuwezi kuruhusu na tutawachoma kwa gharama zake kama ni adabu ya kufanya fujo kutaka kuharibu biashara. Nilitaka Mhe. Spika, niliweke sawa, kuku si wabovu.

Mhe. Mwenyekiti, masuala mengine kuhusu suala la kuku walishafanyiwa uamuzi Baraza la Mapinduzi tangu mwezi wa Oktoba mwaka jana, ilikuja ajenda hii kama waraka na Wizara na maamuzi yakafanywa. Sasa kama kuna watu waliokuwa wanababaisha itakuwa ni tatizo la usimamizi na Waziri wa Fedha nadhani bahati mbaya hayupo yeye ndiye angeweza kutoa jinsi ya maamuzi ya Baraza la Mapinduzi kuhusu suala hili. Moja katika kilichoamuliwa sina hakika kama nasema siri ya Baraza la Mapinduzi kwamba wafugaji wa kienyeji wasaidiwe, chakula kifidiwe na vifaranga vifidiwe ili waweze kupata *competition* na kwamba makontena yanayotoka nje yawe yanatozwa zaidi ili kuhakikisha kwamba mfugaji wa chini analindwa, maamuzi yalifanyika hakukuwa na nia mbovu na Serikali haina nia mbaya na wakulima.

Mhe. Mwenyekiti, si ajabu maana mara nyengine vile vile inategemea na maarifa, si ajabu na sina hakika kwamba Bara wanazuia lakini si ajabu kwamba Bara wanazuia kwa kulinda viwanda vyao, kwa sababu kule kuna makampuni yanazalisha kuku ndio wakawa wanalinda viwanda vyao, pia wanalinda viwanda vyao vya saruji, sukari. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe mimi nadhani tungefahamiana vizuri, tungefahamiana vizuri ili tukaelewana hii ni Wizara ya Mifugo na Uvuvi. Suala tunalolizungumza hapa ambapo tumezuia fungu hili ni suala la biashara. Sasa nafikiri si vyema kuzuia fungu la Wizara hii kwa masuala ya biashara. Hiyo moja lakini la pili nafikiri tuangalie pande zote mbili. Mimi nakumbuka wakati fulani kuna baadhi ya wafugaji wa nje walitaka kuekeza wakati ule Mhe. Said Ali Mbarouk, alikuwa ndiye Waziri wa Wizara hii tunayoizungumzia sasa hivi. Mwekezaji yule akaambiwa mnapowekeza suala la mifugo itabidi uuze tu sehemu, mimi nadhani aliambiwa 5% ya uzalishaji wako katika soko la ndani, hatukatai kwamba usifuge hapa lakini asilimia 5% ndio uuze katika soko la ndani ili kuwalinda wafugaji wetu. Hii ndio ilikuwa sera ambayo imewekwa kwa sababu yule alitaka kuja kufuga na hapa tuna wafugaji wa ndani. Sasa nadhani tungeangalia katika sura hiyo.

Jambo jengine ni hili suala kwamba soko la ndani bado hatujalikidhi haja. Nitoe mfano ambao sio sahihi sana lakini unaoana. Tuliwahi kuwa na Kiwanda cha Sukari ambacho kilikuwa hakikidhi haja ya soko la ndani, sukari

ya nje ilikuwa inakuja lakini kiwanda chetu tunacho. Mfano mwengine ni saruji ya Tanga nayo ikawa inajaribu kuuwa saruji ya nje isiingie kwa bahati mbaya ikasemekana kwamba saruji ya Tanga wale watumiaji haina *quality* nzuri na kwa bahati mbaya ikawa ni bei kubwa zaidi kuliko ya nje yenye *quality* nzuri, saruji ya nje iingie wananchi wanufaike na ya Tanga *automaticaly* imekufa, mie sijaiona ndani ya soko kwa sababu wale wanaoitumia wenyewe binafsi hawaitaki kwa sababu ya tatizo la *quality* kwa wanavyoeleza, mimi uthibitisho sina. Sasa utenganishe suala la biashara na suala la ufugaji.

Tuna mifugo, mifano mengine, tuna mifugo miwili mitatu ya mbuzi na ng'ombe lakini siku zote ng'ombe wanatoka Bara wengi sana, wanachofanya wenzetu hawa Wizara ya Mifugo ni kuwaweka kwenye karantini kuhakikisha wako safi na ni wazima. Ingelikuwa sisi soko letu ni zuri kubwa la kutosha, tuna uzalishaji wa kutosha wa nyama ya ng'ombe, ingelikuwa hakuna haja ya kuleta mifugo kutoka nje, hili tumelinyamazia kimya kwa sababu nyama tunaihitaji ambayo sisi wenyewe wazalishaji wenyewe hatukidhi soko. Tukija katika eneo hili ukienda Pemba wanaokwenda wa nje nadhani ni kidogo sana, kwa sababu uzalishaji wa ng'ombe pale ni wengi zaidi, limesaidia soko la pale kuwa wanalimudu wenyewe, lakini hapa kuna upungufu mkubwa zaidi wa mifugo. Nadhani hata takwimu zinasema hivyo kwamba Pemba kuna ng'ombe zaidi wanaofugwa kuliko hapa. Sasa haya mambo tuyaangalia katika sura hiyo Waheshimiwa Wajumbe. Hilo moja.

La mwisho ninalotaka kusema tujitahidi sana chombo chetu hichi tusiwe watendaji, tukifanya utendaji ufanyike humu ndani siku moja Serikali hii tutaiangamiza itagonga mwamba, kama ni utendaji tuwaachie watendaji ambao ni Serikali, kuna maelekezo tutoe ili Serikali baadaye ituletee maelezo lakini tukisema twende humu ndani hapana tutakosea mtendaji ni serikali. Kwa hivyo, kama kuna jambo lina wasi wasi chombo hiki kinaweza kutoa maelekezo na ushauri kama vile tunavyokwenda kwenye kamati zetu na ripoti zile tunashauri, tunapendekeza serikali inayatizama yale halafu inatekeleza na baadae mengine tunaletewa ripoti kwamba hii ni kutokana na ushauri uliotoka kutoka kamati fulani ripoti yake. Mawaziri nao wanapowasilisha hoja zao mbali mbali wanasema tunashukuru sana kamati ilitusaidia katika moja, mbili, tatu. Sasa Waheshimiwa Wajumbe kuna mambo mengine hata utaratibu wa kusema kuwa uyapigie kura unaweza ukafika pahala mkakosea.

Nataka tujikumbushe suala la Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania juu ya suala la *Richmond* lilipoifikisha serikali pagumu sana kwa sababu ya kutenda mle ndani ya Bunge, hatimaye serikali ikawa imeingia kwenye mkataba ikawa inadaiwa malipo makubwa mno sote tunaelewa. Kwa hivyo, tujiepushe sana katika masuala ya kutenda. Sisi kama kuna mambo ya

maelekezo tutoe maelekezo serikali ikayafanyie kazi kama kuhitaji ripoti ituletee ripoti juu ya utekelezaji. Wataalamu wa utekelezaji na utendaji wako serikalini sio sisi. Mimi sishauri kwamba jambo hili liendelee kuwa ni hoja, jambo hili Waheshimiwa Wajumbe kwa heshima kubwa sana liendelee kuwa hoja.

Suala kwamba mahitaji yapo yanahitajika, suala kwamba wafugaji wetu tena ripoti imetolewa pale wasaidiwe yapo, suala kwamba kodi haitozwi itozwe, hiyo ni usimamizi kama kitu kile kinatakiwa kitozwe kodi kiasi fulani usimamizi wa watu wa kodi sio sisi. Tunaweza tukasema, tukaelekeza, serikali ifanye kazi juu ya kutoza kodi na pale ambapo serikali inasema inasamehe kodi kwa madhumuni ya kuwasaidia wananchi kuhusu bei vyakula vingi vinafanyika hivyo, vyakula vingi vinafanyika hivyo kwa nia ya kuwasaidia wananchi wapate unafuu, sasa haya mambo tuyaangalie sana.

Mimi wananchi nawapenda sana binafsi na kweli tumeshajihisha mno uwekezaji wa mifugo ya kuku pamoja na mifugo mengine. Wananchi wameitikia lakini muitikio wao haujafikia soko ambalo linahitajika, kama kuna mjumbe ambaye ana takwimu kwamba soko hili wame-*limit* atuletee. Mhe. Mbarouk Mussa Wadi pale nimemwambia atuletee, takwimu zako inaonesha kwamba hili soko wana-*limit* hawa wananchi hana, anataka kupinga hoja bila ya kufanya utafiti juu ya jambo ambalo yeye hana uhakika nalo, tena kifungu kile kinasema hivyo hivyo kama alivyokisema yeye mwenyewe.

Waheshimiwa Wajumbe tuangalie sana mambo haya, naomba sana tujiepushe katika suala la chombo hiki kutenda, penye tatizo tuliseme, tuielekeze serikali wakafanye kazi na tuiambie kwa hili tunataka mtuletee ripoti ambayo ni sahihi, lakini tukisema kila jambo tuliamue hapa serikali itatekeleza hatimaye chombo hiki itakuja hoja nyengine kwamba sasa ile hoja tuliyoipitisha kumbe ilikuwa si sahihi tuiondoe, hiyo haitaonesha umakini wa chombo chetu.

Waheshimiwa Wajumbe mimi nashauri. Kwanza fungu hili kulizuwia kwa sababu ya biashara ya kuku si sahihi, ingekuwa hawa watu wamewekeza hapa nchini na wametoa vitu vya aina hiyo, hiyo sasa ni sahihi tena nayo ingekuwa kama lile soko wanawauwa hawa jamaa kwa sababu ya kuwekeza mifugo. Suala la biashara watu wa biashara mnajua zaidi kama ingekuwa hapa pana vitu fulani vingi mno basi hakuna mtu atakayeleta kwa sababu anajua hakitanunuliwa maana tunacho cha kutosha.

Waheshimiwa Wajumbe nawaomba tuzingatie hayo tujiepushe utendaji moja, tuiambie serikali isimamie vyema jambo hili kama kuna kodi hailipwi sawa sawa isimamie ulipaji kodi, kama kuna kitu kimekuja kiko chini ya kiwango

vyombo vinavyohusika vifanye kazi, kama kuna kitu kimeharibika vyombo vinavyohusika vifanye kazi halafu viangamizwe kwa mujibu wa taratibu. Sasa tukiyachanganya yote nadhani itafika pahala si pazuri sana. Kwa fikra zangu nahisi fungu hili tungeliachia na wala hakuna haja ya kupiga kura juu ya jambo ambalo si la wizara hii na tujielewe.

Waheshimiwa tunaporuhusu upigaji wa kura juu ya jambo ambalo halihusiani na wizara ile inayohusika tunaweka *precedent* mbaya; itakuwa si vizuri, si sahihi, maana yake tutafika pahala tutakuja kusema mbona kipindi kile tulikubali kuzuia fungu la wizara fulani wakati jambo lenyewe wala halihusiani huko. Tuwe tunakwenda kwa utaratibu, kwa nidhamu ili tufike pahala serikali hii tuielekeze, tuishauri mambo ya kufanya, kama tuna wasi wasi kwamba wafugaji wetu wanalifikia soko kama inavyohitajika basi serikali inaweza kufanya kazi zaidi lakini taarifa imeshatoka hapa. Waheshimiwa Wajumbe mimi nadhani tuzingatie sana, sisi ndio viongozi tunaotakiwa tufanye kazi kwa faida ya wananchi wote. Narudia kusema kama pana upungufu wa ukusanyaji wa kodi basi kodi ikusanywe kwa mujibu wa taratibu zilivyo, kama kuna watendaji hawakusanyi kodi vizuri isiwe sababu ya kuzuwia fungu la wizara hii. Mimi nadhani Waheshimiwa Wajumbe naomba sana hili suala tuwe tumelizingatia hivyo.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru sana kwa busara zako, lakini naomba nikisome ukiacha hili fungu la Mipango na Sera, naomba nisome fungu ambalo linalohusu mifugo limeandikwa vipi, Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja ukurasa wa 201. Kwa hivyo, ina maana kama unasema Idara ya Maendeleo ya Mifugo ndio inayoruhusu wafugaji wapewe fursa, wapewe uwanja mpana wa kuendeleza mifugo, ukinizuwia hapa, nakuja kuzuwia huku.

Mhe. Mwenyekiti, kule Bara waziri aliyezuwia kuku wasiingie sio Waziri wa Biashara ni Waziri wa Mifugo tena anawajua idadi kwa kichwa kuku wangapi, mbuzi wangapi, ng'ombe wangapi *live* nilikuwa namuangalia Ndugu David Matayo. Mheshimiwa kuku hawa ambao hawana kiwango hata ukimuona mtu anafoji *sticker* hakuna ubora, leo mtu kitu hakina ubora anakuja kuingiza nchini ili kuuwa hawa watu wetu ambao hawana kulindwa.

Mhe. Mwenyekiti, fungu hili linasema Idara ya Maendeleo ya Mifugo, kuna pesa zimetoka *TASAF*, kuna fedha zinatoka wizarani kwenyewe kuwaelimisha wakulima. Sasa leo Mheshimiwa mimi nataka niseme mimi nimeshafanya utafiti, twendeni katika hao wazalishaji wa vifaranga nilisema mwanzo, zamani vifaranga vilikuwa vinatoka Afrika ya Kusini, sasa hivi vifaranga vinazalishwa nchini na mitambo imeshafungwa, tukiendelea kuruhusu hawa

Mhe. Mwenyekiti, wafugaji wetu ndio tunawamaliza watakuja zao Darajani kuomba tutawafukuza.

Mhe. Mwenyekiti, ukinizuwia kwenye mipango nakuja kuzuwia kwenye Idara ya Maendeleo, nitoe tafsiri ya maendeleo maana yake nini? Maendeleo sio kufuga kuku ukala maendeleo ya mifugo ni kuwa kutoka katika kuku wa kula kwenda katika kuku wa biashara.

Katika niliyozungumza nao Mhe. Mwenyekiti, kuna mmoja alikuwa aki-*supply* mahoteli karibu matano sasa hivi kishafunga, kuna wengine wanasa-*supply* mahoteli mbali mbali wameshafunga hayo ndio maendeleo ya mifugo Mheshimiwa. Mhe. Mwenyekiti, sio kila kitu kama tunaikamia tumeshapitisha vifungu vingapi Mheshimiwa, hatuikwamishi serikali tutaikwamisha serikali itakapokuwa haiwatendei haki wananchi. Hapa Mheshimiwa haki haitendeki.

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika alikuwa anafuga kuku sasa hivi sijui kama anafuga, mwenzetu aliyekuwa Mwakilishi Mhe. Tafana Kassim Mzee miongoni mwa watu ambao aliyeleta hiyo mitambo ya uzalishaji wa vifaranga, sasa hivi hauzi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna Waarabu fulani pale Fuoni wameamua kuhamia Bara wamekwenda kufuga huko Bara. Huko tunakoambiwa kwamba kuna kuku wanaotosheleza soko miongoni mwa wafugaji wametoka hapa wanakwenda kufuga Bara, hawa ambao wanaendelea kuzalisha vifaranga Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hao wateja sasa hivi wameanza kukosa soko hawendi kununua sasa hivi wanasafirisha vifaranga vinapelekwa Bara. Mheshimiwa ndio maendeleo ya mifugo hayo? Sikubali bado ninayo haki ya kuendelea kuzuwia fungu, kama mipango nitaliachia nakuja kuzuwia kwenye Idara ya Maendeleo ya Mifugo, Mheshimiwa kwa hoja zangu bado nina mantiki ya kuzuwia fungu Idara ya Maendeleo ya Mifugo niambiwe maendeleo ya mifugo, maana yake nini, kufuga kuku ukala?

Maendeleo ya mifugo tumeleta sekta ya utalii. Mimi naipongeza serikali imeleta sekta ya utalii, Mheshimiwa mwani hauna soko watu wanahangaika wako Darajani wengine wanakwenda kuomba, wafugaji wa kuku hawana soko, Darajani kushajaa wende wapi. Mheshimiwa hoja ninayo na wala hatuikwamishi serikali tunaisaidia serikali keshokutwa tukienda kwenye uchaguzi wafugaji wa kuku watatujia mlishindwa kutulinda, kura watakupigieni wanaoleta Peduu sisi tuachieni. Mheshimiwa hoja ninayo banda la kuku Kwamtipura limefungwa na mabanda maeneo mengi yameshafungwa. Idara ya Maendeleo ya Mifugo ukiniruhusu tuendelee hapa ili Mhe. Waziri aendelee kupata mshahara na wafanyakazi wengine fungu la

maendeleo ya mifugo tunalifunga bwaa! Mheshimiwa hoja ninayo naamini ndani ya miezi miwili wazalishaji wa Zanzibar watajitutumua watazalisha kuku kama walivyokuwa wakizalisha mwanzo na kwa sababu sasa hivi vifaranga vinapatikana Zanzibar kuku watapatikmana katika mahoteli Mheshimiwa utaalamu sasa umeshakuwepo.

Mimi nataka niseme kitu kimoja katika hao wazalishaji wa kuku, kuna wengine sasa hivi wameshasoma mpaka utayarishaji wa chakula kile chenyewe Mhe. Mwenyekiti, unatakiwa kuwe kuna *calcium* katika chakula cha kuku ili wale kuku waweze kuimarika kimifupa wakue kwa haraka. Miongoni mwa taaluma hiyo Mhe. Mwenyekiti, kuna mifupa ya hawa wanyama inakuwa inasagwa ili ipatikane *calcium* iingizwe katika chakula cha kuku.

Sasa nauliza je, hiyo mifupa ya Brazil tuna uhakika gani kwamba hamna mifupa ya nguruwe ndio inayotengezewa chakula cha kuku, sitaki kusema kwamba wanalishwa mifupa ya nguruwe aah! katika utaalamu wa kutengeneza ndio maana nikakwambia Mhe. Mwenyekiti, nishafanya utafiti mkubwa, nimekaa na wafugaji wa kuku na wazalishaji wa chakula cha kuku wamenieleza kila kitu, hapa Zanzibar kwa kuwa hatuna mifugo mingi yenye mifupa wanasaga kombe za baharini. Utafiti nimeufanya wanasaga kombe za baharini kule *calcium* inayopatikana wanachanganya katika chakula cha kuku na ndio hao kuku waliokuwa wanauzwa kwenye mahoteli.

Mhe. Mwenyekiti, kwa *plant* tulizokuwanazo za uzalishaji wa vifaranga, uzalishaji wa kuku ndani ya miezi miwili Zanzibar utakuwepo wa kutosha na wananchi wengi waliokuwa na mwani wao hauna soko watahamia katika ufugaji wa kuku, hata na mimi mwenyewe nitaingia katika soko hilo ili kuhakikisha kwamba soko la kuku Zanzibar tunatosheleza mahoteli yetu na ile sera ya serikali na katika MKUZA kuimarisha mifugo, kuuboresha utalii wetu. Sisi siku zote Mhe. Waziri wa Biashara anasema kila kitu tunaagiza kutoka Bara, mananasi, matikiti kwamba mahoteli yetu yanalishwa na vitu kutoka Bara leo tunashindwa kulinda wafugaji wetu wakalishe mahoteli ya Zanzibar. Mheshimiwa ajira kubwa sana na ninaamini mkinikubalia hoja yangu hii mtakuja kuniambia mwakani uzalishaji wa kuku umeongeza pato la wananchi kwa kiasi gani. Mheshimiwa bado naendelea kuzuwia fungu.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi namuelewa sana ile hamu yake aliyonayo Mhe. Hamza Hassan. Mhe. Hamza anatumia juhudi yake yote kuwatetea wafugaji wa kuku na ni wajibu wake na kwa kweli sisi sote tunamuunga mkono kwamba ana wajibu wa kutetea wafugaji wa kuku nchini.

Lakini tukiangalia *deficit* iliyopo ya *365 ton per month* kashindwa Mhe. Hamza kutueleza ana utaratibu gani atakaotumia ili kuweza kuziba nakisi ya tani 365 kwa mwezi kipindi hichi. Si kazi rahisi ni kazi ya kupata muda baina ya serikali na wafugaji kuangalia namna gani wataweza kuziba nakisi ya hiyo tani 365. Lakini nataka nimueleweshe Mhe. Hamza kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi Bara na Zanzibar kidogo tunahitilafiana, nyama ya ng'ombe, mbuzi, kuku, kabla ya kuchinjwa inakuwa chini ya jukumu la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, lakini ikishachinjwa tu ikawa nyama wakati huo haipo tena chini ya jukumu la Wizara hiyo, iko chini ya jukumu la Wizara ya Afya yaani Bodi ya Chakula, Madawa na Vipodozi ndio inayoshughulikia na nyama zote sio Wizara hii ya Uvuvi. Kwa hivyo, kuzuwia fungu katika wizara hii naamini kwamba mimi sio sahihi. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, tuangalie wenzetu Bara wametumia fursa gani ya kuzuwia kuku wasiingie nchini. Kule Bara walizuwia kuku wasiingie nchini miaka miwili na kidogo iliyopita na walitumia fursa pale yalipotokea matatizo ya mafua ya ndege. Yalipotokea mafua ya ndege Bara wakapiga marufuku kwamba nyama ya kuku isiingie nchini, lakini walitumia njia sahihi ya kuzuwia ambayo kuwa wao haitoweza kuwapa shida na ule mkataba ambao umetiwa sahihi na mikataba ya *WTO* kwamba wana *safe guard* kuku na ndege wa Tanzania. Sisi tuna sababu gani sasa hivi ya kuzuwia ghafla tu suala la kuku wasiingie Zanzibar, mpaka tuwe na ushahidi wa kina kwamba kuku hawa wana jambo fulani ambayo yote haya yanatakiwa yawe *establish*, si jambo rahisi.

Vile vile tukumbuke huko Bara wamezuwia mpaka mayai ya kuku kutoka nje kwa sababu ukizuwia wewe ku-*safe guard* kuku kwa mafua ya ndege, ina maana unazuwia mpaka vifaranga wadogo wadogo mpaka mayai kutoka nje, ninavyoelewa mimi wenye *incubator* Zanzibar wanaagiza mayai kutoka nje. Bara huruhusiwi kuleta mayai kutoka nje Zanzibar wanaruhusiwa kuleta mayai kutoka nje na hayo mayai wanayotumia Bara kutia katika *incubator* mengi yao yanapitia Zanzibar kwa sababu wao ndio wenye vibali vya kuingiza mayai kutoka nje. Tumesema kwamba hao wenye *incubator* hapa Zanzibar mayai hawazalishi Zanzibar kwa sababu hawana *per age* kutoka Zanzibar hapa. Utakapozuwia kuku wasiingie hapa Zanzibar inabidi uzuwie na mayai yasiingie Zanzibar, hiyo *incubator* yake Mhe. Hamza anayolilia mayai yake atapata wapi kuja kuangulia.

Kwa hivyo, masuala haya jamani si ya kuamua ghafla, serikali iliyakalia kitako katika BLM mara tatu kuzungumza kwa kina masuala haya na tutakwenda hatua kwa hatua mpaka tuhakikishe kwamba Wazanzibari wameweza kuziba hili pengo la nakisi ya ukosefu wa nyama ya kuku nchini. Naomba Wawakilishi mtuamini serikali ina mpango thabiti, waraka huu hapa uliokwenda katika BLW huu ni waraka wa tatu. Kwa hivyo, kwa nini serikali

ikapeleka nyaraka tatu katika BLM? Kwa sababu ya kuhakikisha kwamba Wazanzibari, wafugaji kuku wa Zanzibar wapate nafasi ya kuja kumiliki kulijaza soko hili la kuku, hakuna njia mbaya jamani hapa.

Mimi Mhe. Mwenyekiti, nasema kuzuwia fungu hapa wakati wizara hii haihusiki na wizara inayohusika na nyama imeshapita Wizara ya Afya itakuwa si halali. Mhe. Mwenyekiti nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninawajibika kutoa maelezo kwanza kwa mujibu wa utaratibu. Tunachokifanya sasa kuzuwia fungu hili si sahihi na tunafanya matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, naomba nipewe tafsiri kabla ya hiyo kauli ya Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora anayosema kwamba tunatumia vibaya matumizi ya fedha za serikali, nataka nipewe tafsiri ya maendeleo ya mifugo, maana yake nini? Maendeleo ya mifugo inapokuwa huyo mfugaji hana pa kuuza ndio maendeleo hayo? Mhe. Mwenyekiti, mimi nafikiri…

UTARATIBU

Mhe. Hamza Hasssan: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu….

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa mimi nadhani kuhusu utaratibu ulikuwa useme jambo gani utaratibu umekosewa, muache ajieleze kama ulivyojieleza wewe kwa mapana. Mhe. Waziri endelea.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme kwamba tuvumiliane kila mmoja anapopata nafasi ya kutoa maelezo kwa mujibu wa nafasi yake iliyomleta hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Hamza Hassan toka juzi tumekuwa tunamvumilia sana, anatoa maelezo na wananchi wamepata *message* na *message* waliyoipata wananchi wengine *negative* na wengine *positive.*

Mhe. Mwenyekiti, kinachojionesha hapa kama kwamba yale anayoyasema Mhe. Hamza ndio wanayoyakubali wananchi wote. Kwanza tuondokane na dhana hiyo. Wananchi wote hawana uelewa huo, wako wanaoona kwamba tunapoteza fedha zao kwa kutumia vibaya mamlaka yetu tuliyonayo. Hoja hii imeletwa kinyume na utaratibu, kifungu ambacho kimezuwiwa na ikafika pahala tukaahirisha Baraza la Wawakilishi kuja kuendelea na mjadala wa

kifungu hiki ni matumizi mabaya ya fedha za walipa kodi, hatukupaswa kufanya hivyo.

Lakini la pili Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa chini ya mfumo wa Umoja wa Kitaifa inawapenda sana wananchi wake na ndio maana kama serikali tulikaa vikao vitatu kujadili hoja ya wafugaji wa Zanzibar, tukajadili, tukafanya utafiti na hatimaye tukaja na maamuzi haya ambayo yanaelezwa na serikali. Sasa leo nimemsikia Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais anaeleza mahitaji kwa mwezi ni tani 585, ameeleza hapa tani zinazozalishwa ni 163, *deficit* ni 369; maelezo hayo yameelezwa kwa urefu kabisa sina haja ya kurejea. Hiyo ni kuonesha kwamba tuna mapungufu ya nyama ya kuku ndani ya Zanzibar, tunaposema kwamba fungu hili silo kwa sababu inayoagiziwa ni nyama ya kuku ni chakula sio mfugo. Mnyama akishachinjwa hawi tena mfugo unakuwa ni chakula kwa tafsiri ya Wazanzibari.

Mhe. Mwenyekiti, kwa tafsiri ya Wazanzibari kuku kabla hajachinjwa, akishachinjwa na kusarifiwa inakuwa ni nyama na ikishakuwa nyama kinakuwa ni chakula hauwi mfugo tena. Tunachosema kwamba kifungu hiki hakistahiki kuzuiliwa anaweza akawa na hoja Mhe. Hamza lakini si kwa kifungu hiki. Mhe. Mwenyekiti, umeeleza vizuri sana tunachosema serikali hii inawapenda sana wananchi wake.

Halafu sisi tunataka sana wafugaji wetu kama serikali wafuge na hata kama tuna uwezo wa kusafirisha nje tusafirishe na ndio maana serikali imeunda Wizara ya Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi na Ushirika. Wizara hii itatoa taaluma kwa wafugaji ikishirikiana na Wizara ya Mifugo kwa ajili ya kutaka wafugaji wanapofuga kuku wao wafikie viwango vinavyoweza kwenda kwenye soko. Wako wafugaji baadhi yao wazuri wanafuata vigezo vya ufugaji na kufikia *standard* ya kuuza kuku kwenye soko, mfugaji yeyote ambaye anayefuga kuku kwa kipindi cha miezi mitatu na akamlisha sawa sawa hana sababu ya kutokuogopa kushindana na mtu mwengine yeyote atakayeleta jambo kwa sababu huyo kuku atakuwa amefikia *standard.*

Lakini kuku wa nyama mtu anafuga kwa wiki mbili au mwezi mmoja anamlisha ikifika saa 12 anamzimia taa ili usiku asile, halafu unategemea mfugaji huyo achukue kuku wake akamuuze ashindane na mtu mwengine ambaye anafuata vigezo, haiwezekani.

Kwa hivyo, kama tunataka kuwasaidia wananchi wetu kwanza tuwape taaluma juu ya namna gani wanaweza wakamfuga kuku wa nyama afikie miezi mitatu, halafu tuone kwamba kuku huyo hatonunuliwa na mtu yeyote yule ambaye anataka hilo jambo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima zote naomba Baraza hili tukubali kwamba maelezo tuliyoyatoa kwamba Serikali imeandaa utaratibu wa kuwasaidia wafugaji na kama mfugaji anapata hivyo vigezo vya kumfuga kuku miezi mitatu ataingia kwenye soko na anaweza kushindana na kuku anaetoka Brazil, na atauza kwa elfu ishirini mpaka thatathini. Lakini tuone kuku anauzwa shilingi elfu sita, huyu ni kuku au kifaranga, kuku wa wiki mbili. Kwa hivyo, kama tunataka kuwasaidia wananchi wetu lazima tuseme kweli. Niliposema kwamba wananchi wana mawazo tofauti wapo wananchi ambao walilazimika wende marikiti wakanunue kuku. Lakini wakenda kule wananunua kwa shilingi elfu sita kifaranga, lakini akenda kwenye maduka yanayouza nyama ya kuku anapata nyama ya shilingi elfu mbili anapata kufutari vizuri na hilo nalo tusilisahau.

Kwa hivyo, ili wafugaji wa Zanzibar waweze kujitosheleza soko letu la ndani tufikie haya mahesabu sisi tunakwenda kwa hoja. Sasa na wataalamu tunao, kama tunakwenda kwa hoja hizi ambazo tumesema kwamba ni mahitaji ya Zanzibar kama wafugaji wetu wameshazifikia hatuoni sababu sisi serikali turuhusu waagiziaji wa kuku walete kuku. Kama hatujafikia kulishibisha soko letu la ndani la Zanzibar Serikali haiwezi kufanya hivyo kwa sababu tutauwa na sekta ya utalii kwa sababu hawa wawekezaji wa utalii kabla wananchi wenyewe kuagizia kuku kuleta hapa, baadhi yao wananchi maana wanaoagizia ni wananchi. Wawekezaji wenyewe walikuwa wakiagizia kuku moja kwa moja kutoka kwenye nchi zao. Sasa hapa liliopo kama ulivyosema Mhe. Mwenyekiti, kama kuna mapungufu kwenye kodi serikali iambiwe hivyo mbona hamtozi kodi.

Wataalamu wetu wanafanya utafiti kwa kina juu ya jambo hili. Mhe. Mwenyekiti, mimi sioni sababu na mimi nakuunga mkono na nawaunga mkono wale waliosema kwamba hoja hii ilipoletwa sipo. Lakini maelezo ya serikali sio kwamba hayapo, maelezo ya serikali ni hayo kwamba soko letu kwa wafugaji wa ndani bado hatujaweza kulitimiza, tukitimiza hivyo Serikali hatuoni sababu kuwaacha wananchi wetu wakaendelea na umaskini tukawanufaisha wafugaji wa nje. Kwanza wananchi waelewe hiyo, isizungumzwe hapa inaonekana kwamba Serikali hii inawakandamiza wafugaji wa Zanzibar sio kweli na sio sahihi. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, hoja hii imechukua muda mrefu kidogo na mimi nataka nitoe ufafanuzi kidogo tu kwa sababu katika maelezo yake Mhe. Waziri ametaja juhudi za serikali. Mimi ndiye Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kwa sasa hivi.

Nataka nithibitishe hilo kwamba sasa hivi Serikali imetenga karibu bilioni moja na milioni mia moja, kwa madhumuni ya kuwawezesha wananchi katika shughuli mbali mbali, shuguli za kutembeza watalii, suala la wafugaji wa samaki mafunzo mbali mbali na ufugaji wa kuku. Mimi Mhe. Mwenyekiti, ni mfugaji wa kuku maarufu sana nilikuwa sasa hivi nimeacha tu. Wakati nikifuga kuku Dunga kule mabanda yapo, shamba ninalo lakini kuku hawamo. Na nimewahamisha si kwa sababu sikupata soko, kaniadhibu yule niliyempa dhamana ya wale washughulikiaji wale kuku wangu.

Mhe. Mwenyekiti, siku moja nilimchukua meneja wa Serena nikaenda nae kule, nikamchukua na meneja wa *Beach Resort* nikenda naye wakati ule mimi nilikuwa ni Naibu Katibu Mkuu. Nikampa kuku wangu pale, mimi niliona wazuri lakini wale kuku wale *broilers* wanadasturi wakishashiba na wakesha kunywa maji wanatanua mabawa kama hivi, sasa utaona hili bonge la kuku. Basi alipokuja meneja Mhe. Mwenyekiti, akamchukua yule kuku akampindua akampekua hapa kwenye kifua anahesabu mbavu na pale kwenye kifua ndio panapo kuku. Sasa nini maana yake, inabidi sasa wakanambia kuwa tatizo kuwa aina ya vyakula vinavyotumika na mambo mengine kama haya yana matatizo uongeze dagaa kwenye chakula chao. Sasa mafunzo haya wananchi wengi sana hawana.

Mhe. Mwenyekiti, serikali imeanza kutoa kuku kuwapa wafugaji sasa hivi kwa majaribio karibu kuku 800 maeneo mbali mbali. Tunajaribu sasa hivi kuwapatia mafunzo ili wawe na kuku ambao watalingana na hadhi na daraja tunayoaitaka. Sasa namuomba sana Mhe. Hamza Hassan Juma sitaki kutumia wadhifa wangu wa ualimu kwa sababu hapa sote ni Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ana haki yake ya kufanya hivyo. Isipokuwa ninachoweza kusema kwamba Mhe. Mwenyekiti, serikali inafanya juhudi kubwa sana kuendeleza wafugaji na bajeti hii pesa hata kama ninazo mimi lakini uratibu uko chini wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa sababu wao ndio dhamana wa mifugo, wao ndio dhamana wa ufugaji wa samaki. Kwa hivyo, wanachohitaji wao kufanya sasa kwa kushirikiana na tumeshirikiana na kama sikosei tumetumia karibu kama milioni 17 sasa hivi kwa ajili ya maandalizi ya mafunzo haya. Mwaka huu tena Serikali imetoa pesa kama hizo kwa ajili ya kutoa mafunzo kuwaendeleza wafugaji wale wafuge kwa mujibu wa *standard* ambayo tuyoitaka.

Mimi nina hakika Mhe. Mwenyekiti, wapo wanaofuga kuku sasa hivi wanauza katika mahoteli mbali mbali na ninawajua wapo. Isipokuwa kinachohitajika sasa hivi ni kuzidisha taaluma kwa wafugaji wetu ili waweze kuendelea. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Ismail Jusa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, ingelikuwa si mjadala huu jinsi unavyokwenda hata nisingelazimika kusimama. Lakini kidogo napata hofu kwa sababu ile ile uliyoisema pale awali kwamba tunayoyaamua au tukielekeza hapa wataingia kwenye utaratibu wa muongozo wa taratibu za uimarishaji wa uendeshaji wa chombo chetu.

Sasa nilikuwa nataka utuwekee sawa kitu kimoja tu kwa sababu hapa kidogo unanishughulisha na nisingependelea ukaja ukafunga mjadala huu ukahoji kabla ya hili kupatiwa ufafanuzi.

Mhe Mwenyekiti, kanuni yetu wa 98 (6) (b) iko ukurasa wa 72, inasema kwamba naomba hii ifahamike, nasoma pale kwenye (6):-

> "Hoja ya kupunguza fungu lolote katika makadirio ya matumizi wa mwaka itayotolewa wakati kifungu kinachohusika cha fungu hilo kitakapokuwa kinajadiliwa na kamati kwa namna ifuatayo.

(a) Inasema kwa kupunguza shilingi mia moja ikiwa ni ishara ya kutokuridhika na sera ya jambo maalum lililo chini ya usimamizi wa wizara au idara ya Serikali. Isipokuwa taarifa itatolewa kabla ya Kamati ya Matumizi kukaa na majadiliano yatahusu tu jambo maalum lililotolewa.

Ninaloliuliza hapo na kutaka muungozo wako ni kwamba Mhe. Mjumbe ambaye amezuia fungu hili tulipokuwa tukijadili alitoa taarifa hii na tulipofika hapa akazuia fungu na kutaka maelezo.

Sasa tafsiri yangu ni hili baina ya mawaziri wanavyozungumza na hata kidogo kwa ufafanuzi ulioutoa Mhe. Mwenyekiti, kwamba hapa si pahala pake. Hili ndilo linalonipa shida kidogo nataka muungozo wako kwa sababu sera ya biashara kwa jumla iko katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Sera ya kulinda afya za wananchi kwa jumla yake ikiwemo na afya ya jamii iko katika Wizara ya Afya, lakini sera ya kuendeleza mifugo iko chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti, tukitizama kitabu hichi sitaki kunukuu kwa sababu ya kupoteza muda lakini labda kwa ufupi sana ifahamike ukitizama katika ukurasa wa 5, hotuba aliyokuja kutusomea Mhe. Waziri hapa katika sekta ya mifugo kuna kifungu pale cha (c) katika malengo au mtizamo wa baadae katika sekta ya mifugo juu pale. Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 5 kuongeza ajira kwa vijana kupitia shughuli za uzalishaji na mifugo.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, katika ukurasa wa 17 vile vile katika Idara ya Uzalishaji Mifugo ukurasa wa 17 malengo ya mwaka 2012/2013. Katika eneo la (d) kutoa nafasi za ajira kwa vijana kupitia shughuli za ufugaji.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka muongozo wako kwa sababu nahofia tukija kusema kwamba kila sekta ambayo ina wizara yake ikiwa itaingiza biashara suala la sera hatuwezi kulisimamia katika kifungu cha wizara ile tuingoje Wizara ya Biashara kidogo napata matatizo na ninavyofahamu mimi sera inahusu jambo lolote na tunafanya ufugaji ni pamoja na bidhaa na hata ukisoma hotuba ya wizara hii inazungumzia ufugaji na mazao au bidhaa zinazotokana na ufugaji. Kwa sababu haya yote yanakwenda kwenye mtiririko mmoja na sidhani kama mtu anafuga kuku kwa *hobby* tu kwamba ukiamka asubuhi. Tunafuga kuku kwa sababu ya kibiashara kupata nyama ambayo inakwenda kuuzwa kwenye soko la biashara ni ajira.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naona utuongoze vizuri ili baadae tusije kuingia huku, ikija kuingia kwenye wizara nyengine tutakuwa hatuwezi kuijadili kwa upana wake na hatuwezi kuhoji sera inayohusu kifungu cha kanuni 98 (6) (b) kinazungumzia kuzuia shilingi mia kwa kutokubaliana na sera. Nilikuwa nataka muongozi wako Mhe. Mwenyekiti, katika hilo. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nimekufahamu na kanuni iko wazi kwamba kama huafikiani na sera nzima kama ilivyo hapa basi unaondoa shilingi mia kama huafikiani na matumizi.

Sasa hapa sera inayozungumziwa ni ya kuleta nyama labda ndio hiyo lakini sera nyengine ni ile ya kuimarisha mifugo na kutoa ajira kwa vijana ndio iliyozungumzwa katika kitabu hichi na ndio nadhani hoja yako.

Mimi nafikiri hapa hii sera hasa si tunachozungumzia hapa moja kwa moja. Tunachozungumzia hapa ni mahitaji. Mimi nakubali kwamba ipo haja ya kuongeza ajira kupitia mifugo na ndio maana serikalai ikawa imefanya kila njia kuwafundisha, kuwashajihisha na wakati mwengine hata kutoa kama alivyosema Mhe. Waziri wa Kazi ili kuongeza ajira kupitia suala la mifugo ambayo wizara hii ndio sasa inatoa mafunzo nadhani kila kitu juu ya ufugaji ulio bora. Huko mimi sina matatizo nako.

Suala hoja inayopingana hapa ni hii kwamba kuna mahitaji makubwa kuliko uzalishaji. Suala hili la ubora au kutokuwa na ubora linaweza likazingatiwa kwa pande zote mbili. Mhe. Waziri hapa amezungumza kwamba juu ya ufugaji ulio bora ili kuhakikisha kuku wanaozalishwa wana kiwango. Serikali nia yake ile ile ya kuwahamasisha wananchi wetu wale ambao wanakubali

kufuga wafuge vizuri watoe mazao yaliokuwa mazuri ndicho alichokuwa akisema Mhe. Waziri wa Kazi.

Sasa mimi hoja kubwa naiona hapa ni suala la kukataa mara moja kwamba kuku wasiletwe tuangalie, *in fact* zake na Mhe. Waziri wa Biashara naye amezungumza vizuri. Twende *step* kwa *step*, mtoa hoja alisema kwamba katika kipindi cha miezi miwili soko litakuwa lime-*block* licha ya kufeli, kama ni sawa hiyo au si sawa.

Mimi nilikuwa nataka kushauri jambo moja pengine linaweza litasaidia. Hoja ya kuimarisha wafugaji wetu haina sababu ya kupingwa, kwa nia ile ile kama ilivyokuwa kwenye kitabu hiki cha Wizara ya Mifugo kutoa ajira kwa vijana. Hoja hiyo, ndio sasa na ndio mtizamo wa Serikali lakini hoja kwamba pia tunahitaji chakula hiki cha nyama ya kuku nayo pia ipo. Haya ni mambo mawili yote yana umuhimu yote yazingatiwe.

Ingekuwa tukiiachia Serikali pamoja na wafugaji na wizara inayohusika kwa ujumla na Wizara ya Biashara tukaiacha kazi hii ikafanywa ili tujue hatua kwa hatua tunapunguza kiasi gani uagizishiaji. Huku upande mmoja tunawainua wafugaji wetu, huku upande mmoja tunapunguza uagiziaji. Sasa mambo haya ndio nnayosema sisi hapa kama Wajumbe hatuwezi kuyafanya. Isipokuwa tunachoweza kufanya ni kuielekeza Serikali kuendelea kushajihisha wafugaji wetu kwa upande mmoja na kila pale *statistic* za mazao ya wafugaji yanapokuwa huku ndio tunapunguza uagizishiaji. Mpaka kufikia hapa sasa tumekidhi soko asilimia mia kwa mia tutafunga.

Sasa kazi hiyo mimi nafikiri humu ndani hatuwezi kuifanya. Kazi hiyo ifanywe na serikali kupitia kwa watendaji wake, kupitia Wizara inayohusika Wizara ya Biashara. Kwa hivyo, na Wizara ya Afya wakati wowote lazima ifanye hivyo kwa sababu ya kile kinacholetwa kiwe kiko bora na kinafaa kuliwa na binadamu. Lakini tukiamua hapa ndani kwamba sawa kata soko kuanzia leo la kuleta nyama. Kwa kweli hiyo itakuwa ina matatizo.

Sasa mimi ningeshauri kazi hii tuiachie Serikali ifanye utafiti wake tunapunguza uagizishiaji kwa kiasi gani wakati huku soko la uzalishaji wa wananchi tunaukuza. Lazima kuwe na *balance* katika mambo haya. Tukikata moja kwa moja keshokutwa hapa wananchi watalalamika na mahotelini kutakuwa na matatizo.

Waheshimiwa Wajumbe nadhani tulione hilo kazi hii tuiachie Serikali, kutizama mambo yote mawili uagiziaji tuanze kuupunguza lakini uzalishaji uweze kukua. Sasa kama hatukufanya hivyo itakuwa tatizo. Tatizo kwa

wafugaji wetu, tatizo kwa wananchi wetu, tatizo kwa utalii wetu. Ushauri Mhe. Hamza Hassan Juma lakini nadhani imefahamika.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, mimi nakushukuru sana kwanza kwa ushauri wako lakini na mimi katika huo ushauri wako nataka niongeze wazo katika ushauri wako ili tuendelee vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wa Afya pale amekuja na *documents* maamuzi ya Baraza la Mapinduzi katika suala zima la uletwaji wa kuku. Maagizo hayo watendaji hawakuyazingatia na ndio maana limefika hili tatizo. Mimi naamini bado Serikali yetu sijasema kwamba haiwapendi wananchi lakini Serikali ikishasema Baraza la Mapinduzi sisi tunasimamia na kwa kuwa ameshasema pale, sasa hilo Baraza la Mapinduzi kwa mujibu wa kifungu cha 45 cha Katiba linawajibika kwa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nina ushauri Serikali imeshatoa maagizo mengi hayatekelezwi na hapa kitu kimoja kile ambacho nilichokizungumza mwanzo kinachoua hili soko la ndani ni kwamba wale hawalipi kodi, ushuru wanalipa *VAT*. Kwa hivyo, kama hawalipi ushuru unalinda nini, Mhe. Waziri wa Biashara alizungumza kwamba wenzetu Bara wanalinda viwanda, Bara wanaruhusa kuweka viwanda vikubwa na vya kati, hapa Zanzibar hatuna viwanda sisi hatuna viwanda.

Sasa mimi ushauri wangu Mhe. Mwenyekiti, Serikali tusiiachie peke yake. Mimi niko tayari kufanyakazi nisilipwe hata shilingi kwa sababu tayari kuna dhana kwamba nnajenga hoja ili kufanya matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Mimi niko tayari Mhe. Mwenyekiti, na ninaamini na Waheshimiwa wenzangu wapo watajitolea tufanye kazi.

Kwanza kuangalia ile niliyozungumza mwanzo kwa nini kontena ya mwanzo ya futi 40 lilipitishwa kwa milioni 30, kwa nini kontena za sasa hivi zinalipishwa milioni 8 za futi 40. Hayo ni mapato ya wananchi na ya Serikali na Serikali tunaipenda. Sasa tukipata kujua sababu za kufanya hivyo, sasa tutapata kushauri kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, hawa kama alivyosema Mhe. Haji Omar Kheir unafika pahala mtu anakwenda kununua nyama mpaka shilingi elfu mbili. Lakini kuku wetu sisi anauzwa shilingi elfu sita. Ndio maana nikasema tuulize ile bei ambayo wanaonunua kuku kule. Lakini vile vile tujiulize kwa nini wakafoji *sticker*. Kwa hivyo, inawezekana kampuni hiyo hiyo iliyoomba kuingiza kuku wanaletwa kuku wa kampuni nyengine ambao hawana kiwango kile, hawa hawana leseni hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tulikwenda China tulisoma masuala ya kulinda biashara na kulinda viwango. Hawa kwanza wanatakiwa washitakiwe kwa

kufoji katika masuala ya kulinda biashara ukenda katika *WIPO*, kuna sera ya sheria tumesoma na huyu hapa mzee. Hawa wanatakiwa wapandishwe mahakamani kwa kufoji. Sisi bado tunawatetea. Sasa mimi nadhani Mhe. Mwenyekiti, utateuwa wewe mweyewe kamati ambayo bila ya malipo kamati ya wananchi ili sasa tukae na maamuzi ya Baraza la Mapinduzi yalielekeza vipi na tuangalie hayo maelezo yalisababishwa na nini. Kwa sababu wafanyabiashara wengi wanaoleta biashara hayakaliwi na Baraza la Mapinduzi. Ina maana hapa huyu mfanyabishara Baraza la Mapindizi lilikaa likaona namna gani ya kuweza kum-*treat* ili aweze kuingiza nyama katika nchi yetu. Halafu tutaweza kuzungumza na watu wa *TRA* watwambie kama ni maelekezo ya Baraza la Mapinduzi wapunguze kodi tutajua. Sisi kama ni chombo cha wananchi tutapata kuishauri Serikali ipasavyo.

Sisi ushauri wetu bei iendane na soko tujue bei wanayonunulia *form original* na ikiwezekana kamati ya kujitolea sisi tutakwenda mpaka Brazil tukaangalie ni nini wanavyonunua. Sisi tunawajua wafanyabiashara Mhe. Mwenyekiti, tunapita humo humo tunajua wananunua bei gani wanavyoeka. Je, hii walioileta hapa ni sahihi. Sasa hapo kwenye *sticker* ndio hapo tutapokwenda kuwafungisha. Maana yake tukija kulishughulikia suala la *sticker* itabidi ile Kampuni ya Afrika ya Kusini tutauliza je, *sticker* zile kama wamezitoa wao wenyewe Afrika ya Kusini na wao kwa mujibu wa sheria ya *WTO* wafungiwe. Mhe. Mwenyekiti, tukiingia sisi wananchi hili suala litakuwa kubwa sana na hiyo kampuni baada ya kuleta nyama itafilisika kabisa. Sasa tuamue moja tuingie kazini tukafanye utafiti toka wanaponunua na *sticker* wanazipata wapi na kampuni gani, Mhe. Mwenyekiti hiki chombo kinafanyakazi kweli kweli.

Mhe. Mwenyekiti, haya mafunzo umetupa wewe tumeshakwenda Jambiani zaidi ya wiki sita sitaki kuanza usanii na malumbano. Lakini Mhe. Mwennyekiti, mimi nikiwa Mwakilishi wa wananchi hii hoja naisimamia kwa nguvu kwa sababu najua kuna tatizo kubwa na namshukuru sana Mhe. Waziri wa Afya watendaji wake wanajitahidi sana kutulinda. Lakini hizi *sticker* Mhe. Mwenyekiti, nataka nikwambie sio kontena hili lililozuiwa tu *sticker* hizi kontena nyingi zimeshaingia kwa *sticker* feki na wananchi nyama wameshakula kwa siku nyingi sana. Kuna sababu gani ya kuendelea kulinda kitu hichi. Hawa si wafanyabishara ni wababaishaji.

Mhe. Mwenyekiti, ukiniruhusu kuunda kamati ya kujitolea tutafanyakazi tutakwenda mpaka Brazil, tutakopa nauli tutakwenda Afrika ya Kusini na Baraza la Mapinduzi wenzetu hawa tutakopeshana pamoja. Mimi bado nazuia ruhusa ili kwanza tufanye mambo haya tukishajiridhisha wataleta lakini kwa kodi ambayo watahakikisha na wazalishaji wa ndani.

Mwisho kabisa Mhe. Mwenyekiti, katika hao wazalishaji wakubwa waliofunga biashara zao ndio hao waliokuwa wanasambaza mahoteli sio kama wameshindwa kwa sababu kuku wao hawana ubora walishindwa bei watu wetu. Hayo mamilioni ya Mhe. Haroun Ali Suleiman utayatoa utakwenda kuelimisha yatakwisha kwa sababu watu wameshindana kwenye bei leo mwenye hoteli paja nono la shilingi elfu nne kweli ananunua kuku kwa shilingi elfu sita.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari sasa hivi wanazalisha mapaja mawili nono na uwezo wa kuzalisha na kusambaza upo ndio maana nikamwambia ndani ya miezi miwili kwa utafiti nilioufanya uzalishaji hapa utakuwa mkubwa na ndio maana nikasema Mhe. Waziri atakuja kusema katika hili fungu la maendeleo ya mifugo wananchi waliweza kuzalisha na ukaongeza mara nyingi uzalishaji wao.

Mhe. Mwenyekiti, kama utaukubali ushauri huo mimi fungu hili naliachia tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Haya Mhe. Waziri suala la taarifa aliyotoa Waziri wa Afya tuendelee kuiachia Serikali ifanye kazi na pale inapohusu kushitakiwa au laa, hiyo itakuwa ya serikali. Hili lisitukwazwe usimamizi kuhusu makontena mengine nayo yanatumia *sticker* feki bado ni usimamizi wa serikali.

Sasa hii iliyotokea iwe ni mfano kwamba inawezekana makontena mengine yanakuja kwa utaratibu huo huo. Hapo maana yake serikali ikaze buti neno hili watu wanalitumia sana ikaze buti. Serikali ikaze buti kama walivyofanya kwa hii lakini makontena mengine yote yanaweza yakaletwa si tu ya nyama ya kuku lakini vitu vyengine vyote ambavyo tunaviagiza kusimamia ni wajibu wake serikali.

Kamati ya kujitolea kuna haja ya kutoa ruhusa hapa kwamba Spika atoe ruhusa? Wakati mwengine hapa Mhe. Ismail Jusa analeta ma- *documents* ameyapataje hatujui, kajitolea kwenda kufanya utafiti na hata Mhe. Hija Hassan Hija baadae huwa analeta *documents* hapa na Mhe. Makame Mshimba yuko wapi naye huwa anatuletea hapa wamejitolewa kwa ajili ya kuona kwamba wanataka kuthibitisha jambo fulani.

Sasa Mhe. Hamza Hassan Juma kamati hii ya kujitolea watafute wenzako mkajitolee. Hii haina haja hata kutolewa hapa kwa sababu tukiitoa hapa itakuwa kama hoja hiyo si ya kujitolea tena. Nafikiri kwa mujibu wa taratibu zetu sheria ile ya fursa, haki na kinga za Wajumbe wanayo haki ya kupata

information kutoka Serikalini, wanayo haki hiyo tunataka *documents* fulani, atoe taarifa na Serikali ina wajibu wa kutoa taarifa.

Mhe. Hamza Hassan Juma mimi nadhani tukubali kwamba tuendelee na kazi na kama una wenzako mfanye hivyo, muifanye sahihi lakini isiwe ni ruhusa ya kutolewa hapa. Tukiitoa hapa kama ni hoja iliyokuja, hapana. Hiyo itakuwa sio kamati ya kujitolea mtanidai na pesa zenyewe sina.

Lakini wakati huo huo serikali tuiwachieni kazi Waheshimiwa Wajumbe, kwa kufanyakazi Wizara ya Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ili tujue tunapunguza uagizishiaji kiasi gani chini ya usimamizi madhubuti watu wasilete vitu *fake*. Tena Mufti wapo hapa, maana kusingizia kwamba mali hii inatoka pahala fulani ili ipate *quality* hiyo sio haki. Mufti mmoja yuko hapa. Mimi namkumbuka sana huyo.

Kwa hivyo, mimi nadhani hili suala lisitupe kazi. Nataka nitoe maelekezo kwa niaba yenu Waheshimiwa Wajumbe kwamba serikali tufanyeni kazi ya pamoja Wizara ya Mifugo na Uvuvi ndio serikali kwa ujumla hiyo, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kushajihisha wafugaji wetu kwa upande mmoja na kupunguza uagizishaji kwa kadri ya wazalishaji wetu wanavyotoa mazao yaliyo bora ya kutosha. Kazi hiyo kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Hamza Hassan pale. Mimi nadhani serikali izingatie, kupunguza uagizishiaji katika kipindi hiki cha miezi miwili mpaka mitatu baada ya kuona wananchi wamefanikiwa kwa kiasi gani kuzalisha zaidi na kwa ubora.

Sasa Waziri wa Mifugo na Uvuvi ufanye kazi kubwa, ukaze buti. Waziri sijui kama yupo, ukaze buti kuwashajihisha wafugaji watoe mazao yaliyo bora ili Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko awajibike, sasa kusema kwamba hapana tunapunguza kwa sababu wananchi wameshakuja juu katika kuzalisha vizuri zaidi. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko nadhani hayo maelekezo unayasikia. Mfanyekazi kwa pamoja Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi akimudu kuwashajihisha wakulima, tena na hapa kuna msaada mkubwa sana kuzalisha zaidi. Sasa na wewe peleka waraka serikalini ili kuona ni namna gani ya kupunguza. Maana mlipokubali uagizishiaji huu mlikwenda serikalini, si ndio hivyo. Itabidi murudi kule kule, mkaseme sasa wananchi wetu wameshakuwa wanazalisha kiasi kadhaa, tupunguze uagizishiaji chini ya usimamizi madhubuti wa Wizara ya Afya kwamba kila kitu kije kwa *quality* kiwe kinafaa kwa ajili ya matumizi ya binadamu. Sio tu wananchi wetu lakini pia kwenye mahoteli yetu.

Waheshimiwa Wajumbe nadhani tumeshafanyakazi ya kutosha na inaelekea watoa hoja wangu mbali mbali, wameona mantiki ya kuwa sasa tuendelee. Nashukuru basi tuendelee.

Kifungu 0201 Idara ya Mipango Sera na Utafiti 206,026,000

Kifungu 0401

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa jinsi unavyotuongoza na kutuelekeza na huu ndio umuhimu wa kuwa na kiongozi mtu mzima. Kwa hivyo, endelea kutushauri, kutuelekeza kwa niaba ya wananchi wa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, nikuthibitishie tu kwamba *backbenchers* na serikali hatuna ugomvi, lengo ni kusaidia wananchi na tunakwenda vizuri.

Baada ya maelezo yangu hayo Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye hoja katika wizara hii. Kwenye kitabu hiki Mhe. Waziri alisema kwamba ana changamoto la wataalamu hasa wa mifugo na akaashiria kwamba wameajiri wataalamu mbali mbali. Nimepata wasi wasi kwamba kuna wafanyakazi watano ambao wameajiriwa bado wakiwa ni wanafunzi na nilimpelekea majina Mhe. Waziri kwamba ayafuatilie. Sasa naomba maelezo yake.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Mwenyekiti, Idara ya Utumishi Serikalini ndio yenye kazi sasa hivi ya kuweza kuajiri pamoja na Tume ya Ajira. Sisi tunapeleka maombi ya kuomba wafanyakazi wanapelekwa kwenye tume na tume inatangaza nafasi zile, baada ya kutangaza ndio wanafanyiwa *interview*, halafu baadae tunaletewa wafanyakazi tu. Hatuajiri wala hatufanyi *interview* kwa wafanyakazi wale. Kwa hivyo, zote tunapeleka kule kwenye Tume ya Ajira halafu sisi ndio tunaletewa wafanyakazi. Wizara yangu haina *mandatory* ya kuweza kuajiri mtu yeyote.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwa mujibu wa maelezo ya Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Tume ya Utumishi Serikalini ilipelekewa majina. Hoja yangu ni kwamba tume hupokea majina ya wale watu waliohitimu, watu hawa walioajiriwa walimaliza *Certificate in General Agriculture* wakiwa watu watano, baada ya hapo wakaingia *Diploma in Animal Production*. Sasa wakiwa wanaendelea na *diploma* wameajiriwa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu ni kwamba ni muda gani wanakwenda kazini na muda gani wanakwenda chuoni, inawezekana wizara ilipeleka majina utumishi bila ya kuweka wazi kwamba hawa bado wanasoma. Kwa hivyo, sawa Utumishi waliwaajiri kwa sababu walipeleka vyeti lakini hadi sasa watu hawa wanasoma, ni muda gani wanakwenda ofisini na ni muda gani

wanakwenda chuoni, wakati hakuna hata ule muda wa miaka miwili ya kumaliza kusoma. Kwa hivyo, nilitaka nijue kwamba wao waliwaambia Utumishi kwamba hawa bado ni wanafunzi na je, wanafanyakazi vipi wakati wanafunzi na huku wanakwenda ofisini. Kwa hivyo, sio suala la Utumishi walipelekewa vyeti vya *General Agriculture* wakaajiri lakini bado wanasoma. Sasa nataka waziri aniambie ni muda gani wanasoma na muda gani wanafanyakazi za wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, bado naendelea kumjibu Mhe. Hija Hassan Hija kwamba Tume ya Ajira ndio inayoajiri, kwa sababu sisi tunapeleka kule wala hatupeleki majina, tunachopeleka tunaomba nafasi za kazi, nafasi za kazi zinatangazwa kwa kupitia Tume ya Ajira na wao ndio wanaofanya *interview*, sisi wanatuletea wataalamu.

Lakini vile vile nataka kusema kama wapo na tukiwajua basi tuwaambie neno moja, waendelee kusoma waache ajira ile au waendelee na kazi waache kusoma. Labda hivyo tunaweza kukusaidia.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mhe. Hija Hassan Hija kwa hoja yake hii lakini pili nimpongeze Mhe. Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi alivyoeleza ni sahihi kwamba kwa utaratibu wa ajira wa sasa unatakiwa uajiri utangazwe, muhusika anatakiwa aombe, halafu zinafuata taratibu nyengine mpaka anaajiriwa.

Sasa kutokana na tatizo hili ambalo amelisema Mhe. Hija Hassan kama hivyo ndivyo ilivyo, kwamba wameajiriwa katika kipindi hiki na wakati huo huo wanasoma. Basi kinachotakiwa kabla ya kufika miaka miwili, waache kwanza kusoma wafanyekazi baadae warudi waende wakasome. Kwa hivyo, mimi nasema wachague moja kama alivyosema Mhe. Naibu Waziri, wachague kazi au wachague kusoma. Kama wameajiriwa na miaka miwili haijafika basi ni lazima wafuate taratibu, waache kusoma wabaki kazini au waache kazi waende wakasome ili nafasi hizo ziweze kuwapata Wazanzibari wengine ambao wanaweza wakaitumikia taasisi hiyo. Hayo ndio maelezo ya serikali.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, mimi naona maelezo ya Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni sahihi. Juzi nilipochangia nilimuandikia Mhe. Waziri mpaka majina, mtu a, b, c, na d.

Sasa tangu juzi Ijumaa mpaka leo hawajapata ufumbuzi, maana yake hawajafuatilia. Mimi nasikitika tunamfanya haya Mhe. Mwenyekiti, kwa nia safi. Mhe. Waziri nilimuandikia mimi majina na Katibu Mkuu nikamletea

majina kwamba haya tuna wasi wasi nayo wameajiriwa wakiwa ni wanafunzi, Ijumaa, Jumamosi na leo Jumatatu mpaka leo hawajafuatilia, wananiambia hawajawajua basi kama hawajawajua nitoke mimi na wewe nikuoneshe.

Mhe. Mwenyekiti, tusiende hivi, tukenda hivi ndio serikali itakula hasara. Utumishi alipelekewa majina aajiri bila ya kuambiwa ukweli. Ndio maana nikawaambia kwa nia safi kuwa hawa wafuatilieni, angalau muwe na jibu sahihi. Sasa kama hawajawajua basi nitoke mimi na wao nikawaoneshe.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosema mimi ni kwamba utaratibu wa ajira usiende hivyo. Huko nje kuna watu wamesoma na wamemaliza hawana kazi. Kwa hivyo, tunapowaajiri watu kwa njia ya chini kwa chini basi tunasababisha malalamiko kwa Wazanzibari wengi ambao hawana ajira.

Mhe. Mwenyekiti, naomba utaratibu ufuatwe na Mhe. Waziri anithibitishie kwamba atachukua hatua gani ikiwa atawachunguza wale na kutambua kuwa bado ni wanafunzi. Ninachomuambia tu ni kwamba watatu kati ya wale wanasoma *Certificate in General Agricultural* na wawili ni *Diploma in Animal Production,* hivi sasa wako Kizimbani. Wanakwenda vipi ofisini na wanakwenda vipi chuoni. Naomba Mhe. Waziri aniambie atachukua hatua gani, hatua ambayo itakuja humu kuthibitisha kwamba ama wamesoma ama wanaendelea na ajira, hatuna tatizo nalo. Tunataka wasome kwa manufaa ya Zanzibar na waajiriwe kwa manufaa ya Zanzibar, sio wasome halafu aajiriwe. Jambo hili Mhe. Mwenyekiti, tumelichunguza mwaka juzi kwenye Wizara ya Miundombinu, watu wameajiriana wakiwa wanafunzi na likaleta gharama kubwa kwa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naomba Mhe. Waziri aniambie kwamba atachukua hatua gani ili kuweka nidhamu kwenye serikali kwa manufaa ya Wazanzibari wote.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nimemuelewa sana ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija na mimi maelezo niliyoyatoa hayawezi kuendana kinyume na hivi. Hayo majina anipatie mimi, nikishakuyapata tutakaa na wenzangu tutalimaliza hilo tatizo, wala hakuna haja ya yeye kwenda kuwaonesha, akishakunionesha, sisi tunataka kuthibitisha tu kwamba kama wameajiriwa katika kipindi hiki na wameajiriwa wakiwa wanasoma, huo sio utaratibu.

Kwa hivyo, hilo halina haja wala asipate tabu ndugu yangu Mhe. Hija Hassan Hija, mimi bado nina nguvu ya kufuatilia kama ni Kizimbani, kama wanasoma Uyole tutakwenda Uyole, kama wanasoma Ruvu tutakwenda Ruvu au kama wanasoma kule SUA Morogoro basi tutakwenda SUA. Anipe hayo majina mimi kama alivyowapa Waheshimiwa ili nijiridhishe, kama hivyo

ndivyo ilivyo basi hilo tatizo serikali haikubaliani na utaratibu huo, Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa hivyo, mimi nadhani hakuna haja kwa yeye kwenda kuwaonesha, anipe hayo majina tu sisi tutafanya hivyo, madhali keshawapa wenzangu na mimi anipe. Mimi ndiye Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Utumishi wa Umma maana yake ni wafanyakazi wote waliomo katika nchi hii, ukiachia wale sekta binafsi. Kwa hivyo, kama kuna taratibu za kiutumishi zimekiukwa basi mimi napaswa kusimamia. Mhe. Mwenyekiti, naomba niseme hayo.

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Waziri kwa sababu inawezekana tokea Ijumaa hadi leo majina wameshayatupa. Kwa hivyo, nitampelekea majina baada ya dakika tano, shukrani tuendelee.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia nilizungumzia suala la mradi wa *MACEMP* na kulikuwa na hoja mbili nilizizungumza. Moja imeshapata majibu nikaridhika kabisa inahusu mapato yanatokana na zile hifadhi za ghuba.

La pili ambalo nililizungumza lilikuwa ni kufanya uhakiki wa mali kwa maana ya *assets* zilizotokana na mradi mzima wa *MACEMP*. Sasa Mhe. Waziri alipokuwa akinijibu, nashukuru kanijibu vizuri kasema kwamba uhakiki umefanywa na hilo daftari la mali zake lipo.

Mhe. Mwenyekiti, sitaki kurefusha muda bure wa mjadala, nimesimama kwa sababu moja tu. Mimi binafsi kutokana na utafiti nilioufanya naamini kuna matatizo katika hili. Lakini sitaki tubishane bure Mhe. Mwenyekiti. Mimi nataka kutoa hoja ndogo halafu tuendelee, wizara au serikali ikikubali. Nayo ni kwamba ikiwa wizara imejirishisha na hilo, hasi kwanza tuna Kamati yetu ya Mifugo, Utalii, Uwezeshaji na Habari, Kamati yako Mhe. Mwenyekiti, kamati ya Spika. Naomba hili kwa sababu ni kamati ya kisekta nijiridhishe. Lakini niombe vile vile na Kamati ya *PAC* kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni zetu, uzuri mmoja kanuni zetu katika Kamati ya *PAC*. Kanuni ya 118(2)(c) inasema kuchunguza kwa njia yoyote inayofaa, mambo yote yanayohusu hesabu za serikali na asasi zake.

Mimi ningeomba hili likawa ni moja katika wajibu wao kwenda kujiridhisha kwa sababu ninazo taarifa kuna mvutano mkubwa wizarani madamu inawajibika kwa pamoja inawezekana kwamba inalinda hadhi yake. Lakini ninazo taarifa kwamba kuna mvutano mkubwa ndani ya wizara kwa sababu kuna Mkurugenzi ambaye anadhani kwamba hizi ni mali zake binafsi au za idara yake hawezi kuingiliwa. Kama lile la kwenye *account* ambalo waziri juzi kakiri hapa kwamba mapato ya ghuba anaambiwa haya sio ya serikali ni

ya kurugenzi. Hakuna mapato ya kurugenzi katika nchi hii Mhe. Mwenyekiti, mapato yote ni ya serikali yanapaswa kutambuliwa na Hazina na kusimamiwa na Baraza hili.

Kwa hivyo, na hili naomba nipate maelezo. Tukikubaliana hapo kwamba kamati ya sekta itakwenda kujiridhisha na kamati ya *PAC* nayo baadae ikajiridhishe kuona kwamba hilo daftari la mali zote zinazotokana na mradi wa *MACEMP* limekidhi haja, mali zote ambazo zimepatikana katika mradi ule zipo salama na zipo katika mikono inayohusika, sio mikono ya watu binafsi. Nikipata makubaliano na serikali, sina tatizo Mhe. Mwenyekiti, nitasema tuendelee. Naomba maelekezo ya serikali katika hili.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, serikali siku zote ipo kwa ajili ya kuwatumikia wananchi na msingi mmoja mkubwa ni kuhakikisha kwamba fedha za umma zinatumika kwa mujibu wa taratibu. Ni lazima taratibu kwa mujibu wa sheria zifuatwe na hakuna mtu mwenye uwezo kwa mujibu wa sheria ya kumiliki mali za umma ama kuzitumia visivyo.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, ushauri huu wa Mhe. Ismail Jussa Ladhu sisi tunaupokea kama serikali ili tuufanyie kazi na pale ambapo kuna mtendaji yeyote au kiongozi yeyote anayetumia mamlaka vibaya au matumizi ya fedha za umma vibaya, basi hatua zitachukuliwa. Ndio maana Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu imeanzisha sheria na sera mbali mbali kwa nia ya kudhibiti ubadhirifu katika mamlaka na taasisi za serikali. Kwa hivyo, jambo lolote ambalo linasaidia kudhibiti ubadhirifu wa fedha au matumizi mabaya ya fedha, au kwa mtu yeyote yule kutumia kinyume na taratibu zilizowekwa hatua zitachukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nilihakikishie Baraza hili kwamba ushauri tunaupokea kwa kwenda kuufanyia kazi.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa serikali kukubaliana na hoja yangu na naamini kwamba baadae kamati zinazohusika zitakuja kutupa ripoti, hata kama ni katika kikao chake cha kawaida cha Baraza kile cha mwezi wa Machi ambacho huwa tunapokea ripoti za kamati kuja kujua juu ya uhalisia wa mali ambazo zilitokana na mradi wa *MACEMP*. Baada ya maelezo hayo Mhe. Mwenyekiti, nashukuru tuendelee ahsante.

Kifungu 0401	Idara ya Uendeshaji na Utumishi	701,768,000
Kifungu 0601		

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii lakini pia nilipongeze sana serikali juu ya uamuzi wake au msimamo wake juu ya suala zima linalohusiana na nyama ya kuku.

Mhe. Mwenyekiti, wakati nilipokuwa nikichangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi, niliwasilisha masikitiko yangu juu ya wajasiriamali zaidi ya 300 ambao wamechukuliwa fedha zao au sijui kama wametapeliwa sina uhakika, wajasiriamali ambao ni wafugaji.

Nilimueleza Mhe. Waziri juu ya kuhusika kwa wizara yake, Wizara ya Tawala za Mikoa na Wizara ya Uwezeshaji juu ya utapeli ambao wamefanyiwa wananchi wale, ambapo kwanza walifanyiwa semina juu ya masuala ya mifugo ya kuku na ng'ombe lakini baadae wakachangishwa fedha ili waletewe mifugo na kuku kutoka Tanzania Bara, lakini hadi leo hii hawajapata na wakatakiwa wajenge mabanda kwa kujitayarisha, na mabanda walijenga lakini hadi leo hii hawajaletewa mifugo hiyo. Waliwahi kuletewa kuku lakini walikuwa ni vijogoo.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri alipokuwa akijibu alisema kwamba wizara yake haikuwa na mkataba na watu hawa. Kwa hivyo kwa namna moja au namna ya pili kwamba wao hawahusiki moja kwa moja. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa taarifa niliyokuwanayo ni kwamba maofisa wanaoshughulikia masuala ya mifugo walishiriki. Kwa kweli hawa watu waliotoka Bara kuja huku walipokelewa na serikali na kwa sababu malipo hayo yalifanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, lakini nilipata taarifa kwamba mpaka Pemba watu hawa wamefika na Wilaya ya Magharibi pia wamefika.

Sasa kwa kuwa serikali inafanyakazi hii kwa pamoja na kwa kuwa Waziri anayeshughulikia Tawala za Mikoa ambapo fedha hizi zililipwa chini ya mikono yao na ndani ya ofisi yao, na kwa kuwa Waziri wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika alikuwa ni mgeni rasmi siku hiyo wakati wa kuzindua hayo mafunzo. Kwa hivyo, nilikuwa nataka maelezo ya serikali.

Je, wananchi hawa baada ya kutapeliwa na kuchukuliwa pesa zao ni hatua gani za serikali juu ya mama yule ambaye kachukua fedha na kisha baadae kaingia mitini na hatua ambazo mpaka sasa zimechukuliwa. Mhe. Mwenyekiti, naomba maelezo.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nashukuru sana suala hili Mhe. Salmin Awadh kulileta. Naomba nipongeze juhudi zinazochukuliwa na Wizara hii ya Mifugo na Uvuvi. Nimehusishwa na suala hili, nasema nimekuwa *victim* na

circumstances, kwa sababu mimi nilialikwa tu niwe mgeni rasmi nikatoe vyeti kwa wajasiriamali wale.

Miongoni mwa wajasiriamali wale wako wananchi wanatoka jimboni mwangu na kwa kweli miongoni mwa wafugaji waliopata matatizo na walioumia na kupata hasara ni wafugaji mbali ya jimbo langu, lakini karibu Mkoa mzima wa Kusini na mikoa mengine.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya tukio lile sasa wale wajasiriamali wote wanatuambia wewe ulikuwepo siku ile unawajua hawa. Kweli anayekamatwa na ngozi ndiye mwizi lakini mimi nimefanya juhudi Mhe. Mwenyekiti, nilimpigia simu yule mama mara nyingi sana, alinipa dharura kubwa. Aliniambia mume wake alipata maradhi ya baridi akampeleka India na magharama. Nikamwambia lakini mama umechukua pesa za watu, wananchi wanazitaka wale maskini ya Mungu pesa watazipata wapi. Akasema aliwahi kufanya mazungumzo labda wizara itatusaidia kidogo na Mkurugenzi wa Mifugo inawezekana hili analijua. Lakini masuala haya zaidi yalisimamiwa na Wakuu wa Mikoa ndio waliwaalika wakaja pale, kwa kupitia wapi mimi sijui. Mimi ndio kama ninavyokuambia Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa ni mgeni rasmi tu. Sasa hivi itabidi kabla sijenda mahali nitafute kabisa kuna tatizo gani, kama hakuhusiki nisiende maana mambo mengine yanakuwa ni mazito.

Sasa huyu mama aliniahidi mimi kwamba ni juzi tu kama leo ya tatu nimezungumza naye, aliniahidi katika kipindi cha mwezi mmoja atakuja hapa atakutana na wajasiriamali hao na wakulima na ataanza kuleta mifugo ile. Makubaliano yalikuwa yanasema kwamba ataleta kidogo kidogo. Lakini kuna kosa moja limetendeka, walikubaliana waletwe hao kuku wa kawaida ambao tunataka tuwaimarishe hao wajasiriamali wetu. Kwa bahati mbaya waliletewa vile vijogoo na utavilisha vile kwa miezi au miaka viko vile vile tu, soko liko wapi halipatikani ndio maana yake Waheshimiwa wakati mwengine wanapiga kelele, ni kweli.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nasema hili suala kwa upande wangu ninavyolijua niliona nilieleze hivyo, na nilichukua juhudi kuisaidia hii wizara kwa sababu sote tunawajibika kwa pamoja, nimeliulizia. Lakini pengine wao wana taarifa za nyongeza basi wangetusaidia. Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi niseme kwamba kwa kweli mtoto anapoharibu mambo huko nje, sasa wao wanajua ni baba, ijapokuwa alipokuwa anafanya hajakushirikisha ni sawa sawa na mimi.

Kwa kweli wizara haikushirikishwa, wajasiriamali hawa walipitia huko nafikiri kwenye Tawala za Mikoa lakini lilipoharibika ndipo walipokuja sasa. Naamini kama lingetengenea hata kupita wasingepita, walikuja na malalamiko yao tukawaambia sawa, ilivyo sisi hatuhusiki kisheria, maana yake kwa sababu hatuna mkataba na nyinyi. Mikataba yao walifanya na Tawala za Mikoa huko. Tukawaambia lakini hata hivyo kama wizara itabidi lazima tukusaidieni. Siku ya pili musizowee kwa sababu mnapofanya kitu kama hiki ni lazima jambo la kwanza mutie mkataba na wizara yenyewe husika, kwa sababu leo ndio limeharibika hilo. Sasa sisi hatujui tuanzie wapi, sisi hatuna nguvu za kisheria za kuwashtaki wale kwa sababu hatuna mkataba nao na hivyo ndivyo ilivyotokea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe binafsi kama waziri nilimuita mama Lucy na nikamueleza hii hali na yeye mwenyewe alieleza akasema kwamba tumpe muda na watawafidia fedha wale ambao wamekula hasara. Kwa hivyo, mimi niseme tu kwamba hili suala kama alivyoeleza Mhe Waziri pale wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika, sisi kama Wizara ya Mifugo na Uvuvi hatuhusiki kabisa. Wao wamejaza mikataba na Tawala za Mikoa.

Mimi ninawashauri kwamba linapotokea jambo kama hili basi wafugaji waje kwanza wizarani ili tutie mikataba na wao, ili linapokuja kuharibika sasa sisi tutahusika moja kwa moja, kama kuchukua hatua za kisheria au vipi lakini kwa hatua hii mimi ningewaomba basi wafugaji wachukue hatua ya kumpeleka Mahakamani yule mama basi, sisi hatuna nguvu za kisheria kwa sababu hatuna mkataba na wao. Mhe. Mwenyekiti, ni hivyo tu. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, mimi ndio kwanza nilisikie hili suala leo hapa. Huo ndio ukweli kabisa na Mhe. Waziri anazungumza kwamba Tawala za Mikoa kama ni wizara. Mimi nafikiria labda angekuwa *very specific* angezungumza labda Wakuu wa Mikoa fulani au fulani.

Mimi ninachoomba tu Mhe. Mwenyekiti, basi ndio limeshatendeka tutalichukua kama wizara sasa, nikae na wenzangu pamoja tuone vipi tunalishughulikia na hasa kama alivyoeleza Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika kuwa keshazungumza naye huyo mama, basi tutakaa pamoja ili tuone vipi tunalitatua mapema iwezekanavyo Mhe. Mwenyekiti. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Labda ingawa imezungumzwa kuwa waathirika wakubwa zaidi wako Mkoa wa Kusini lakini mtoa hoja pale amesema imekwenda katika wilaya mbali mbali kwa Unguja na Pemba. Kwa hivyo, nafikiri kazi hii

uifanye kwa jumla sio kwa Mkoa wa Kusini tu, uifanye kwa ujumla na mtoa hoja pale asaidie hizi taarifa zimegusa katika maeneo gani ya wilaya gani na mikoa gani mengine. Mhe. Salmin Awadh Salmin.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyotangulia kusema kwamba walioathirika karibu wananchi wengi, yaani nimepata taarifa mpaka Pemba wamefika, lakini walionileta malalamiko ni wa Mkoa wa Kusini.

Sasa mimi ninachotaka kusema Mhe. Mwenyekiti, kwamba siku hizi kumekuwa na watu wajanja wengi, yaani matapeli wengi. Kwa hivyo, serikali inatakiwa iwe makini sana juu ya watu wa aina hii, kwa sababu ni aibu kuona kwamba kama mtu yule amekusudia kweli kuwatapeli wananchi na anakwenda kuzikabidhi fedha katika Ofisi za Mikoa na Wilaya.

Kwa kweli ni jambo la hatari sana na kwa sababu serikali hapa haiwezi kukwepa na kama ingekuwa wajasiriamali wale wameitwa pembeni, yaani katika nyumba za pembeni pale serikali ingekuwa haihusiki, lakini wamekuja katika Ofisi za Mikoa na hizi ni ofisi za serikali na fedha zile amelipa pale na stakabadhi wanazo. Mhe. Mwenyekiti, serikali lazima iwe makini sana juu ya watu wana aina hii na wala wasivamie watu tu ni lazima wawe makini. *(Makofi)*

Lakini la mwisho Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri anieleze kwamba pamoja na kuwa watakaa na kuzungumza juu ya suala hili. Kwa hivyo, mimi nataka kujua ni lini suala hili watakaa na kulishughulikia na kwa kuwa mimi ndiye niliyewasilisha hapa wananipa *feedback* juu ya utekelezaji wa jambo hili, ni siku gani ili tuone utekelezaji wa jambo hili na tuwape taarifa wale wananchi kama watulie au uchukuliwe utarataribu wa kuwafikisha Mahakamani wote waliohusika na kadhia hii. (*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante ni kwamba sisi baada ya kumaliza bajeti naona ni wakati muafaka wa kukaa na mimi pamoja na waziri muhusika na hata na yeye mwenyewe Mhe. Mjumbe si vibaya tukamshirikisha pia ili tuone hatua gani itakuwa ni muafaka kuchukuliwa. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Waziri nadhani ifanyike kazi hiyo na ikiwa mgeni rasmi atatakiwa tena huko au vipi. Mhe. mgeni rasmi anasema yuko tayari. *(Vicheko/Makofi).*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru na mimi. Wakati nilipokuwa nikichangia Idara ya Maendeleo ya Mifugo nilizungumzia kwa

kina zaidi jinsi ya serikali ilivyoweka maeneo kwa nia njema ya kufugia wanyama sehemu tofauti na nikajaribu kuyatolea mfano maeneo mawili. Eneo la Kitumba na Tunguu kwamba haya maeneo ile dhamira ya serikali kuyaweka, ili wananchi wetu au serikali kwa jumla iweze kufuga. Sasa maeneo yale yamekuwa yakivamiwa na watu mbali mbali.

Mhe. Waziri alipokuwa akijibu hapa kwa wastani kidogo amelitolea ufafanuzi zaidi kwamba kwa eneo la Kitumba tayari serikali inalifanyia kazi kuona wale waliovamia wanachukuliwa hatua za kisheria na kuondoka. Lakini kwa eneo la Tunguu Mhe. Waziri alinijibu kwamba Wizara ya Mifugo na Uvuvi imerejesha eneo lile katika Wizara ya Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati na tayari Wizara ya Ardhi ina mpango wa kuligawa katika sekta tofauti za serikali na watu binafsi. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, hapa naomba nipate ufafanuzi zaidi pamoja na jitihada za wizara kurejesha shamba lile la Tunguu, kwa ajili ya ardhi ile igaiwe. Kwa kweli naelewa kwamba kuna watu ambao wameanza kulichukua shamba lile kabla ya kurejeshwa Wizara ya Ardhi na kwa mujibu wa taratibu haikubaliki.

Kutokana na hali hiyo, nataka kujua kwamba wale ambao waliochukua eneo lile kabla ya kurejeshwa Wizara ya Ardhi. Vile vile kuna wale ambao sio kama waliopewa ardhi, isipokuwa wamechukua lile eneo kwa kulihodhi tu wao wenyewe na wameshajenga makaazi na maeneo mengine yako katika *foundation* na mengine hatua ya matofali manne mpaka matano.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kujua kwamba labda wizara hapa imepanga utaratibu gani kwa yule ambaye alichukua kabla ya kurejeshwa na wale ambao wamevamia kinyume na utaratibu.

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru ni kweli anavyosema Mhe. Mjumbe kwamba kuna mtu fulani amelivamia lile eneo kabla ya kulikabidhi kwa Wizara ya Ardhi. Lakini kwa taarifa tu kwamba yule mtu ameshafariki dunia na Mwenyezi Mungu amlaze mahala pema ijapokuwa amedhulumu na tayari tumeshaipelekea *notice* familia yake, ili watujibu na tumewapa muda na kuona kwamba hakuna mtu ambaye amechukua sehemu ile. Mhe. Mwenyekiti, kwa ufupi ni hivyo tu.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nimemsikia Mhe. Waziri lakini nataka nimthibitishie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, hebu hiyo simu tuizime. *(Makofi).*

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nimshukuru Mhe. Waziri pamoja na majibu yake mazuri sana na jitihada za serikali nataka nimsaidie zaidi

kwamba huu wakati ambao serikali inafanya jitihada ya lile eneo kuligawa katika utaratibu wa kisheria bado kuna wananchi wanaendelea kulivamia, yaani huu wakati serikali imo katika mipango hiyo.

Sasa kwa kusaidiana baina yake yeye na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati ambaye ni mzee wangu, basi naomba hizi jitihada za kukata lile eneo zifanyike haraka ili kuja kuondosha huo uvamizi. Kwa kweli tatizo linalojitokeza kama hapo watu wanavamia na anapokufa inakuwa tatizo na inabaki wende kwa watoto na watoto wanakwambia eneo tumerithi kwa mzee na lile eneo linaendelea kuvamiwa tena kwa nguvu sana.

Mhe. Mwenyekiti, nimuombe Mhe. Waziri pamoja na kushirikiana na Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati hizo jitihada zifanywe haraka ili lile eneo lipate stara.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo tuendelee.

Mhe. Mwenyekiti: Jitihada za haraka kwa mashirikiano zifanyike kuzuia uvamizi na eneo lile linatumika kwa mujibu wa taratibu. Tunaendelea.

Kifungu 0601	Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja	605,598,000/=
Kifungu 0701	Idara ya Mazao ya Baharini Unguja	198,745,000/=
Kifungu 0801		

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwenye mchango wangu nilielezea kuhusu ukatili wanaofanyiwa wanyama ikiwemo kupigwa, kunyimwa chakula, kunyimwa huduma za matibabu pamoja na kubebeshwa mizigo mizito. *(Makofi)*

Vile vile nilizungumzia kuhusu ukatili ambao umejitokeza hivi karibuni wa baadhi ya watu kuingia katika maeneo wanaolazwa ng'ombe na wakawachinja na baadaye wakawaachia maandishi ya kuwa ng'ombe wako ni halali kula tumemchinja kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, nilimuomba Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi au Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa sababu ndio inayolisimamia Jeshi la Polisi hapa Zanzibar na wakati kazi ya Jeshi la Polisi ni kulinda raia na mali zao. Kwa hivyo, niliomba anieleze kwamba kuna hatua gani iliyochukuliwa juu ya ukatili ule au kuna mtu gani ambaye ametuhumiwa kufanya suala lile. Lakini Mhe. Mwenyekiti, katika majibu ya Mhe. Waziri sikupata ufafanuzi. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli ni suala ambalo kwa kweli halikataliki ukatili wa wanyama upo na unakithiri siku hadi siku. Lakini kwa taarifa yake tu ni kwamba hivi sasa tunajaribu kuipitia ile sheria upya na iko kwa Mwanasheria Mkuu inaangaliwa ili kuona inajaribu kupunguza yale makali ya wafugaji. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Mjumbe awe na subra na sheria kweli tunaipitia hivi sasa na iko kwa Mwanasheria Mkuu na itakapokuwa tayari basi tutakuja kuileta ili ionekane hapa, nashukuru.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ukatili huu ni mkubwa na unarudisha sana maendeleo ya wafugaji. Kwa mfano mfugaji anapokwenda kwenye eneo lake ambalo analaza ng'ombe na kumkuta ng'ombe wake amechinjwa na hakuchukuliwa hata sikio kama tukasema ni mwizi na akaekewa maandishi kwamba ng'ombe wako ni halali kula na hali hii inasikitisha Mhe. Mwenyekiti.

Vile vile kama nilivyosema mwanzo kwamba Jeshi la Polisi kazi yake ni kulinda raia na mali zao na tokea kitendo hichi kitokee ni zaidi ya miezi 6 na serikali haijatoa kauli yoyote. Kwa mara ya mwisho Mhe. Mwenyekiti, mimi nilipokuwepo Pemba alichinjwa ng'ombe na maandishi yaliyoachwa ni kuwa ng'ombe wako ni halali kula na zoezi hili linaendelea. Kutokana na hali hiyo, inathibitisha kama ule ukatili unaendelea kwa *message* iliyoachwa na niliandika swali na kulileta Barazani lakini kwa bahati mbaya halijaletwa mpaka leo na ndipo nilipochangia hapa. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri au serikali kwa jumla itoe kauli na inawaambia nini wafugaji juu ya ukatili huu unaofanywa ukizingatia wafugaji wengine wanategemea ile mifugo kwa ajili ya kuendesha maisha yao. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, mimi binafsi ng'ombe huyo wa mwisho niliyemkuta amechinjwa na ikawekwa *message* hiyo ni ng'ombe wa mtu maskini sana ambaye ng'ombe yule alimtegemea kwa ajili ya kubebea mizigo akapata angalau mafuta ya taa na wanawe. Sasa leo amemkuta amechinjwa na kuambiwa kwamba kula ng'ombe wako ni halali na uwaambie wenzako kwamba zoezi linaendelea. Lakini mpaka leo hatujasikia kauli ya serikali kuhusu hili. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri kwamba wana kauli gani ambayo wanayowaambia wafugaji juu ya hili. *(Makofi).*

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo mazuri ya Mhe. Waziri naomba nielezee kwa ufupi hoja ya Mhe. Mwakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba ukatili wanaofanyiwa wanyama hasa ng'ombe unasikitisha sana na lazima nimpongeze Mhe. Mwakilishi kwa hatua anazozichukua katika kuhakikisha kwamba tunapambana na ukatili huu. Vile vile na mimi nataka nimhakikishie kwamba serikali kupitia Jeshi la Polisi tunazidi kujipanga zaidi kupambana na ukatili huu, tumeuona na kweli upo na tayari maagizo yametolewa kwa Wakuu wa Polisi wa Mikoa na Wilaya kuchukua kila hatua kwa ajili ya kupambana na ukatili huu wa mifugo, wizi wa mifugo pamoja na wizi wa bidhaa nyengine za kilimo. Kwa kweli jambo hili limezungumzwa sana ndani ya serikali na tayari limeshatolewa maelekezo, ili utekelezaji na usimamizi mzuri uendelee kwa nia ya kudhibiti ukatili huu.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi akubaliane nasi kwamba Jeshi la Polisi litafanya kila jitihada kuwatia mbaroni wale wote wanaofanya ukatili huu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia Baraza hili natoa taarifa kwa Kamishna wa Jeshi la Polisi Zanzibar azidi kuchukua jitihada za ziada kuhakikisha kwamba wale wote ambao wanashiriki katika ukatili wa mifugo pamoja na wizi wa mifugo na hata wizi mwengine yeyote. Kwa hivyo, hatua zinazofaa zichukuliwe kwa mujibu wa sheria, kwa ajili ya kuwasaidia zaidi wananchi wetu katika kuhakikisha kwamba wanaendeleza jitihada zao za mifugo, kuimarisha kilimo pamoja na kuweza kufanya shuguli zao za kila siku za maisha bila ya bughudha wala tabu ya wezi hao.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi kwamba tukubaliane na kumwambia kwamba jambo lake tunalipokea na kulifanyia kazi ili jambo hili liweze kuwa historia katika nchi yetu.

Mhe. Salma Mohamed Ali: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante. Tunaendelea.

Kifungu 0801	Idara ya Uzalishaji Wanyama Unguja	565,637,000/=
Jumla ya Fungu		**3,611,000,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

Kifungu 0016	Idara ya Maendeleo ya Uvuvi Unguja	100,000,000/=
Kifungu 0201	Idara ya Mipango Sera na Utafiti	200,000,000=
Kifungu 0601	Idara ya Maendeleo ya Mifugo Unguja	230,000,000/=

Kifungu 0701	Idara ya Mazao ya Baharini Unguja	437,600,000/=
Kifungu 0801	Idara ya Uzalishaji Wanyama Unguja	100,000,000/=
Jumla ya Fungu		**1,067,600,000/=**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Mifugo na Uvuvi: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko. Sasa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio hayo.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, niwahoji wale wanaokubaliana na makisio hayo wanyanyue mikono, wanaokataa, waliokubali wameshinda. *(Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunashukuru na tunaendelea.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Kilimo na Maliasili

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, sasa naomba nimkaribishe Mhe. Waziri wa Kilimo na Maliasili. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe, najua mumempigia makofi mengi kwa sababu ndio *spare part* yetu hii. *(Vicheko/Makofi)*

Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati (Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili): Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu, likae kama Kamati kwa ajili ya kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kazi za Kawaida na Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, sitasoma hotuba yote kama walivyogaiwa Waheshimiwa Wajumbe, na badala yake nitawasilisha muhtasari wa hii hotuba na Waheshimiwa Wajumbe watapata nafasi kusoma kwenye kitabu.

Mhe. Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuibariki nchi yetu kuwa na amani na utulivu, na kwa kutuwezesha kufikia siku ya leo tukiwa wazima na wenye afya njema, ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar ambao wengi wao ni wakulima.

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuijaalia nchi yetu kuanza matayarisho ya kuadhimisha miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar tukiwa na umoja na mshikamano, ambapo kauli mbiu yake "Tudumishe Amani na Umoja, Tulete Maendeleo – Mapinduzi Daima". Kauli mbiu hii inabeba ujumbe mzito kwa wananchi wote wa Zanzibar, katika kutekeleza wajibu wao wa kudumisha amani na kulinda Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964.

Mhe. Spika, nachukua fursa hii kumpongeza kwa dhati Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kusimamia vyema utekelezaji wa ILANI ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010 - 2015; katika kuendeleza kwa vitendo Mapinduzi ya kilimo yenye dhamira ya kuwaendeleza wakulima na kuongeza tija katika sekta ya kilimo.

Mhe. Spika, pia nazipongeza juhudi za Mhe. Rais Dkt. Shein kwa kuendeleza Sekta ya Kilimo. Juhudi hizo zimeonekana katika kazi zake za kufuatilia kwa karibu utendaji wa taasisi za serikali kupitia maagizo, maelekezo, ziara zake za Mikoa yote ya Zanzibar na majadiliano ya ana kwa ana na watendaji. Hatua hizo zimeweza kuimarisha ufanisi katika utendaji, uwajibikaji, usimamizi na ufuatiliaji wa karibu wa majukumu ya wizara na taasisi za serikali.

Mhe. Spika, napenda kuwapongeza viongozi wakuu wa kitaifa wakiwemo Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad, Makamu wa Kwanza wa Rais, na Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar kwa juhudi zao za kuhamasisha na kutoa miongozo katika kuendeleza sekta ya kilimo kupitia ziara zao za mikoa, taasisi na maeneo yanayohusiana na sekta ya kilimo.

Mhe. Spika, napenda kuchukua fursa hii pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya kudumu ya Baraza la Wawakilishi ya Fedha, Biashara na Kilimo sambamba na kumpongeza Mwenyekiti wake Mhe. Salmin Awadh Salmin Mwakilishi wa Jimbo la Magomeni na Mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM,

kwa kuchaguliwa tena kuiongoza Kamati hii. Hii inadhihirisha kwamba utendaji wake mahiri na imara katika kutekeleza majukumu yake. Mungu ampe uwezo zaidi wa kusimamia na kutekeleza ipasavyo majukumu yake ya kila siku.

Mhe. Spika, napenda pia kuipongeza na kuishukuru Kamati hii kwa miongozo na ushauri iliyoipa Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya mwaka 2012/2013. Aidha, tunaishukuru Kamati kwa maelekezo yao waliyotupa katika maandalizi ya bajeti ya Wizara ya mwaka 2013/2014. Napenda kulihakikishia Baraza lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati yamezingatiwa katika bajeti hii .

Mhe. Spika, naomba pia nikupongeze tena wewe binafsi kwa umahiri wako katika kuliongoza Baraza lako Tukufu ambalo linatoa maamuzi mazito katika kusimamia demokrasia na utawala bora nchini, na kwa kadumisha mshikamano katika Baraza. Vile vile, nawapongeza Wenyeviti wa Kamati zote za Baraza lako Tukufu kwa kuendesha na kusimamia Kamati za Baraza kwa ufanisi.

Mhe. Spika, natoa shukrani na pongezi za pekee kwa wananchi wa Jimbo langu la Jang'ombe kwa kuendelea kunipa mashirikiano na kuwa na imani na mimi katika kusimamia na kuleta maendeleo ya jimbo hili. Nawaahidi kwamba nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote kadri Mwenyezi Mungu atakavyonipa uwezo. *(Makofi)*

UKUAJI NA MCHANGO WA SEKTA YA KILIMO KATIKA PATO LA TAIFA

Mhe. Spika, Sekta za Kilimo na Maliasili bado zinaendelea kuwa ni mhimili mkuu wa uchumi wa Zanzibar. Sekta hizi zinatoa mchango wa moja kwa moja katika kujikimu kimaisha, kuwa na uhakika wa chakula na lishe bora kwa wananchi walio wengi vijijini na mijini. Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 sekta hizi zilichangia asilimia 30.2 ya Pato la Taifa na inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar wanategemea sekta hizi kwa kuwapatia ajira na mapato.

Mhe. Spika, mwaka 2012/2013, ukuaji wa Sekta ya Kilimo umeshuka kwa asilimia 1.3 kutoka asilimia 2.7 ya mwaka 2011. Hali hii imetokana na ukame na kupungua kwa maeneo yaliyolimwa kwa baadhi ya mazao makuu ya chakula ikiwemo muhogo, ndizi na mahindi.

HALI YA UZALISHAJI

Mhe. Spika, msimu wa kilimo wa mwaka 2012/13 unaonesha kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo hasa ya chakula ukilinganisha na mwaka 2011/2012. Zao la muhogo limeshuka kutoka tani 273,342 mwaka 2011 hadi tani 192,072.68, ndizi kutoka tani 110,250 mwaka 2011 hadi tani 97,934.5 mwaka 2012, mpunga kutoka tani 23,702 mwaka 2011 hadi tani 6,372.1 mwaka 2012, viazi vitamu kutoka tani 92,715 mwaka 2011 hadi tani 31,767.3 mwaka 2012 na zao la mahindi kutoka tani 3,281 mwaka 2011 hadi tani 856.6 mwaka 2012. (Kiambatisho Nam. 1). Mhe. Spika, maelezo zaidi yanapatikana katika *paragraph* ya 1.15 na 1.16

Mhe. Spika, sababu zilizochangia kupungua kwa uzalishaji ni pamoja na:

- Upungufu wa eneo lililolimwa kwa mazao ya muhogo, migomba na viazi vitamu kwa mwaka 2012/2013 kutokana na uvamizi wa maeneo ya kilimo na wakulima kujikita zaidi katika uzalishaji wa mazao ya mananasi na mboga mboga;
- Upungufu wa mvua uliosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa,
- Maradhi, wadudu waharibifu wa mazao na upungufu wa rutuba katika maeneo ya kilimo;

Mhe. Spika, takwimu zinaonesha kwamba wakulima wengi waliongeza nguvu katika uzalishaji wa mazao ya mboga mboga na mananasi na hiyo yalipelekea kuongezeka kwa uzalishaji mazao hayo. Uzalishaji wa mbogamboga umeongezeka kutoka tani 8000 (ekari 3,202.7) mwaka 2011/2012 na kufikia tani 18,232.5 (ekari 9,909) mwaka 2012/2013. Kwa upande wa zao la mananasi uzalishaji umeongezeka kutoka tani 3,309 mwaka 2011/2012 hadi kufikia tani 12,115.5 mwaka 2012/2013. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya pembejeo za kisasa na taaluma bora za uzalishaji.

Mhe. Spika, taarifa za hali ya hewa katika kipindi cha masika 2012/2013 ni za kutia moyo hasa kwa kilimo cha mpunga wa kutegemea mvua. Takwimu zinaonyesha kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la mvua za masika mwaka 2012/2013 ambazo zimenyesha zaidi ya wastani wa kila mwaka. Hali hii imeimarisha kwa kiasi kikubwa ukulima wa mpunga wa kutegemea mvua ambapo sehemu kubwa ya kilimo hicho kimeimarika vizuri na kuleta matumaini ya kupata mavuno mazuri. Kutokana na hali hio, kwa msimu wa mwaka 2012/2013, mavuno yanakadiriwa kufika zaidi ya tani 30,000 za mpunga.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imeendelea na utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo ikiwemo mbegu bora, mbolea, dawa za magugu na huduma za matrekta kwa azma ya kuendeleza zao la mpunga na mazao mengine ya chakula ili kuongeza uzalishaji wa chakula na kudhibiti mfumuko wa bei nchini. Viwango vya pembejeo vilivyosambazwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili vimeelezwa kwenye paragraph 1.18, 1.19 na 1.20.

Mhe. Spika, kwa upande wa utoaji wa pembejeo, kwa mwaka wa 2012/2013, Wizara imeleta na kusambaza kwa wakulima tani 900 mbolea ya kukuzia (Urea), tani 500 za mbolea ya kupandia (*TSP*), tani 535 za mbegu na lita 30000 za dawa ya magugu. Kati ya tani hizo za mbegu, tani 300 zimezalishwa kwa mikataba na wakulima na tani 235 ziliagizwa kutoka Tanzania Bara. Pembejeo hizo zote zilizosambazwa vituoni na kuuzwa kwa wakulima, na hadi msimu huu kumalizika, tani 85 za urea, tani 172 za *TSP*, tani 29 za mbegu na lita 340 za dawa ya magugu zimebaki ghalani, na zinatarajiwa kutumika katika msimu wa Vuli katika mabonde ya umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, wizara inafahamu kwamba kuna baadhi ya wakulima wanalalamika juu ya uhaba wa dawa ya gugu, lakini serikali haiwezi kuagiza dawa ya magugu zaidi ya kiwango cha lita 30,000 kwa mwaka kwa sababu za kimazingira, afya za watu na viumbe wengine. Tunaomba tufahamu kwamba Zanzibar ni nchi ya visiwa vidogo vidogo na maji yake pia yanatoka chini ya ardhi kwa matumizi ya binaadam na viumbe hai wengine.

Kwa hivyo kutumia madawa mengi ya sumu ni hatari kwetu sisi, lakini pia Sheria za Kimataifa haziruhusu kuagizia zaidi ya kiwango maalum kilichowekwa. Wizara ya Kilimo na Maliasili inafanya juhudi ya kuwaelimisha wakulima juu ya kutumia mbinu nyingine za kilimo bora katika kupunguza magugu katika zao la mpunga.

Mhe. Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwashauri na kwa nguvu zetu zote kuwaomba wakulima wachache wanaotumia vibaya fursa ya kupata pembejeo kwa njia ya ruzuku lakini badala ya kutumia pembejeo hizo kwa kilimo cha mpunga ili kutimiza ile azma ya Serikali ya kuongeza uzalishaji, wakulima hao huamua kuuza pembejea hizo kwa magendo au mbegu ya mpunga kuitwanga na kuitumia kwa chakula badala ya mbegu. Kufanya hivyo ni kinyume cha utaratibu wa Serikali na ni kosa. Suala la kutumia mbegu kwa chalula ni kuhatarisha maisha yao na ya familia zao kwani mbegu ya mpunga huchanganywa na dawa ya sumu kwajili ya kuihifadhi na wadudu.

Mhe. Spika, napenda kuwahakikishia wakulima wote kupitia Baraza lako kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo na Maliasili itaendelea na utoaji wa ruzuku kwa pembejeo za kilimo

hasa zao la mpunga ikiwemo mbolea, dawa za kuulia magugu, mbegu bora pamoja na huduma za matrekta. Aidha, wizara inaendelea na maandalizi ya msimu ujao wa kilimo na kuimarisha utaratibu wa kuwapatia wakulima pembejeo na huduma za matrekta kwa wakati.

MUELEKEO WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO NA MALIASILI 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea kusimamia na kutekeleza malengo ya Dira ya 2020, ILANI ya Uchaguzi ya CCM 2010 – 2015, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini (MKUZA II), Malengo ya *Milenia* (*MDGs*), Mipango na Mikakati ya Kisekta pamoja na Mpango wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo (*ATI*).

Mhe. Spika, muelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2013 2014 kama ilivyoelezwa kwenye *paragraph* 1.23.

Mhe. Spika, muelekeo wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2013/2014 ni kama ifuatavyo:

- Kuimarisha uzalishaji wa zao la karafuu kwa kuendeleza utoaji wa elimu ya ukulima bora wa mikarafuu kupitia skuli za wakulima; kuendelea kutoa miche ya mikarafuu 1,000,000 na kuwapatia wakulima bila malipo na kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa wakulima wa mikarafuu.
- Kuongeza uzalishaji wa mpunga nchini kupitia uimarishaji wa miundombinu ya umwagiliaji maji na matumizi ya utaalamu katika kilimo cha mpunga;
- Kuimarisha utoaji wa huduma za matrekta na zana nyengine za kilimo, elimu kwa wakulima na kuongeza upatikanaji wa pembejeo za kilimo kwa wakati zikiwemo, mbegu bora, mbolea, dawa za kuzuia magugu na wadudu waharibifu;
- Kuimarisha uzalishaji na usindikaji wa mazao maalum ya Kilimo na Maliasili *(Specific Value Chain Development)* ikiwemo Muhogo, Viungo, Matunda na Mboga mboga.
- Kushajiisha uibuaji wa miradi ya kuongeza kipato katika Sekta ya Misitu na Maliasili ikiwemo uzalishaji wa asali na utalii wa kimaumbile *(eco-tourism)* katika maeneo ya Jozani, Ngezi, Masingini na Kiwengwa. Lengo ni kupunguza ukataji wa miti ambao utapelekea kupungua kwa hewa ukaa *(carbondioxide);*
- Kuhamasisha ushiriki wa vijana katika kilimo cha biashara

- Kuendeleza utafiti na uibuaji wa teknolojia mpya za uzalishaji katika kupambana na changamoto za kilimo zikiwemo wadudu waharibifu, maradhi na mabadiliko ya hali ya hewa;
- Kushajiisha upandaji wa miti na njia bora za utunzaji, uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili.
- Kuendeleza utoaji wa mafunzo ya Kilimo na Mifugo kupitia Chuo cha Kilimo Kizimbani na Skuli za Wakulima.
- Kuratibu na kuimarisha kazi za uhakika wa chakula na lishe kitaifa ikiwa ni pamoja na kukusanya na kutoa taarifa za tahadhari ya mapema na kusimamia uanzishaji wa maghala ya chakula cha akiba.
- Kuimarisha mfumo wa kisheria na kisera ili uendane na mabadiliko ya kiuchumi na kimazingira kwa kufanya mapitio ya Sera za kilimo na misitu, na kutayarisha Sheria za Uhifadhi wa Mimea na Sheria ya mbegu;
- Kusimamia upatikanaji wa hati miliki za mali za Serikali zilizopo chini ya Wizara ya Kilimo na Maliasili;
- Kuhamasisha jumuiya za wakulima ili washiriki kikamilifu katika shuguli za kilimo na hatimae kurahisisha utoaji wa huduma kwa wakulima;

TAARIFA YA UTEKELEZAJI MWAKA 2012/2013

MAPATO NA MATUMIZI

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ilikadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 426,000,000/=. Hadi kufikia mwezi wa Juni 30, 2013, wizara imekusanya shilingi 550,216,660/= sawa na asilimia 129 ya makadirio ya lengo.

MATUMIZI YA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ya Kilimo na Maliasili iliidhinishiwa jumla ya shilingi 11,878,194,460/= kwa kazi za kawaida na sh. 388,800,000 ikiwa ni Ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani. Hadi kufikia Juni, 2013, fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni shilingi 11,219,804,188/= sawa na asilimia 94. Kwa upande wa Chuo cha Kilimo ruzuku ya shilingi 288,800,000/= imepatikana ikiwa ni sawa na asilimia 94 (Kiambatisho Nam. 14).

Mhe. Spika, katika kutekeleza kazi za maendeleo, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, iliidhinishiwa jumla ya shilingi 2,090,000,000/= ikiwa ni mchango wa SMZ. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2013, fedha zilizopatikana ni shilingi 463,211,520/= sawa na asilimia 22.

Kwa upande wa washirika wa maendeleo, fedha zilizotengwa kwa mwaka 2012/2013 ni shilingi 9,417,116,000/=. Hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013, wizara imepata jumla ya shilingi 2,787,620,584 sawa na asilimia 30 ya lengo. (Kiambatisho Nam. 11).

MAKADIRIO YA MAKUSANYO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inakadiriwa kukusanya mapato ya sh. 748,000,000/= kwa mwaka wa fedha 2013/2014 (Kiambatisho Nam. 13). Aidha, wizara pia inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi 30,320,998,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 12,069,000,000/= ni matumizi ya kazi za kawaida na shilingi 500,000,000/= ruzuku Chuo cha Kilimo Kizimbani (Kiambatisho Nam. 16) na shilingi 17,751,998,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi 14 ya maendeleo (kati ya hizo Tsh. 1,560,000,000 ni mchango wa SMZ na Tsh. 16,191,998,000 ni mchango wa washirika wa maendeleo *(Kiambatisho Nam. 10).*

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2012/2013 imepata mafanikio yafuatayo:

- Skuli mpya 300 za wakulima zimeanzishwa kupitia Programu za kuendeleza Huduma za Kilimo na Mifugo *ASSP* na *ASDP-L*. Kwa ujumla idadi ya skuli za wakulima Zanzibar hivi sasa ni 1,200,

- Chuo cha Kilimo Kizimbani kimeanza kutoa mafunzo katika ngazi ya Diploma ambapo wanafunzi 49 (wanawake 28 na wanaume 21) wameanza mafunzo hayo katika muhula wa masomo wa 2012/2013. Aidha, kupitia Programu za *ASSP* na *ASDP-L* Wizara imekamilisha ujenzi wa dakhalia la kisasa ambalo limeanza kutumiwa na wanafunzi 49 wanaosoma Diploma ya Kilimo na Mifugo,

- Kuimarisha ukulima wa kilimo cha mpunga kwa kuwapatia wakulima pembejeo bora ikiwemo mbegu, mbolea, dawa na huduma za matrekta kwa njia ya ruzuku ili kuongeza uzalishaji na tija;

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA (2012/2013) NA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014

Mhe. Spika, utekelezaji wa kazi za Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara na taasisi zake kwa mwaka 2012/2013 pamoja na malengo ya mwaka 2013/2014 ni kama ifuatavyo:

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, majukumu ya Idara hii ni kusimamia na kuratibu Sera, Sheria, Mikakati, Mipango ya Maendeleo na Utafiti. Idara pia inaratibu mashirikiano ya Wizara na taasisi za ndani na nje ya nchi ikiwemo Washirika wa Maendeleo na Sekta Binafsi.

MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Idara ilipanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kuimarisha mifumo ya Kisera, Sheria, Mikakati na Mipango/Miradi ya Wizara ili kukabiliana na changamoto zilizopo kwa kufanya mapitio ya Sera za Kilimo, Karantini na Mbegu, Mswada wa Sheria ya Haki Miliki ya Wagunduzi wa Mbegu, Sheria na,

- Kanuni za Misitu; Mkakati wa Mageuzi ya Kilimo (*ATI*), na Mpango wa Utekelezaji wa Sera ya Masoko (*ZAMP IP).* Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa juu ya matukio muhimu ya kisekta na Wizara *(M & E),* ikiwemo mawasiliano na utoaji taarifa kwa njia ya tovuti ***(www.kilimoznz.or.tz);*** kutoa nakala 2,000 za Jarida la Mkulima,

- Kuimarisha mashirikiano kati ya Wizara na taasisi za ndani, za kikanda na nje ya nchi; ikiwemo kukamilisha na kuratibu mfumo wa pamoja wa kitaasisi katika Sekta ya Kilimo *(ASP-Z),* kushiriki katika Vikundi Kazi vya kitaifa, mikutano na makongamano ya kitaifa; kikanda na kimataifa,

- Kuimarisha tafiti za kijamii, kiuchumi na kisayansi ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo kwa kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya maeneo ya kipaumbele ya utafiti; na Kuandaa warsha na kutoa Toleo la Tatu la Utafiti wa Kilimo ***(3rd Annual Agricultural Research Proceeding)*** na Kuendelea kusimamia programu na miradi mipya na inayoendelea.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, mwaka wa fedha 2012/2013 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Sera ya Masoko imekamilika na Rasimu ya Sera ya Misitu na Rasimu ya Sheria ya Wagunduzi wa aina mpya za mbegu za mimea zimekamilika kwa ngazi ya Wizara.

- Mapitio ya Sheria ya Utibabu wa mimea na ukaguzi wa mazao yamefanyika kwa mashirikiano na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu.

- Mafunzo ya Tathmini ya Sera kwa wafanyakazi 25 kutoka Wizara ya Kilimo na Maliasili na Taasisi nyengine za Serikali yametolewa kwa mashirikiano na *USAID*, Utayarishaji wa Programu ya Kuendeleza Mazao ya Matunda na Viungo unaendelea.

- Kazi za ukusanyaji wa Takwimu za bidhaa za kilimo katika masoko na za uzalishaji wa mazao ya kilimo zimefanyika na zinaendelea. Aidha, mradi wa uimarishaji wa ukusanyaji wa takwimu za mazao ya kilimo umeanza kwa kuwafundisha mabwanashamba 25 (12 Pemba na 13 Unguja).

- Kukijengea uwezo kitengo cha habari cha Wizara kwa kukipatia vifaa vya kisasa ikiwemo ***Digital Voice Recorder, Digital Camera*** na ***Video Moving Camera***.

- Uingizwaji wa taarifa katika Tovuti ***(Website)*** ya Wizara ulifanyika kwa lengo la kuelimisha wadau mbali mbali. Aidha, vipindi viwili vya TV na vitano vya redio vimetayarishwa na kurushwa hewani.

- Jumla ya nakala 1500 za Jarida la mkulima limechapishwa na kusambazwa kwa wakulima na wadau wengine.
- Wizara imeshiriki katika vikao vya mashirikiano na taasisi za ndani ya nchi, kikanda na nje ya nchi kwa lengo la kuimarisha uhusiano.

- Mkutano wa mapitio ya tafiti ***(3rd Annual Agricultural Research Review Meeting)*** umefanyika na kuhudhuriwa na wajumbe kutoka taasisi zinazojihusisha na kazi za utafiti na maendeleo za Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Idara iliendelea kusimamia utekelezaji wa programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo kama ifuatavyo:

- Programu ya Kuimarisha Huduma za Kilimo–*ASSP*, *(Kiambatisho Nam. 2)*
- Programu ya Kutoa Huduma za Mifugo *ASDP-L (Kiambatisho Nam. 3).*

- Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Masoko ya Kilimo na kuongeza Thamani ya Mazao (MIVARF) (Kiambatisho Nam. 4).
- Programu ya Usarifu wa Mazao *(Kiambatisho Nam. 5).*

MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti kwa mwaka wa 2013/2014 pamoja na malengo iliyojipangia, Idara itasimamia utekelezaji wa Programu mpya ya Kusaidia Kilimo na Uhakika wa Chakula Duniani *(GAFSP).*

Lengo kuu la Programu hii kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za mpunga, na kutumia teknologia ya uzalishaji ambayo itapelekea kuongezeka kwa uzalishaji wa zao la mpunga na kipato kwa wakulima na kuwa na uhakika wa chakula. Katika kutekeleza Programuhii, kwa mwaka 2013/2014, kazi zifuatazo zinatarajiwa kufanyika:

- Kujenga mitaro katika eneo la hekta 115 Unguja na hekta 65 Pemba.
- Kuchimba visima vitano na kuviwekea pampu.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2013/2014 Idara imelenga kutekeleza yafuatayo:

- Kwa kipindi hiki, Idara itafanya mapitio ya Sera ya Kilimo na Misitu, Sheria ya Uhifadhi wa mimea pamoja na kutayarisha Sheria mpya ya mbegu.

- Kuimarisha mfumo wa ukusanyaji, uchambuzi na utoaji wa taarifa juu ya matukio muhimu ya kisekta na Wizara *(M & E)*, ikiwemo mawasiliano na utoaji taarifa kwa njia ya tovuti *(www.kilimoznz.or.tz)*,

- Kutoa nakala 2,000 za Jarida la Mkulima pamoja na matayarisho ya vipindi 10 vya TV na Redio juu ya elimu kwa wakulima (mpunga, matunda, karafuu na mbogamboga) na kuvirusha hewani,

- Kutayarisha makala 15 na vipeperushi 1000 kwa ajili ya wakulima ili kupata taarifa muhimu za kilimo cha kisasa, taarifa za masoko na matumizi ya pembejeo,
- Kukusanya taarifa na takwimu muhimu za kijamii na kiuchumi katika sekta ya kilimo, ikiwemo uzalishaji na masoko ya mazao ya chakula biashara pamoja na kukamilisha mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ukusanyaji wa taarifa.

- Kuimarisha mashirikiano kati ya Wizara na taasisi za ndani, za kikanda na nje ya nchi.

- Kuratibu mfumo wa pamoja wa kitaasisi katika Sekta ya Kilimo *(ASP-Z)* pamoja na kushiriki katika vikundi Kazi vya Kitaifa, mikutano na makongamano ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa,

- Kuimarisha tafiti za kijamii, kiuchumi na kisayansi ili kuongeza uzalishaji na tija katika kilimo kwa kutoa ushauri wa kitaalamu juu ya maeneo ya kipaumbele ya utafiti. Aidha, Idara itaandaa tafiti mbili ikiwemo:

    - Tafiti juu ya mafanikio na changamoto zinazokabili uendelezaji wa zao la karafuu.

    - Tafiti juu ya mfumo wa uingizaji na usambazaji wa pembejeo za kilimo.

- Kuandaa warsha na kutoa Toleo la Nne la Utafiti wa Kilimo ***(4th Annual Agricultural Research Meeting).***

- Kuratibu na kusimamia miradi inayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara iliombewa Tsh. 634,523,647 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 628,350,735 sawa na asilimia 99 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 idara inaombewa jumla ya Tsh.449,548,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kusimamia rasilimali watu na kutoa huduma za utawala katika Wizara, ikiwa ni pamoja na masuala ya ajira, mafunzo, maslahi ya wafanyakazi na uwekaji wa kumbukumbu. Aidha, Idara inaratibu masuala mtambuka kama Ukimwi, jinsia, kusimamia utunzaji na uhifadhi wa mali za Serikali, utoaji wa huduma za manunuzi na uhifadhi wa vifaa.

MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka 2012/2013 Idara ilipanga malengo yafuatayo:

- Kukusanya mapato yanayokadiriwa kufikia Tsh 426,000,000.
- Kuendelea kuhakiki mali za Serikali zilizochini ya Wizara na kupata hati miliki.
- Kujenga uwezo wa kitaaluma kwa wafanyakazi.
- Kusimamia maslahi na kuweka mazingira mazuri ya kazi.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Jumla ya wafanyakazi 106 wa Wizara wamepatiwa mafunzo, kati ya hao, cheti 19, Diploma 41, Shahada ya kwanza 11, stashahada ya juu 3, Shahada ya Pili 13, na 19 mafunzo ya muda mfupi,

- Jumla ya wafanyakazi saba (wanawake 4 na wanaume 3) wamefariki dunia. Aidha, wafanyakazi 50 wamestaafu kwa hiari na kwa mujibu wa Sheria na 36 wamekwenda likizo bila ya malipo.

- Upimaji na uchoraji wa Ofisi ya Utibabu wa mimea na mashamba ya utafiti ya Matangatuani umefanyika,

- Mapitio ya upimaji na uchoraji wa mipaka ya maeneo ya Chuo cha Kilimo Kizimbani na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Kizimbani pamoja na kupatiwa ramani na hati miliki mpya kwa maeneo hayo umekamilika,

- Jumla ya TSh. 526,708,150 sawa na asilimia 124 zimekusanywa.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, Kwa mwaka wa 2013/2014 Idara imepanga kutekeleza malengo yafuatayo:

- Kuendelea na uhakiki wa mali za Serikali zilizo katika Wizara na kuzipatia hati miliki,

- Kuwajengea uwezo wa kitaaluma wafanyakazi 15 wapya na 106 wanaoendelea,

- Kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi,

- Kuratibu utaratibu wa manunuzi ya Wizara,

- Kuratibu ukusanyaji wa mapato ambayo yanakadiriwa kuwa ni Tsh 748,000,000,

- Kuratibu maadhimisho ya miaka 50 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar kwa upande wa Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara iliombewa Tsh. 718,767,623 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013 Idara imepatiwa jumla ya Tsh 712,520,052 sawa na asilimia 99 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya Tsh. 1,130,634,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA KILIMO

Mhe. Spika, idara hii ina majukumu ya kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo kwa wakulima, uhifadhi na ukaguzi wa mazao na kutoa mafunzo kwa wazalishaji.

MALENGO YA IDARA YA KILIMO MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/13, idara iliwekewa malengo yafuatayo:

- Kuhakikisha upatikanaji wa mbegu ya mpunga tani 570, mbolea tani 1,500 (UREA 1,000 na TSP 500) na dawa ya kuulia magugu lita 30,000 ili kuongeza uzalishaji,

- Kutoa huduma za kilimo na kusimami ukulima wa mpunga ekari 40,000,

- Kuwaelimisha wakulima 1,500 juu ya mbinu za kilimo bora,

- Kudhibiti maradhi ya mimea na wadudu waharibifu wa mazao,

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa mabibi/Mabwana shamba 95 juu ya mbinu bora za kilimo,

- Kuzalisha tani nane za mbegu ya mahindi tani mbili za mbegu ya mtama na tani 570 za mbegu ya mpunga ikiwemo *NERICA*,

- Kuzalisha mbegu ya mpunga kwa mikataba ya wakulima na mashamba ya JKU,

- Kutayarisha lita 500 za dawa ya asili kwa ajili ya kuulia wadudu waharibifu wa mimea na kupunguza matumizi ya dawa za viwandani,

- Kuyafanyia matengenezo matrekta 46 na power tiller 75 kwa ukulima wa mpunga wa 2012/2013,

- Kutoa mafunzo kwa mafundi na madereva 100 wa matrekta na ***Power Tillers.***

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2012/13

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara imetekeleza kazi zifuatazo:

- Jumla ya tani 535 za mbegu ya mpunga zimesambazwa kwa wakulima (sawa na asilimia 94 ya lengo). Kati ya mbegu hizo, tani 300 zimenunuliwa kutoka Tanzania Bara na tani 235 zimenunuliwa kupitia wakulima wa mikataba Zanzibar. Aidha, tani tano za mbegu ya kunde zimenunuliwa kutoka Tanzania Bara na kuuzwa kwa wakulima,

- Tani 500 za mbolea aina ya TSP na tani 1000 aina ya *UREA* na dawa ya kuulia magugu lita 30,000 zimenunuliwa na kusambazwa kwa wakulima,

- Ekari 34,317 za mpunga wa kutegemea mvua zimelimwa kwa msimu wa kilimo 2012/2013 (Pemba 20,048 na Unguja 14,269) sawa na asilimia 86 ya lengo,

- Mitego 2,239 ya kunasia nzi waharibifu wa matunda imesambazwa kwa wakulima wa Wilaya 9 za Pemba na Unguja. Kazi za uangamizaji wa nzi waharibifu wa matunda zinaendelea na tathmini iliyofanyika hivi karibuni inaonesha kuwa uharibifu wa matunda

unaosababishwa na nzi hao umeshuka kutoka asilimia 75 mwaka 2007 hadi kufikia asilimia 25 mwaka 2012,

- Ekari 4 za mbegu za mahindi, 2 mtama na 20 za mpunga wa *NERICA* zimepanda katika kituo cha uzalishaji mbegu Bambi,

- Mafunzo kwa wakulima 80 (35 Pemba na 45 Unguja) ya udhibiti wa wadudu na maradhi ya mimea kwa kutumia dawa za asili yametolewa Pemba na Unguja,

- Matrekta 37 (Pemba 13 na Unguja 24) yametengenezwa katika msimu wa kilimo wa mwaka 2012/2013,

- Mafunzo yametolewa kwa mafundi na madereva 60 (Pemba 20 na Unguja 40) juu ya matumizi na matunzo ya matrekta na zana zake,

- Vipindi 10 kwa njia ya Redio vimetayarishwa na kurushwa hewani kuhusu uzalishaji na uendelezaji wa mazao ya chakula, utunzaji na uhifadhi wa mazingira na uhifadhi wa misitu na maliasili zisizorejesheka. Aidha, makala tatu juu ya uzinduzi wa maabara ya Taasisi ya Utafiti Kizimbani na uzalishaji mbegu bora za muhogo yametayarishwa,

- Jumla ya miche 5000 ya minazi imeoteshwa na kuuzwa kwa wakulima kwa msimu wa Masika 2012/2013.

MALENGO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kusimamia ukulima wa mpunga ekari 35,000 kwa msimu 2013/2014 (Unguja ekari 15,000 na Pemba 20,000),

- Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Mabibi/Mabwana shamba 140 (90 Unguja 50 Pemba) juu ya mbinu shirikishi za elimu kwa wakulima,

- Kununua seti mbili (seti moja Pemba na seti moja Unguja) za Ng'ombe wa kulimia kwa ajili ya mafunzo ya ukulima kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng'ombe pamoja na kutoa mafunzo kwa wakulima 40 (20 Pemba na 20 Unguja),

- Kuzalisha tani 5 za mbegu ya Mahindi, tani 2 za mbegu ya mtama katika vituo vya Idara vya kuzalisha mbegu na tani 300 za mbegu ya mpunga kupitia kwa wakulima wa mikataba,

- Kununua na kusambaza tani 1,300 za mbolea (*TSP* tani 300 na *UREA* tani 1000), lita
  30,000 za dawa ya magugu na tani 300 za mbegu ya mpunga kutoka T.Bara,

- Kuzalisha mbegu ya mpunga aina ya *NERICA* tani 20 katika vituo vya uzalishaji mbegu Bambi na kupitia mikataba na wakulima,

- Kutengeneza matrekta 37 (13 Pemba 24 Unguja), kutoa mafunzo kwa mafundi na madereva 60 wa matrekta na kutoa huduma za matrekta kwa wakulima kwa msimu wa mpunga wa mwaka 2013/2014,
- Kuendelea na kazi za ukaguzi wa mazao yanayoingia na kutoka nje ya nchi na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima juu ya mbinu bora za kudhibiti wadudu waharibifu wa mimea na uhifadhi wa mazao,

- Kuendelea na kazi ya kusambaza na kubadilisha dawa katika mitego ya kunasia nzi waharibifu wa matunda,

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara iliombewa Tsh. 5,618,502,820, hadi kufikia mwezi Juni, 2013 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 5,113,513,078 sawa na asilimia 91 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya Tsh. 5,649,736,000/= kutoka Serikalini.

TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO

Mhe. Spika, Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ina jukumu la kubuni, kupanga na kutekeleza kazi za utafiti katika sekta za Kilimo na Maliasili na kutoa matokeo yake kwa walengwa wakiwemo wakulima, wanafunzi na wadau wengine. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo inajumuisha vituo vyote vya utafiti vilivyo ndani ya sekta ya kilimo na Maliasili.

MALENGO YA TAASISI YA UTAFITI KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Taasisi ililenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuendeleaza utafiti wa mbegu bora za mpunga, mazao ya mizizi mboga mboga na matunda ili kupata mbegu mpya zitakazotoa mazao mengi zaidi na zinazokubaliana na mazingira ya Zanzibar,

- Kufanya utafiti wa mazao ya biashara yakiwemo mazao ya karafuu na nazi,

- Kuimarisha miundombinu na wataalamu wa utafiti kwa ajili ya kuongeza uwezo wa Taasisi katika kutoa huduma za utafiti,

- Kufanya tafiti za kuendeleza misitu na matumizi bora ya maliasili zisizorejesheka,

- Kuendelea na utayarishaji wa mpango mkakati wa miaka mitano wa Taasisi ya Utafiti.

UTEKELEZAJI WA MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Taasisi imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo:

- Utafiti wa zao la mpunga uliojumuisha mbegu 76 kutoka vituo vya utafiti vya ndani na nje ya nchi vikiwemo *IRRI, Africa Rice, Vietnam* na *INGER-Africa* zimejaribiwa katika mabonde ya Mtwango, Kizimbani, Tungamaa na Mwera. Matokeo ya awali yanaonesha miongoni mwa mbegu 76 zilizofanyiwa utafiti, mbegu za aina tano (5) kutoka *IRRI* zimeonekana kufanya vizuri na utafiti kwa mbegu zilizobakia bado unaendelea,
- Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kushirikiana na Programu ya *Feed the Future (USAID)* imewapatia mafunzo wakulima 400 juu ya mbinu bora za uzalishaji wa mpunga kuanzia kutayarisha ardhi mpaka hatua ya uvunaji kutoka mabonde ya Bumbwisudi, Kilombero na Kipange,

- Utafiti kwa ajili ya kupata mbegu za muhogo zitakazostahamili maradhi ya michirizi ya kahawia ***(cassava brown streak disease)*** na zitakazokuwa na uzazi mkubwa umefanyika katika vituo vya utafiti vya Kizimbani, Matangatuani na kwa kushirikiana na wakulima wa Unguja na Pemba. Aina 13 za mbegu za muhogo zimefanyiwa utafiti huo na utafiti bado unaendelea,

- Majaribio mawili yanayojumuisha aina 20 ya mbegu za viazi vitamu vyenye viini lishe yamefanyika kwa lengo la kutafuta mbegu ambazo

zina viwango vikubwa vya uzalishaji na viini lishe. Aina 15 za mbegu hizo zimeonesha matokeo mazuri na zimechaguliwa kwa utafiti zaidi,

- Ukusanyaji na utunzaji wa viasilia vya mimea ***(germplasm conservation)*** aina 65 za mbegu za muhogo, 33 za viazi vitamu, 50 za mpunga na 36 za migomba zimefanyika katika vituo vya Kizimbani na Matangatuani,

- Mafunzo yametolewa kwa maafisa wa utafiti na Mabwana/Mabibishamba 140 (50 Pemba na 90 Unguja) juu ya udhibiti wa maradhi na wadudu waharibifu wa muhogo. Aidha, wakulima 70 wamepatiwa mafunzo juu ya matumizi ya viazi lishe,

- Jumla ya wafanyakazi 50 wa Taasisi ya utafiti walifundishwa mbinu za utafiti, uandishi na usimamizi wa miradi ya utafiti,

- Utafiti wa ukuaji wa miche ya mikarafuu kwa kutumia udongo wa (kinamo, kichanga na fuwe) pamoja na matumizi ya viwango tofauti vya maji unaendelea kwenye vitalu na katika kituo cha Matangatuani,

- Utafiti wa matumizi ya viwango tofauti vya mbolea ya samadi katika kilimo cha migomba unaendelea na takwimu za awali zimekusanywa,

- Mapitio ya ramani ya aina za udongo wa Unguja na Pemba kwa kutumia mfumo wa digitali unaendelea,

- Kazi ya utayarishaji wa Mpango Mkakati wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar inaendelea,

- Ujenzi wa maabara mpya kwa ajili ya utafiti wa mpunga na ukarabati wa maabara za udongo, *tissue culture* na usarifu wa mazao uko katika hatua ya mwisho.

MALENGO YA TAASISI KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Taasisi imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuanzisha na kuendeleza tafiti 17 za mbegu na mbinu mpya za uzalishaji wa mazao makuu ya chakula,

- Kufanya utafiti wa mbinu bora za uzalishaji wa mazao ya biashara yakiwemo mikarafuu, minazi na matumizi bora ya udongo,

- Kujenga miundombinu ya maji na uzio katika maabara mpya ya mpunga pamoja na kukarabati jengo la uchunguzi wa mimea ***(screen house)*** liliopo Kizimbani na ukarabati wa maabara ya mazao iliyoko Matangatuani Pemba na ununuzi wa vifaa,

- Kuendelea na utayarishaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano na utayarishaji wa Kanuni za Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo ili kuweka mazingira mazuri katika utekelezaji wa kazi za utafiti,

- Kuotesha miche 10,000 ya minazi katika vitalu vya Selemu na Kidichi.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/13, Taasisi iliombewa jumla ya Tsh**.** 842,307,280 kwa kazi za kawaida na Tsh. 400,000,000 kwa kazi za aendeleo. Hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013 Taasisi imepata Tsh. 834,140,250 sawa na asilimia 99 kwa kazi za kawaida na Tsh. 41,000,000 sawa na asilimia 10 kwa kazi za maendeleo zimepatikana. Kwa mwaka wa fedha wa 2013/14, Taasisi inaombewa kupata Tsh. 967,498,000 kwa kazi za kawaida na Tsh. 140,000,000 kwa kazi za maendeleo.

CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI

Mhe. Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani kina jukumu la kutoa utaalamu/mafunzo katika fani za kilimo, maliasili na mifugo katika ngazi tofauti.

MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2012/2013

Mhe. Spika, mwaka wa fedha wa 2012/2013 Chuo kimelenga kutekeleza malengo kama ifuatavyo:

- Kutoa mafunzo kwa wanafunzi 130 wa Cheti na 20 wa Diploma,
- Kujenga bweni la wanafunzi wa kike,
- Kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima wa mpunga kwa kushirikiana na Mradi wa *TANRICE II.*

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2012/2013

Mhe. Spika, mwaka wa fedha wa 2012/2013 Chuo kimetekeleza malengo yake kama ifuatavyo**:**

- Mafunzo yalitolewa kwa wanafunzi 210, kwa upande wa ngazi ya Diploma ni wanafunzi 49 (21 wanaume na 28 wanawake) sawa na asilimia 245 ya lengo, na ngazi ya Cheti ni wanafunzi 161 (63 wanaume na 98 wanawake) sawa na asilimia 124 ya lengo,

- Kazi ya kutayarisha michoro na makadirio ya ujenzi wa dakhalia itakayokuwa na ghorofa nne na vyumba mia moja na ishirini na tano (125) inaendelea.

Mhe. Spika, katika mwaka huu wa fedha 2012/2013, kwa kushirikiana na mradi wa EPINAV, Chuo pia kimetekeleza kazi zifuatazo:

- Utayarishaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano unaendelea,

- Ukarabati wa maktaba na ununuzi wa vitabu 840 na machapisho 50 umefanyika,

- Vifaa vya uchunguzi na tiba za mifugo vimenunuliwa kwa lengo la kuimarisha mafunzo katika Kitengo cha Mifugo,

- Kompyuta 10 zimenunuliwa kwa ajili ya kufundishia na kuimarisha huduma za mtandao ***(Internet)*** katika maktaba ya Chuo na ofisi ya Mratibu wa masomo,

- Ziara mbili za kimasomo kwa wafanyakazi wa Chuo cha Kilimo Kizimbani kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Kilimo - Sokoine, kutembelea vyuo vya Kilimo na Mifugo vya Tanzania Bara na ***"University of Life Sciences"*** ya Norway zimefanyika kwa lengo la kukuza uhusiano, kubadilishana uzoefu wa mbinu za usomeshaji na kuangalia uwezekano wa kuwa na miradi ya pamoja ya maendeleo.

MALENGO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo kimelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kutoa mafunzo kwa wanafunzi 184, ngazi ya Cheti 135 na Diploma 49,

- Kuendelea na kazi za ujenzi wa dakhalia moja yenye ghorofa 4 yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 500 wa kike kwa wakati mmoja,

- Kufanya ukarabati wa dakhalia mbili,

- Kutoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga wa umwagiliaji maji katika bonde moja kwa kushirikiana na Mradi wa *TANRICE II.*

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Chuo kiliombewa Tshs. 308,800,000 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013 Chuo kimepatiwa jumla ya Tshs. 288,800,000 sawa na asilimia 94 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Chuo kinaombewa jumla ya Tshs. 500,000,000 ikiwa ni ruzuku kutoka Serikalini na Tsh. 90,000,000 fedha za maendeleo kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya Chuo (Ujenzi wa bweni jipya).

IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Spika, idara ina jukumu la kulinda na kuhifadhi misitu ya asili na wanyama pori, kusimamia mashamba ya misitu na mbegu, upatikanaji wa miche bora, kuhamasisha kilimo cha biashara na kuratibu uvunaji wa maliasili zisizorejesheka.

MALENGO YA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara imelenga kutekeleza malengo kama ifuatavyo:

- Kuotesha miche 1,000,000 ya mikarafuu pamoja na kufanya Sensa,

- Kuotesha miche 1,000,000 ya matunda, viungo, misitu na mapambo katika vitalu vya Serikali,

- Kupanda miti ya misitu eneo la hekta 100,

- Kutoa elimu ya uhifadhi wa misitu na kilimo cha mazao ya biashara,

- Kufanya tathmini ya akiba ya mchanga,

- Kurejeshea maeneo yanayochimbwa matofali ya mawe na mchanga hekta 10,

- Kufanya tathmini ya misitu na miti iliyopo Zanzibar ***(Woody Biomass Survey).***

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo**:**

- Jumla ya miche 1,152,111 imeoteshwa sawa na asilimia 115. Kati ya miche hiyo, miche 886,050 ya misitu na 141,874 ya matunda imeoteshwa Unguja na miche 105,000 ya misitu na 19,187 ya matunda imeoteshwa Pemba,

- Jumla ya miche 594,850 ya mikarafuu imeoteshwa katika vitalu vya Serikali, kati ya miche hiyo 254,800 Unguja na 340,050 Pemba. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia 59 ya lengo. Aidha, jumla ya miche 158,302 imezalishwa kutoka katika vitalu vya watu binafsi,

- Jumla ya hekta 162.2 zimepandwa miti katika Msimu wa Vuli na Masika katika Mashamba ya Serikali Unguja na Pemba,

- Elimu ya Uhifadhi imetolewa katika Shehia 58 za Unguja na Pemba katika Wilaya ya Kaskazini 'A','B', Kati na Kusini kwa Unguja na Wilaya za Micheweni, Wete, Chakechake na Mkoani kwa Pemba,
- Jumla ya hekta 18 zimepandwa miti katika maeneo yaliyochimbwa mchanga katika maeneo ya Donge, Panga Tupu na Zingwe Zingwe kwa Unguja na Kangagani, Vitongoji, Micheweni na Kishindeni kwa Pemba,

- Uzinduzi wa Mradi wa Sensa ya miti umefanyika sambamba na utayarishaji wa ramani za visiwa vya Unguja na Pemba. Aidha, kazi ya ukusanyaji wa taarifa zinazohusiana na sensa hiyo imekamilika na uchambuzi wa taarifa unaendelea,

- Katika kusimamia taratibu za uvunaji wa maliasili jumla ya matukio 78 Unguja na 43 Pemba yameripotiwa kati ya hayo watu watano kesi zao zipo mahakamani Unguja na jumla ya misumeno 51 imekamatwa na kuchomwa moto Unguja 28 na Pemba 23.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuotesha miche 1,500,000 katika Vitalu vya Serikali, kati ya miche hiyo 1,000,000 ya Misitu na 500,000 ya matunda,

- Kuotesha miche 1,000,000 ya mikarafuu,

- Kupanda miti ya misitu hekta 300 katika Misitu ya Serikali, hekta 30 za eneo la Mikoko na kilomita 50 maeneo ya barabarani,

- Kutayarisha na kutekeleza mipango shirikishi ambayo itawezesha matumizi endelevu ya Maliasili Zizisorejesheka katika Wilaya za Kaskazini 'A', Kaskazini 'B' na Kati kwa Unguja na Wilaya za Mkoani na Wete kwa Pemba,

- Kutayarisha na kutekeleza mpango wa kujikinga na matukio ya moto kwenye misitu ya jamii na Serikali,

- Kuimarisha na kuendeleza ufugaji nyuki wa kisasa kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa asali, kuongeza kipato kwa jamii na utunzaji wa misitu katika maeneo yanayozunguka misitu ya hifadhi,

- Kupitia kanuni ya msumeno wa moto kwa lengo la kutotumika tena,

- Kukamilisha Sensa ya Miti ***(Woody Biomass Survey).***

Mhe, Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara itasimamia miradi mikuu minne ambayo ni:

- Mradi wa Mpango wa Taifa wa Uimarishaji Mikarafuu, **(Kiambatisho Nam. 6)**
- Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili (HIMA), (**(Kiambatisho Nam. 7**)
- Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Ukanda wa Pwani, *(Kiambatisho Nam. 8)*
- Mradi wa Kuangamiza Adui Kunguru *(Kiambatisho Nam. 9).*

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara iliombewa Tsh. 1,236,890,000 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013 Idara imepatiwa jumla ya Tsh 1,224,181,025 sawa na asilimia 99 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya Tsh. 1,299,318,000 kutoka Serikalini.

IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE

Mhe. Spika**,** Idara hii ina jukumu la kuratibu kazi za uhakika wa chakula na lishe ikiwa ni pamoja na kufuatilia, kutathmini na kutoa taarifa juu ya hali ya uhakika wa chakula na lishe na tahadhari ya mapema juu ya matukio yanayohusiana na hali ya uhakika wa chakula na lishe hapa nchini. Idara pia ina jukumu la kusimamia na kuendesha Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar ***(Zanzibar Food Reserve).***

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara imelenga kutekeleza malengo kama ifuatavyo:

- Kuendelea kuratibu ushiriki wa Sekta na Taasisi mbali mbali katika kutekeleza Sheria ya Uhakika wa Chakula na Lishe, Sheria namba 5 ya mwaka 2011;
- Kutoa mafunzo kwa wadau juu ya ukusanyaji, uchambuzi na uandishi wa ripoti juu ya masuala ya uhakika wa chakula na lishe;
- Kuendeleza mfumo wa ufuatiliaji na tathmini na utoaji wa tahadhari ya mapema juu ya hali ya Uhakika wa Chakula na Lishe nchini;
- Kukarabati maghala ya akiba;
- Kutoa elimu ya lishe na afya bora kwa jamii kwa njia ya redio na televisheni pamoja na taarifa nyengine za hali ya uhakika wa chakula nchini.

UTEKELEZAJI WA MALENGO YA 2012/2013

Mhe. Spika**,** kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo**:**

- Mikutano miwili ya Kamati Tendaji na Baraza la Taifa la Uhakika wa Chakula na Lishe imefanyika kwa lengo la kujadili hali halisi ya uhakika wa chakula na lishe nchini;
- Wafanyakazi wanne wa Idara wamepatiwa mafunzo ya uchambuzi wa sera na utoaji wa matoleo ya kisera *(Policy Analysis and Briefs);*
- Mifumo ya ukusanyaji wa taarifa kwa ajili ya kuimarisha ufuatiliaji na tathmini za uhakika wa chakula na lishe imetayarishwa. Kazi hii bado inaendelea;

- Rasimu ya kanuni za kusimamia na kuendesha hifadhi ya Chakula imetayarishwa na kazi hii inaendelea;
- Mafunzo ya lishe yametolewa kwa wanajamii 48 katika shehia za Tazari, Kijini, Kilimani na Kidoti kwa upande wa Unguja na Shehia za Tumbe Magharibi, Tumbe Mashariki, Pujini na Mbuzini kwa upande wa Pemba.

MALENGO KWA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka 2013/2014, Idara imelenga kutekeleza yafuatayo:

- Kukarabati ghala moja la Hifadhi ya Chakula liliopo Unguja;
- Kutayarisha miongozo ya uendeshaji wa Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar;
- Kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji na utoaji wa tahadhari ya mapema juu ya hali ya uhakika wa chakula na lishe kwa kujenga uwezo katika ukusanyaji wa takwimu. Kazi zilizopangwa ni:

✓ Utayarishaji wa taratibu za ukusanyaji wa taarifa na takwimu;

✓ Mafunzo kwa wafanyakazi wanane juu ya ukusanyaji wa takwimu, uchambuzi na uandishi wa ripoti za uhakika wa chakula na lishe;

- Kutoa taarifa za Hali ya Uhakika wa Chakula. Kazi zilizopangwa ni:

✓ Kukusanya takwimu na taarifa juu ya hali ya uhakika wa chakula na lishe;

✓ Uchambuzi na takwimu na taarifa za uhakika wa chakula na lishe;

✓ uandishi na uchapishaji wa ripoti za hali ya uhakika wa chakula na lishe ***(****Food Balance Sheet Reports, Policy Briefs; Food insecurity Reports);*

- Kuratibu ushiriki wa Sekta na wadau husika katika kutekeleza masuala ya uhakika wa chakula na lishe.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara iliombewa Tsh. 232,717,811 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 202,613,350 kwa kazi za kawaida sawa na asilimia 87 ya makadirio. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya Tsh. 142,188,000 kutoka Serikalini kwa kutekeleza kazi za kawaida.Kwa kazi za maendeleo Idara inaombewa jumla Tsh. 160,000,000.

IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI

Mhe. Spika, Idara hii ina majukumu ya kuendeleza na kuimarisha kilimo cha umwagiliaji maji nchini pamoja na kutoa taaluma za kiufundi juu ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu, pamoja na kushajiisha na kusimamia jumuiya za wakulima kwenye mabonde ya umwagiliaji. Idara pia inatoa huduma za elimu na pembejeo za kilimo kwa wakulima wa umwagiliaji maji.

MALENGO KWA MWAKA 2012/2013

Mhe. Spika, mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara imelenga kutekeleza malengo yafuatayo**:**

- Kukamilisha ujenzi wa miundombinu kwa ekari 300 za maeneo yanayofaa kwa kilimo cha Umwagiliaji maji;
- Kutekeleza Mpango maalum wa kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji kama ifuatavyo:

✓ Kujenga mitaro ya saruji mita 800 pamoja na vigingi vyake;
✓ Kujenga msingi wa udongo mita 1000;
✓ Ukarabati wa njia za shambani mita 1,000, mabanio, pampu na visima, pamoja na ofisi na ghala za mashambani;
✓ Kuchimba visima sita na kununua pampu sita pamoja na uwekaji wa umeme katika vituo vya Kiboje Mkwajuni, Kibokwa, Kibonde Mzungu, Cheju, Bumbwisudi na Ole;
✓ Uwekaji wa umeme katika visima vya bonde la Mtwango kwa Unguja na Machigini na Makombeni kwa Pemba na;
✓ Utayarishaji wa ardhi hekta 80 kwa ajili ya kilimo cha Umwagiliji maji.

- Kutoa mafunzo kwa wakulima na wafanyakazi wa Sekta ya umwagiliaji maji.

UTEKELEZAJI WA MALENGO 2012/2013

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013 Idara imetekeleza malengo yake kama ifuatavyo**:**

- Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji maji katika bonde la Makombeni umefanyika kama ifuatavyo:

✓ ujenzi wa matuta ya kugawia plot kwa eneo la hekta saba;

- ✓ ujenzi wa matuta mita 220 kwa ajili ya misingi ya ndani; ujenzi wa vigingi 20;
- ✓ ujenzi wa milango 16 ya kuingizia maji;
- ✓ ujenzi wa barabara ya kifusi mita 900;
- ✓ ujenzi wa sanduku la kugawia maji ***(Division box)***
- ✓ uwekaji wa transfoma na pampu;

- Kisima kimoja cha kumwagilia maji kimechimbwa na mitaro ya kutolea maji mita 2000 imechimbwa katika bonde la Banda maji;
- Mtaro wa saruji wa kumwagilia maji mita 600 umejengwa na pampu ya kumwagilia maji imenunuliwa na imefungwa katika bonde la Cheju –Jendele;
- Matuta kwa ajili ya ujenzi wa msingi wa umwagiliaji maji yenye urefu wa mita 4000 yamejengwa katika bonde la Koani (mita 2000) na Kirindunda-Bumbwisudi (mita 2000).
- Upimaji na usanifu wa mitaro ya kutolea maji mita 500 bonde la Koani na mita 2100 bonde la Kirindunda–Bumbwisudi umefanyika;
- Visima viwili vimechimbwa katika mabonde ya Koani na Kirindunda–Bumbwisudi;
- Ununuzi na ufungaji wa surface motor yenye kilowati 15 umefanyika sambamba na ukarabati wa transfoma katika bonde la Bumbwisudi;
- Uwekaji wa nguzo za umeme kwenye visima vya umwagiliaji maji katika bonde la Mtwango umefanyika;
- Ujenzi wa matuta ya kuzuia uingiaji wa maji ya bahari katika maeneo ya kilimo umefanyika katika mabonde ya Chamawe mita 250 na Koowe mita 190. Kazi hii inaendelea;
- Mafunzo kwa wakulima 25 (wanawake 18 na wanaume 7) namna ya kupanda mbegu ya mpunga aina ya NERICA kwenye mashamba ya umwagiliaji maji kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu yamefanyika katika kituo cha Bumbwisudi.

MALENGO YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imelenga kutekeleza mambo yafuatayo:

- Kuchimba visima vinane katika vituo vya Kibondemzungu, Ole, Kisimamchanga, Kibojemkwajuni, Cheju, Kibokwa na Bumbwisudi

- Kujenga mtaro wa saruji mita 500 na kununua pampu mbili kwa ajili ya mabonde ya Bumbwisudi na Kibokwa kupitia mradi wa KOICA;
- Ujenzi wa vibanda vinne vya kuendeshea pampu katika kituo cha Kibokwa (1), Bumbwisudi (1) na Mtwango (2);
- Kuunga umeme katika bonde la Machigini Pemba;
- Kupima, kuchora ramani na kusanifu miundombinu ya umwagiliaji maji katika eneo la hekta 2,105 kwenye vituo vya Cheju, Kilombero, Chaani, Mlemele na Makwararani kupitia Mradi wa *EXIM BANK* – Korea;
- Kutayarisha zabuni na kutafuta mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu katika eneo la hekta 2,105;
- Ujenzi wa njia ya kutolea maji ya ziada ***(spillway)*** katika tuta lilioko bonde la Chamawe Pemba;
- Kukarabati visima viwili na pampu nne za vituo vya Bumbwisudi, Cheju, Saninga na Kibokwa;
- Utayarishaji wa ardhi Makombeni hekta 7 kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji maji;

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara iliombewa Tsh. 577,837,500 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 571,469,800 sawa na asilimia 99 ya makadirio. Kwa upande wa fedha za maendeleo mchango wa SMZ Idara ilitengewa Tsh. 500,000,000 hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013 Idara imepatiwa jumla ya Tsh. 167,211,520. Kwa kazi za maendeleo, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara inaombewa jumla ya Tsh. 450,000,000 kutoka SMZ na fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo (*KOREA EXIM BANK)* ni Tsh. 3,328,000,000.

OFISI KUU PEMBA:

Mhe. Spika, utekelezaji kwa upande wa Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2012/2013 unaendana na mtiririko wa maelezo ya kila Idara ambayo yamehusisha na shughuli za Ofisi Kuu Pemba. Ofisi hii ya Pemba ni kiunganishi katika kuhakikisha kwamba majukumu, malengo na shabaha zote za Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa upande wa Pemba zinatekelezwa kama zilivyokusudiwa.

Mhe. Spika, ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Kuu Pemba, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lako Tukufu liliidhinisha matumizi

ya jumla ya Tsh. 1,716,847,779 kwa kazi za kawaida na mpaka kufika tarehe 30, Juni 2013, Ofisi Kuu Pemba imepatiwa Tsh. 1,644,215,898 sawa na asilimia 96. Kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi Kuu Pemba inaombewa jumla ya Tsh. 1,793,012,000 kwa kazi za kawaida.

CHANGAMOTO ZA WIZARA

Mhe. Spika, pamoja na mafanikio yaliyofikiwa, bado Wizara ya Kilimo na Maliasili inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

- Ongezeko kubwa la mahitaji ya mazao ya maliasili kuliko uwezo wa uzalishaji;
- Matumizi mabaya ya zana zinazopelekea uharibifu wa mazingira ikiwemo msumeno wa moto;
- Uhaba na uchakavu wa matrekta kulichangia kutokuwalimia baadhi ya wakulima kwa wakati;
- Uvamizi wa maeneo ya kilimo kwa ajili ya makaazi, uchimbaji wa mchanga na ukataji wa matofali kinyume na utaratibu kunasababisha kupungua kwa eneo la kilimo;
- Wizi wa mazao ya kilimo na maliasili;
- Uchache wa Mabwana/ Mabibi Shamba;
- Mabadiliko ya hali ya hewa na mvua zisizotabirika;
- Ushiriki na uwekezaji mdogo wa sekta binafsi katika maendeleo ya kilimo;

MFUMO WA BAJETI UNAOZINGATIA PROGRAMU

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili inaendelea na utekelezaji wa mfumo wa Bajeti ambayo inazingatia utekelezaji wa Programu na Miradi husika (***Program Based Budget)***. Aidha, naliomba Baraza lako Tukufu lipokee muhutasari wa bajeti itakayotekelezwa na Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa kuzingatia mfumo wa programu. Ni imani yangu kwamba Wajumbe wa Baraza lako Tukufu watapata nafasi ya kuupitia na kuuelewa utaratibu wa mfumo huu wa bajeti unaozingatia programu na miradi husika.

SHUKRANI

Mhe. Spika, Kwa mara nyengine tena naomba nitumie nafasi hii kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa muongozo na ushauri wao uliopelekea kukamilika kwa hotuba hii. Aidha, tunazishukuru nchi na Mashirika ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo, zikiwemo nchi za Japan, Finland, Norway, Ireland, China, India, Israel, Korea ya Kusini, Marekani, Misri, Ujerumani, Vietnam na Uholanzi. Aidha, tunaomba kutoa shukurani za pekee kwa Mashirika na Taasisi za Kikanda na za Kimataifa zifuatazo: *Africa Rice, COSTECH, SUMA JKT, TASAF, ZSTC, SIDO,* Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika ya Tanzania, *SUA, IAEA, INGER-Africa,* Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika- *AfDB, IFAD, UNDP, FAO, JICA, UNICEF, WFP, UPOV, USAID, KOICA, IITA, iAGRI, IRRI, CFC, GEF, Exim Bank of Korea, AVRDC* na *AGRA*. Ushirikiano na misaada ya Nchi na Mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

Mhe. Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara pamoja na mazingira magumu waliyonayo. Hasa wale wakulima wanaochukua juhudi za kubadilisha kilimo cha kujikimu na kwenda katika kilimo cha Kibiashara.

Mhe. Spika**,** pia naomba kuwashukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo na Maliasili, Naibu Katibu Mkuu (Kilimo) na Naibu Katibu Mkuu (Maliasili), Afisa Mdhamini, Wakurugenzi wa Idara na Taasisi, watumishi wote wa Wizara pasi na kuwasahau na wadau wa Sekta ya Kilimo na Maliasili kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2012/2013 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2013/2014 ili kufikia malengo yaliyowekwa.

MAKADIRIO YA MAOMBI YA FEDHA ZA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2013/2014

Mhe. Spika, kwa kuzingatia maelezo niliyoyatoa, naomba sasa Baraza lako Tukufu liidhinishe Tsh. 30,320,998,000 kati ya hizo Tsh. 12,069,000,000 kwa ajili ya kazi za kawaida na Tsh. 500,000,000 ruzuku Chuo cha Kilimo Kizimbani na Tsh. 17,751,998,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi 14 ya maendeleo ambapo Tsh. 1,560,000,000 ikiwa ni mchango wa Serikali na kwa upande wa wahisani wa maendeleo ni Tsh. 16,191,998,000.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Kiambatisho. 1. Takwimu za Uzalishaji wa Mazao ya kilimo kwa Tani Mwaka 2012/2013

Mazao/ Mwaka	**2007**	**2008**	**2009**	**2010**	**2011**	**2012**
Mahindi	1,931	1,920	2,011.75	3,112	3,281	856.67
Mtama	794	610	457	572	512	484.31
Mpunga	20,038	20,857	26,980	21,014	23,702	6,372.15
Muhogo	187,213	153,050	195,674	229,284	273,342	192,072.68
Ndizi	93,641	100,873	100,873	102,258	110,250	97,934.53
Viazi Vitamu	45,620	55,294	53,596	58,953	92,715	31,767.75
Viazi Vikuu	8,192	3,516	11,373	7,488	4,212	3,563.80
Njugu Nyasa	76	465	320.43	432	401	407.26

Chanzo: Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Kiambatisho. 2. Programu ya Kuendeleza Huduma za Kilimo - *(ASSP)*

MWAKA ULIOANZA: Programu ilianza mwezi Juni ya mwaka wa fedha 2006/2007

Gharama Mwaka 2012/2013: Kwa mwaka 2012/2013 Programu iliombewa Tsh. 100,000,000 kutoka SMZ, na Tsh. 584,318,000 kutoka IFAD. Hadi kufikia Juni, 2013 fedha zilizopatikana kutoka Serikalini ni Sh. 30,000,000 na Tsh. 411,087,168 kutoka IFAD	
Malengo 2012/2013	**Utekelezaji**
Kuendeleza kuvipatia taaluma za kilimo bora vikundi 108 vya skuli za wakulima kwa mzunguko wa pili wa vipindi vya masomo vinane.	Vikundi 108 vya skuli za wakulima viliwezeshwa kufanya mafunzo kwa mizunguko miwili ya masomo wa vipindi vya masomo saba.
Kujenga bweni katika chuo cha Kilimo	Ujenzi wa Bweni katika chuo cha

Kizimbani	Kilimo Kizimbani umekamilika.
Kuendelea kusaidia vituo vya kupashana habari	Programu imeendelea kusaidia vituo vya kupashana habari kwa kuwapatia vitendea kazi na huduma za intaneti.
Kupeleka wakulima katika ziara za kimafunzo ndani ya Zanzibar na Tanzania bara	Jumla ya wakulima 18 walipelekwa Morogoro kwa ziara ya kubadilishana uzowefu na taaluma na wakulima wenzao na pia walipata fursa ya kuhudhuria maonesho ya nane nane.
Kuimarisha shughuli za utafiti katika vituo vya utafiti na mashamba ya wakulima	Programme imesaidia kukarabati masanduku manne ya uzalishaji mbegu ***(Germination Boxes)*** katika kituo cha Utafiti Kizimbani

	na kuwapa mafunzo ya ‘utunzaji wa vitalu wafanyakazi wa sehemu ya nursery.
Kuendesha warsha ya wadau kuhusu mapitio ya utekelezaji wa kazi za programu kwa kipindi cha mwaka mmoja	Warsha za wadau kuhusu mapitio ya utekelezaji wa kazi za Programu katika ngazi zote kuanzia Shehia, Wilaya hadi Taifa kwa kipindi cha mwaka mmoja zilifanyika mwezi wa Febuari (Pemba na Unguja).
Kuendesha vikao vya kamati ya uongozi na vikao vya wawezeshaji wa wilaya.	Vikao viwili vya kamati ya uongozi na vikao vya wawezeshaji vilifanyika katika wilaya zote tisa za utekelezaji wa Programu kwa madhmuni ya kutathmini maendeleo ya skuli za wakulima.

Gharama Mwaka 2013/2014: Programu inatarajia kupata Shilingi 55,000,000 kutoka SMZ na Tsh. 518,881,000 kutoka IFAD	
Malengo kwa Mwaka 2013/2014 • Kuendelea kuimarisha kazi za utafiti, tathimini na ufuatiliaji katika maeneo ya wakulima; • Kuwapatia mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu na taarifa Mabwana/Mabibi shamba; • Kutoa mafunzo ya uzalishaji mbegu bora kwa vikundi vya uzalishaji mbegu; • Kuendesha warsha za mwisho za mapitio ya utekelezaji wa programu; na • Kutayarisha ripoti ya kumalizika kwa programu.	

Kiambatisho. 3. Programu ya Kuendeleza Sekta za Mifugo (*ASDP*-L)

MWAKA ULIOANZA: Programu ilianza mwezi Juni ya mwaka wa fedha 2006/2007

Gharama Mwaka 2012/2013: Kwa mwaka 2012/2013 Programu iliom Tsh. 828, 602,000 kutoka IFAD. Hadi kutoka Serikalini ni Tsh. 20,000,000 na
Malengo 2012/2013
Kuwapatia mafunzo msasa watoa hud za msingi za mifugo 50.
Kuongeza watoa huduma za msingi mifugo wapya 45 na kuwapatia mafunzo siku 40 pamoja na kuwanunulia vifaa ajili ya kuanzia kazi za utoaji wa hud hizo.
Kuwapatia mafunzo msasa waweze 100 wakulima na wafugaji.
Kuanzishwa vikundi (skuli) vipya 300 Wakulima na wafugaji na kuvip mafunzo bora.
Kuendelea kuvipa taaluma za kilimo vikundi (skuli) 72 vya skuli za wakulima

Kuendelea kuvipa taaluma za kilimo ufugaji bora vikundi 700 vya skuli wakulima.
Kununua chanjo za kukinga maradhi mahepe dozi 900,000 na kuzikabidhi ka Idara ya Huduma ya Utabibu ya Wizara Mifugo na Uvuvi.
Kununua chanjo za kukinga maradhi vibuma dozi 2000 na kuzikabidhi ka Idara ya huduma ya utabibu ya Wizara Mifugo na Uvuvi
Kuwapatia wafugaji ziara za mafunzo n ya Zanzibar na Tanzania Bara
Kununua mashine 3 za kutotolea vifara na mashine 5 za kusarifu maziwa kwa ya wafugaji.
Gharama Mwaka 2013/2014: Progra kutoka SMZ na Tsh. 828,155,000 kutoka
Malengo kwa Mwaka 2013/2014 • Kununua mashine 3 za kutotol maziwa kwa ajili ya wafugaji; • Kuendelea kutoa taaluma za k kwa awamu ya nne; • Kuendelea kutoa taaluma za k

awamu ya tatu. • Kuwapatia mafunzo msasa ya s mifugo; • Kutoa mafunzo kwa wawezesh kilimo mseto na uhifadhi wa ma • Kufanya utafiti, ufuatiliaji na programu; • Kutayarisha vipindi kwa njia ya ya skuli za wakulima; na • Kuandaa mapendekezo ya kuen ya pili.

Kiambatisho. 4. Programu ya Miundombinu ya Masoko - MIVARF

MWAKA ULIOANZA: 2011/2012

Gharama Mwaka 2012/2013: Kwa mwaka 2012/2013 Programu iliom Tsh. 5,747,650,000 kutoka *IFAD*. Hadi kutoka Serikalini ni Tsh. 15,000,000 na
MALENGO 2012/2013
Kukarabati barabara za mashamban kilomita 50;
Ununuzi na ufungaji wa mitambo miwil ya kuzalisha barafu
Kuwajengea uwezo na kuwaunganish na masoko wazalishaji wadogo wadogo;
Kuwapatia mafunzo wazalishaji juu ya

uhifadhi na usarifu wa mazao na;
Kuandaa ziara za kimasomo (kwa vikundi) kwenye masoko na kwa wasindikaji mazao;
Kutoa mafunzo ya upangaji, utekelezaj na utunzaji wa miradi ya miundombinu;
Kuwapatia mafunzo ya kujenga uwezo wafanyakazi wa Idara ya Ushirika *SACCOS* pamoja na wajumbe wa Bod za *SACCOS*;
Gharama Mwaka 2013/2014: Progra kutoka SMZ na Tsh. 9,348,560,000 kuto
MALENGO KWA MWAKA 2013/20 • Kukarabati kilomita 100 za baraba kiwango cha kifusi; • Kujenga masoko matatu yenye vyu • Ununuzi na ufungaji wa mitambo m • Kutoa mafunzo kwa vitendo kwa w mmoja mmoja 2,150); • Kuchangia kwa asilimia 75 ununuzi • Kuwawezesha watoa huduma na wadogo wadogo 2,500; • Kuwawezesha watoa huduma kuz kifedha vijijini kwa mujibu wa mat • Kuimarisha kitengo cha Microfinan Mipango ya Maendeleo na kuisaidi • Kuratibu kazi za wadau wanaotekel

KIAMBATISHO Nam 5. MRADI WA USARIFU WA MAZAO YA KILIMO (AGRO- PROCESSING)

Maelezo ya Mradi: Mradi huu ulitaraj Julai 2010/Juni 2013**.** **Gharama/Wachangiaji.** KOICA: US SMZ TSh 600 milioni. Hata hivyo ku wetu, wahisani wameshindwa kumaliz Usarifu wa Mazao huko Kizimbani ikiw Mradi huo. Hivyo, hivi sasa Wizara ina kutumia fedha za msaada ***(budget supp*** Bajeti ya Serikali. Vilevile, Wizara ina kukamilisha ujenzi huo.
Lengo kuu: Kujenga uwezo wa wa ujasiriamali pamoja na kutoa hudum zinazozalishwa kwa lengo la kuongeza a
Gharama kwa mwaka 2012/2013: US 150,000,000
2012/2013: • Kazi ya uungaji wa umeme inaende • Kutia milango, madirisha ya alumin • Kuweka sakafu katika vyumba viwi • Kufanya tafhmini ya Jengo ili k iliobakia • Kazi nyengine zilizopangwa haziku wa fedha.
Gharama kwa mwaka 2013/2014: SMZ

Malengo ya mwaka 2013/2014:

- Kuitisha vikao vya bodi ya zabuni (
  kutekelezwa.
- Kuweka dari katika jengo lote la Ki
- Kujenga mnara wa maji kwa ajili
  Mazao.
- Kujenga makaro na kuweka miundo

Kiambatisho. 6. Programu ya Uhakika wa Chakula na Lishe

Programu: hii ni ya miaka mitano na imeanza 2009 **Gharama:** USD 15 Million. **Wachangiaji:** SMZ, *FAO* na Serikali ya Ujerumani
Lengo kuu la Programu ni kuchangia katika hatua za kitaifa za kupunguza umasikini wa chakula na kipato, kukabiliana na hali ya kutokuwa na uhakika wa chakula na lishe katika ngazi za Taifa, jamii na kaya na kushajiisha ushiriki wa jamii katika hatua za kujiongezea kipato.
Gharama Mwaka 2012/2013: Programu iliombewa Sh. 300, 000,000 kutoka SMZ, 236,592,000

kutoka Serikali ya Ujerumani. Hadi kufikia Juni, 2013 fedha zilizopatikana kutoka Serikalini ni Sh. 30,000,000 na Tshs. 55,294,720 kutoka Serikali ya Ujerumani
Utekelezaji 2012/2013 • Kamati nne za Uhakika wa chakula na lishe zimeazishwa Wilaya ya Kati: Shehia za Marumbi na Umbuji; Wilaya ya Kaskazini A: Shehia ya Muembe shauri na Tumbatu Gomani. Jumla ya wanajamii 48 walishiriki katika kazi hizi. • Mafunzo juu ya utekelezaji wa mipangokazi, tathmini na ufuatilijaji, uhamasishaji wa rasilimali za kutekeleza mipangokazi ya uhakika wa chakula na lishe yametolewa kwa wajumbe wa kamati hizi; • Ripoti ya Food Balance Sheet imetayarishwa na kusambazwa kwa wadau; • Mafunzo juu ya elimu ya lishe yametolewa Shehia za Mbuzini na Pujini, Tumbe Mashariki na

Tumbe Magharibi kwa Pemba na Shehia za Kijini, Kilimani, Kidoti na Tazari kwa Unguja. Jumla ya wanajamii 120 wamepatiwa mafunzo hayo.
Gharama Mwaka 2013/2014: Programu inatarajia kupata Tsh. 160,000,000 kutoka SMZ
Malengo Mwaka 2013/2014 • Kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Hifadhi ya Chakula ya Zanzibar kwa: ✓ Kukamilisha Kanuni za Sheria ya Uhakika wa chakula na Lishe; ✓ Kutayarisha miongozo juu ya usambazaji wa chakula cha dharura ***(emergency food distribution systems and guidelines);*** • Kufanya ukarabati wa ghala moja la uhifadhi wa chakula liliopo Unguja;

- Kutoa mafunzo ya lishe katika ngazi ya Shehia kwa Kina mama wajawazito na wenye watoto chini ya umri wa miaka mitano (5).

Kiambatisho. 7 Mradi wa Uimarishaji Mikarafuu

Lengo kuu: Kuongeza pato la mkulima na taifa kwa ujumla.

Malengo mahususi:

- kuimarisha zao la karafuu kwa kuotesha miche bora
- kupanda upya mashamba ya mikarafuu
- kutoa elimu na kufanya utafiti.

Gharama Mwaka 2012/2013:
Kwa mwaka 2012/2013 Programu ilio Fedha zilizopatikana ni 70,000,000
Malengo 2012/2013
Kuotesha miche 1,000,000 ya mikarafuu

Kutengeneza mabanda manne (4) ya kudumu ya kuoteshea miche
Kutoa elimu ya kilimo cha mikarafuu
Kufanya tathmini ya miche iliyoota baada ya kutolewa kwa wakulima.
Kufanya sensa ya mikarafuu
Gharama Mwaka 2013/2014: inataraj SMZ
Malengo ya mwaka 2013/2014 • Kuzalisha miche 1,000,000 ya bila ya malipo; • Kuendelea na ujenzi na mateng katika vitalu vya Selem, Machu Mkatamaini na Chanjaani kwa • Kuendeleza tathmini ya mich katika msimu uliopita; • Kutoa Elimu ya utunzaji wa Wilaya 7 za Unguja na Pemba n • Kuhamasisha upandaji wa m Pemba (Upandaji wa Mikarafu TV, na mikutano 8 ya wadau); • Kupima na kuchora ramani za kuyasafisha.

Kiambatisho. 8 - Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Asili (HIMA)

Lengo kuu: Kupunguza Hewa ukaa kutokana na ukataji wa miti ovyo na uharibifu wa misitu.

Gharama Mwaka 2012/2013: Progra SMZ, na Tsh 857,304,000 kutoka Serik fedha zilizopatikana kutoka Serikalini kutoka Serikali ya Norway.
Malengo 2012/2013
Kuwajengea uwezo kamati 29 za Mipango ya Usimamizi wa Rasilimali za Misitu ya Jamii
Kuelimisha jamii kuhusu MKUHUMI
Kupanda miche ya misitu hekta 200
Kufanya tathmini ya hewa ukaa na tathmini ya matumizi ya gesi ya kupikia (*LPG*)
Kuelimisha wakulima wa vitalu binafsi 22 Unguja na Pemba
Gharama Mwaka 2013/2014: inataraj na Tsh. 250,000,000 kutoka Serikali ya

MALENGO 2013/2014
• Kutayarisha mpango wa kuong • Kutoa gesi ya kupikia bila ya Pemba 2000) pamoja na kuelim • Kufanya Tathmini ya Hewa utaratibu wa malipo ya hewa uk • Kutoa elimu ya MKUHUMI k Mazingira; • Kutengeneza Tovuti itakayohus

Kiambatisho. 9. Mradi wa Hifadhi ya Misitu ya Ukanda wa Pwani

Gharama Mwaka 2012/2013: Progra SMZ, na Tsh 688,470,000 kutoka *UND* zilizopatikana kutoka Serikalini ni Tsh. *UNDP/GEF*.
Malengo
Kuweka mipaka ya kudumu katik maeneo ya misitu ya Hifadhi y Kiwengwa, Masingini, Ras Kiuyu n Msitu mkuu
Kuendeleza utaratibu wa kupandish hadhi ya msitu wa hifadhi ya Masingin kuwa hifadhi ya kimaumbile
Kutangaza Msitu wa Muyuni – Jambian kuwa msitu wa Hifadhi ya Akiba

Kukamilisha mpango endelevu wa usimamizi katika Msitu wa Hifadhi ya Masingini na kupitia mipango ya usimamizi ya Hifadhi za Ngezi Kiwengwa - Pongwe na Jozani na Ghuba ya Chwaka
Gharama Mwaka 2013/2014: inataraji na Tsh. 350,000,000 kutoka *UNDP/GEF*
Malengo ya mwaka 2013/2014 • Kuweka mipaka ya kudumu ka Kiwengwa, Ras Kiuyu na Msitu • Kuendeleza utaratibu wa kupa Masingini kuwa hifadhi ya kima • kutangaza Msitu wa Muyuni - Akiba; • Kukamilisha mpango wa usimam na kupitia mipango ya usimam Pongwe , Jozani na Ghuba ya Ch

KIAMBATISHO 10: MRADI WA KUANGAMIZA KUNGURU:

Lengo kuu: Kuangamiza kunguru wote;

Lengo mahsusi: Kuangamiza kuguru 400,000 kwa kutumia sumu na mitego

Gharama Mwaka 2012/2013: Kwa mwaka 2012/2013 Programu iliomb Finland. Hadi kufikia Juni, 2013 fedha z
MALENGO 2012/2013
Ununuzi wa sumu aina ya DRC 1339 kil 10.

Utengenezaji wa mitego 157 Unguja n Pemba.
Kuangamiza kunguru 300,000 kw kutumia sumu na mitego.
Gharama Mwaka 2013/2014: Kwa mwaka 2013/2014 Programu inaom
MALENGO 2013/2014
• Kununua sumu ya kuulia kungu • Ununuzi wa chambo cha kutege • Kuelimisha jamii kwa njia ya v vijarida; Kuhamasisha wanajamii katika Shehia z kazi ya uangamizaji kunguru.

11. FEDHA ZILIZOTOLEWA KWA MIRA ELEO KUANZIA JULAI,2012 HADI JUNI, 20

LA MRADI	**MAKISIO 2012/2013 WAHISA NI**	**FEDHA ZILIZOTOL EWA JULAI /JUNI, 2013 WAHISANI**	**ASIL MIA (%)**
GRAMU YA NDELEZA TA YA MO NA UGO(ASDP-	828,602,00 0	914,767,920	110
GRAMU YA	584,318,00	411,087,168	70

MARISHA UMA YA MO(*ASSP*)	0		
DI WA KIKA WA KULA NA E	236,592,000	55,294,720	23
DI WA UZA RIFU WA AO YA MO	-	-	
DI WA MARISHA ARAFUU	-	-	
DHI YA TU YA I	857,304,000	376,864,000	44
ADHI WA TU YA NI	688,470,000	374,288,000	54
NGO MKUU NDELEO KILIMO CHA AJI	-	-	
GRAMU YA FITI WA MO NA IASILI	-	-	
GRAMU YA NDOMBINU SOKO, NGEZA MANI NA AADA INI	5,747,650,000	501,510,620	9
NGAMIZA I GURU	474,180,000	153,808,156	32
LA		**2,787,620,58**	**30**

	9,417,116,000	**4**	
PYA			
NZI WA NI MBANI			
SP			
ANZO BORA			
LA YA ADI MIPYA			
LA KUU	**9,417,116,000**	**2,787,620,584**	**30**

12. MAKISIO YA FEDHA ZILIZOO
IKANA JULAI 2012 HADI JUNI, 2013

A LA ADI	**MAKISIO 2012/2013 SMZ**	**FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI /JUNI, 2013**	**%**
OGRAMU ENDELEZA KTA YA TUGO *DP*-L)	60,000,000	20,000,000	33
OGRAMU MARISHA DUMA YA IMO (ASSP)	100,000,000	30,000,000	30
ADI WA AKIKA WA AKULA NA HE	300,000,000	30,000,000	10

ADI WA KUZA ARIFU WA ZAO YA IMO	150,000,000	30,000,000	20
ADI WA MARISHA KARAFUU	200,000,000	70,000,000	35
ADHI YA ITU YA LI-HIMA	100,000,000	30,000,000	30
FADHI WA ITU YA ANI	100,000,000	30,000,000	30
ANGO UU WA ENDELEO KILIMO A U/MAJI	500,000,000	167,211,520	33
OGRAMU UTAFITI KILIMO MALIASILI	400,000,000	41,000,000	10
OGRAMU UNDOMBIN YA SOKO, ONGEZA AMANI NA AADA JINI	180,000,000	15,000,000	8
ANGAMIZA UI NGURU			
MLA	**2,090,000,000**	**463,211,520**	**22**
PYA			
A BWENI			

FSIP			
MLA OGO			
MLA KUU	**2,090,000,000**	**463,211,520**	**22**

Kiambatisho.13: TAARIFA YA MA
KIPINDI CHA JULAI, 2012 HADI

KASMA	**CHANZO CHA MAPATO**	**MAKARIO MWAK 2012/13**
0301 OFISI KUU PEMBA		
142224	MAZAO YA MISITU	120,000 0
142299	UKODISHAJI MIKARAFUU	
142225	ADA YA UUZAJI WA MAWE MCHANGA, KOKOTO	28,000,
	JUMLA NDOGO	**148,000 0**
142254	UKAGUZI WA MAZAO	3,500,0
142257	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	500,000
145001	MAPATO MENGINEYO	1,500,0
142101	MAUZO YA MICHE	1,000,0
	JUMLA NDOGO	**6,500,0**
	JUMLA PEMBA	**154,500 0**
0401 IDARA YA MIPANGO, SERA		
14500	MAPATO	2,000,0

1	MENGINEYO	
	JUMLA NDOGO	**2,000,0**
1501 IDARA YA KILIMO		
142224	UKAGUZI WA MAZAO	8,000,0
	JUMLA NDOGO	**8,000,0**
1701 TAASISI YA UTAFITI WA KI		
142257	MAUZAJI YA MAZAO NA MICHE	3,000,0
142281	ADA YA UINGIZAJI WATALII	2,500,0
	JUMLA NDOGO	**5,500,0**
0701 IDARA YA MISITU NA MALI		
1422101	MAUZO YA MICHE	1,000,0
142224	MAZAO YA MISITU	75,000,
142299	UKODISHAJI MIKARAFUU	
142225	ADA YA UUZAJI WA MAWE MCHANGA, KOKOTO	180,000 0
	JUMLA NDOGO	**256,000 0**
	JUMLA UNGUJA	**271,500 0**
	JUMLA KUU YA WIZARA	**426,000 0**

Kiambatisho. 14. FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI 2012 HADI JUNI, 2013 – KAZI ZA KAWAIDA

IDARA	**BAJET 2012/20**
OFISI KUU PEMBA	1,716,84
IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI	634,523
IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA	1,236,85
IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	577,837
IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI	718,767
IDARA YA UHAKIKA	232,717

WA CHAKULA	
IDARA YA KILIMO	5,618,5
TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	842,307
CHUO CHA KILIMO	308,800
JUMLA KUU	**11,887, 0**

Kiambatisho. 15. FEDHA ZILIZOTOLEWA KUANZIA JULAI 2012 HADI JUNI, 2013 KWA KAZI ZA KAWAIDA

	IDARA	MISHAHARA			MATUMIZI YA KAWAIDA (OC)		
		BAJETI 2012/2013	FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI, 2012 HADI JUNI, 2013	%	BAJETI 2012/2013	FEDHA ZILIZOTOLEWA JULAI HADI JUNI, 2013	%
1	OFISI KUU PEMBA	1,539,200,000	1,480,410,150	96	177,647,779	163,805,748	92
2	IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI	224,700,000	222,002,150	99	409,823,647	406,348,585	99
3	IDARA YA MISITU NA MALI ZISIZOREJESHEKA	1,152,700,000	1,140,532,233	99	84,190,000	83,648,792	99
4	IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	512,080,000	511,729,800	99	65,757,500	59,740,000	91
5	IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	503,760,000	501,766,900	99	215,007,623	210,753,152	98
6	IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA	179,760,000	154,063,350	86	52,957,811	48,550,000	92
7	IDARA YA KILIMO	2,077,600,000	1,946,682,696	94	3,540,902,820	3,166,830,382	89
8	TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	774,200,000	772,797,500	99	68,107,280	61,342,750	90
9	CHUO CHA				308,800,	288,800,	94

	KILIMO KIZIMBANI RUZUKU				000	000	
	JUMLA KUU	**6,964,000,000**	**6,729,984,779**	**97**	**4,923,194,460**	**4,489,819,409**	**91**

Kiambatisho. 16. TAARIFA YA FEDHA ZILIZOOMBWA JULAI, 2013 HADI JUNI, 2014 – KAZI ZA KAWAIDA

	IDARA	**MISHAHARA**	**MATUMIZI MENGINEYO**	**JUMLA**
1	03 OFISI KUU PEMBA	1,463,012,000	330,000,000	1,793,012,000
2	04 IDARA YA SERA, MIPANGO NA UTAFITI	149,548,000	300,000,000	449,548,000
3	07 IDARA YA MISITU NA MALI ZISIZOREJESHEKA	1,139,318,000	160,000,000	1,299,318,000
4	11 IDARA YA UMWAGILIAJI MAJI	528,066,000	79,000,000	607,066,000
5	13 IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI	660,634,000	470,000,000	1,130,634,000
6	14 IDARA YA UHAKIKA	102,188,000	70,000,00	172,188,00

	WA CHAKULA		0	0
7	15 IDARA YA KILIMO	1,899,736,000	3,750,000,000	5,649,736,000
8	17 TAASISI YA UTAFITI WA KILIMO	887,498,000	80,000,000	967,498,000
	JUMLA	**6,830,000,000**	**5,239,000,000**	**12,069,000,000**
	RUZUKU KWA CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI			**500,000,000**
	JUMLA KUU	**6,830,000,000**	**5,239,000,000**	**12,569,000,000**

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: (Kny. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha Biashara na Kilimo):

Mhe. Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, naomba uniruhusu kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Spika, awali ya yote napenda kumshuruku Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika siku hii ya leo ni matumaini yangu kuwa sote ni wazima wa Afya. Aidha napenda kukushukuru wewe kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni kwa niaba ya Kamati yangu kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Spika, kabla ya kutoa maoni napenda kuwashukuru sana Waheshimwa Waziri wa Kilimo na Maliasili Mhe.Suleiman Othman Nyanga pamoja na Naibu Waziri Mhe. Mtumwa Kheri Mbarak kwa mashirikiano makubwa waliotupa katika kipindi chote tunapotekeleza kazi zetu za Kamati.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe na makatibu wa Kamati kwa ushirikiano wao wa dhati waliouonesha wakati wa kuipitia na kuijadili bajeti ya Wizara hii katika

Kamati, naomba muwatambuwe Wajumbe na makatibu hao kwa kuwataja kwa majina yao kama ifuatavyo:-

1)	Mhe. Salmin Awadh Salmin	Mwenyekiti
2)	Mhe. Hija Hassan Hija	Makamo
3)	Mhe. Asha Abdu Haji	Mjumbe
4)	Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Mjumbe
5)	Mhe. Hamad Masoud Hamad	Mjumbe
6)	Mhe. Raya Suleiman Hamad	Mjumbe
7)	Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Mjumbe
8)	Ndg. Haji Khatib Haji	Katibu
9)	Ndg. Shemsa Mabaad Moh'd	Katibu

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili katika kipindi cha miaka mitatu ijayo bado inaendelea na mwelekeo wa kuleta mapinduzi ya kilimo yatakayotoa mchango zaidi katika uchumi wa taifa na kupunguza umaskini.kwa mnasaba huu sekta ya kilimo inaendelea kuwa ni muhimili mkuu wa Uchumi Zanzibar hasa kwa vile Wananchi walio wengi vijijini na mijini wanategemea sekta ya kilimo kwa kuwapatia chakula, ajira na mapato.

Mhe. Spika, Wizara ya Kilimo na Maliasili imejiwekea mikakati na malengo yake mengi mazuri ambayo tunaamini kuwa pindi ikiwezekana kuyatekeleza hali ya uchumi itaiimarika zaidi. Hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa mambo mengi yanashindwa kutekelezwa kutokana na bajeti ndogo inayotengwa na Serikali ya Wizara ya kilimo na pia kutoingizwa fedha hizo kwa wakati.Hata hivyo kwa bajeti hii inaonesha kuwa fedha zilipangwa ni kidogo sana ukilinganisha na malengo na mikakati ya Wizara iliyojiwekea.Ni vyema Serikali ikafikiria upya suala la kuongeza bajeti zaidi ya Wizira ya Kilimo ili ile azma ya kuleta Mapinduzi ya Kilimo iweze kutekelezwa kwa vitendo.

Mhe. Spika, kwa upande wa mapato, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2013,Wizara ya Kilimo imekusanya jumla ya Shillingi Mia Tano Hamsini Millioni, Laki Mbili Kumi na Sita Elfu, Mia Sita na Sitini (Tsh.550,216,660) sawa na asilimia 129 na kuvuka lengo lililowekwa la kukusanya Shillingi Mia Nne Ishirini na Sita Millioni (Tsh 426,000,000). Kamati inaipongeza Wizara kwa kazi hiyo, hata hivyo tungependa kufahamu ni sababu zipi zilizopelekea

ongezeko hilo pamoja na sababu za kukosekana kwa mapato ya mauzo ya mazao na miche.

Mhe. Spika, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Wizara ya Kilimo na Maliasili ilikadiria kupata jumla ya Shillingi Kumi na Moja Billioni, Mia Tano na Sabini na Nane Millioni, Laki Tatu na Tisini na Nne Elfu, Mia Nne na Sitini (Tsh. 11,578,394,460) kwa kazi za kawaida na Shillingi Mia Tatu na Nane Millioni na Laki Nane (Tsh 308,800,000) ikiwa ni Ruzuku kwa Chuo cha Kilimo Kizimbani. Hadi kufikia Juni, 2013 fedha zilizopatikana kwa kazi za kawaida ni Shillingi Billioni Kumi, Mia Tisa Thelathini na Moja Millioni, Elfu Nne Mia Moja na Themanini na Nane (Tsh.10,931,004,188) sawa na asilimia 94. Kwa upande wa Chuo cha Kilimo Ruzuku ya Shillingi Mia Mbili na Themanini na Nane Millioni na Laki na Nane (Tsh. 288,800,000) imepatikana ikiwa sawa na asilimia 94.

Katika kazi za maendeleo, Wizara ya Kilimo na Maliasili kwa mwaka wa fedha wa 2012/2013, iliidhinishiwa jumla ya Tsh. Shillingi Billioni Mbili na Tisini Millioni (2,090,000,000) ikiwa ni mchango wa wa SMZ. Hadi kufikia mwezi wa Juni 2013, fedha zilizopatikana ni Shillingi Mia Nne Sitini na Tatu Millioni, Laki Mbili na Kumi na Moja Elfu, Mia Tano na Ishirini (Tsh.463,211,520) sawa na asilimia 22. Kwa upande wa Washirika wa Maendeleo, fedha zilizoidhinishwa na Baraza lako Tukufu kwa mwaka 2012/2013 ni Shillingi Billioni Tisa, Mia Nne na Kumi na Saba Millioni, Laki Moja na Kumi na Sita Elfu (Tsh. 9,417,116,000). Hadi kufikia mwezi wa Juni, 2013, Wizara imepata jumla ya Shillingi Billioni Mbili, Mia Saba Themanini na Saba Millioni, Laki Sita Ishirini Elfu, Mia Tano na Themanini na Nne (Tsh 2,787,620,584) sawa na asilimia 30 ya lengo.

Mhe. Spika, uchanganuzi na tafsiri ya fedha zilizopatikana inatuonesha jinsi gani hali ilivyokuwa ngumu katika upatikanaji fedha jambo ambalo limepelekea Wizara hii kuwa na madeni makubwa kama vile deni la ununuzi wa mbolea ambapo hadi Kamati ilipoitembelea mnamo mwezi wa Mei, 2013 Wizara hii ilikuwa inadaiwa takriban Tshs. 1.6 bilioni na Kampuni ambayo imeshinda tenda ya kuagiza mbolea iliyopo huko Tanzania Bara, hivyo tunaiagiza Serikali kufanya juhudi za makusudi ili kuweza kulipa deni hilo kwa haraka iwezekanavyo.

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

Mhe. Spika, Idara hii imejipangia malengo kadhaa yakiwemo utayarishaji wa Rasimu ya Sheria pamoja na sera mbali mbali, kuna haja ya kufanya utafiti wa kina na kujua ni sheria zipi ambazo zimeshapitwa na wakati na kuzifanyia marekebisho ili sheria hizo ziende sambamba na hali halisi ilivyo hivi sasa mfano sheria ya ada za machinjio na nyengene nyingi zinoneka kuwa na viwango vya chini sana katika ada hiyo kiasi ambacho hata kama ada hiyo itatozwa haitaweza kusaidia chochote katika shughuliza za uendeshaji wa machinjio hayo.

Mhe. Spika, kwa mwaka huu wa fedha 2013/14 Wizara inatarajia kutayarisha sheria mpya ya mbegu zinazosimamia sekta ya kilimo jambo hili ni la faraja sana la linafaa kupongezwa kwani hali ilivyo hivi sasa wakulima pamoja na wafanya biashara wetu wengi wamekuwa wanaleta mbegu za mazao mbali mbali kutoka sehemu mbali mbali bila ya kujua ikiwa mbegu hizo huko zinakotekea kama zilikuwa katika hali ya usalama ua laa. Sheria hiyo itakapomalizika itasaidia kuepukana na uingizaji wa mbegu ambazo sio salama na ambazo hazijulikani nasabau zao.

PROGRAMU YA USARIFU WA MAZAO

Mhe. Spika, ujenzi wa Kituo cha usarifu wa mazao cha Kizimbani umefikia hatua ya kuridhisha na tunawapongeza wafadhili wetu KOICA. Tunaomba Serikali kuona umuhimu wa kukimaliza haraka kituo kile ambacho ni muhimu sana hasa ukizingatia kuwa katika kisiwa chetu kuna mazao mengi ya matunda hupea na kuwiva kwa wakati mmoja na baadae matunda hayo yanaharibika kwa vile hakuna sehemu na mbinu za kuyahifadhi.Kuna kila sababu ya kukiwekea mkazo zaidi wa kumalizwa kwa kituo hicho na Serikali.

Mhe. Spika, juhudi za Mfadhili KOICA zilikuwa ni kubwa sana na hatua iliyobakia ni ndogo na jambo la faraja zaidi kuwa kemikali (Reangent) zinazohitajika kutumika katika kituo hicho tayari zimeshanunuliwa na hofu yetu kuwa huenda zikaharibika ikiwa zitaachwa kwa muda mrefu bila ya kuzitumia.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Spika, Idara ya utumishi ina jukumu kubwa la kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuwawekea mazingira mazuri ya kazi. Jukumu hili katika

Wizara ya kilimo bado halijatekelezwa ipasavyo kwani kuna idadi kubwa ya Wafanyakazi wanafanyakazi katika mazingira mabaya na yanayohatarisha usalama kwa afya zao Kamati yetu katika kazi zake za kwaida ilitembelea chuo cha kilimo kizimbani na kushuhudia msongamano mkubwa wa Wafanyakazi katika vyumba vidogo sana na ambayo vyumba hivyo vyengine ni maabara za kufanyia uchunguzi wadudu, wafanyakazi hao wapo kwa muda mrefu sasa takribani miaka mitatu.

Mhe. Spika, sote tunaamini kuwa mazingira mazuri ya kazi yanapelekea kuwepo kwa ufanisi katika kazi.na kufanya kazi bila ya kuwa na vitendea kazi hatutaweza kupima ufanisi wa kazi. Hivyo tunaishauri Wizara kuwapatia wafanyakazi wale sehemu nzuri ya kufanyia kazi na pia vitendea kazi vyote muhimu kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kazi Suala la usafiri kwa wafanyakazi, malipo ya fedha za likizo na malipo yakufanya kazi baada ya saa kazi (overtimie) ni miongoni mwa haki za msingi ambazo mfanyakazi anastahiki kupatiwa na muajiri wake.

Mhe. Spika, Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo haijaridhishwa na msongamano wa wafanyakazi katika majengo ya maabara yaliyopo Kizimbani hivyo tunaagiza Wizara kulitafutia ufumbuzi wa kudumu suala la wafanyakazi ambao wamehamishiwa katika Maabara ya wadudu iliyoko Kisimbani haraka iwezekanavyo.

Mhe. Spika, suala la kuyahakiki mashamba na Mali za Serikali limeshakua ni la muda mrefu na kukamilika kwake bado hatuelewi ni lini, bado mashamba, majengo, magari na mali nyengine nyingi za serikali hazijatambuliwa wala kupatiwa hati miliki. Uvamizi wa mashamba ya Serikali na wananchi imekua ni jambo la kawaida. Hivyo, Kamati inashauri katika Bajeti hii zitengwe fedha maalumu kwa ajili ya kulisimamia zoezi hili ili lifanyike na kumalizika kabisa.

Mhe. Spika, jambo muhimu ambalo Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo inapenda kusisitiza ni suala la mafunzo ya wafanyakazi katika fani mbali mbali. Kuna upungufu mkubwa wa wataalamu muhimu sana katika Wizara ya Kilimo pamoja na kuonekana kuwa ni Wizara iliyo na wataalamu wengi katika Serikali hii.Fani muhimu na adimu sana ni ya daktari wa mifugo kwa hapa Zanzibar tunathubutu kusema hakuna wataalamu wa fani hiyo ingawa tuna mifugo mingi ya kila aina.

Mhe. Spika, aidha. mafundi wahandisi ambao wana uwezo wa kutengeneza zana au pembejeo za kilimo na wakati huo huo wawe na uwezo wa kuelewa mambo ya umwagiliaji maji, fani hizo pamoja na nyengine hata watafiti wenye sifa ya kuweza kufanya tafiti za kilimo katika Taasisi ya utafiti wa kilimo ni kidogo sana, kwa hali ilivyo hivi sasa upungufu huo inasababisha kuzorota kwa maendeleo ya kilimo, hivyo ni vyema tukawa na mpango madhubuti wa kuwaendeleza wafanyakazi tulionao kwa kuwangoeza ujuzi pamoja na kuwa elimu ina gharama.

IDARA YA KILIMO

Mhe. Spika, miongoni mwa majukumu ya Idara ya Kilimo ni kusimamia maendeleo ya uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao ya biashara,upatikanaji na usambazaji wa huduma za pembejeo na zana za kilimo.Kamati inaishauri Wizara kuangalia kwa jicho la huruma Idara hii kutokana na majukumu yake muhimu ambapo kilimo chote kinashughulikwa katika idara hii kwanza ni lazima fedha za kununulia mbolea zitolewe kwa wakati na kwa kiwango kile ambacho kilichokusudiwa kutolewa sio kwa upungufu, hali iliyojitokeza mwaka huu hatukufurahishwa kuona kwamba deni la fedha za mbolea limekaa muda mrefu bila ya kulipwa hadi kufikia msambazaji wa mbolea hiyo kuleta mbolea kwa upungufu.

Mhe. Spika, Idara hii inajukumu la kuwaelimisha wakulima juu ya mbinu za kilimo bora ikiwemo matumizi mazuri ya mbolea pamoja na kuchagua na kutumia mbegu bora zitakazowaleta matunda bora. Kwa hali ilivyo hivi sasa wakulima wengi hawajui namna ya kuchagua mbegu bora na matumizi mazuri ya mbegu hizo.

Mhe. Spika, tunaipongeza Serikali kwa kuwapatia wakulima wa Mpunga mbegu za mpunga kwa bei nafuu ya kilo moja kwa Tshs mia mbili tu (200/-) ili na wao waitumie kwa kuzalisha mbegu nyengine. Ni wazo zuri sana na kwa kiasi fulani juhudi kubwa zinafanyika kuwapatia wakulima mbegu hizo za mpunga lakini utekelezaji wa jambo hili unatia mashaka ikiwa unatuletea matunda hasa tunayoyahitaji, kwani changamoto iliyopo ni kuwa wakulima walio wengi kutokana na ukosefu wa elimu wanatumia mbegu kwa matumizi yao ya kawaida ya nyumbani yaani wanatumia kwa ajili ya chakula.

Mhe. Spika, mpunga huo haufai kutumika kwa matumizi ya chakula kwa vile umetayarishwa na kuwekwa kemikali kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu tu na sio vyenginevyo. Kitendo kinachofanywa na baadhi ya watu kutumia mpunga huu kwa chakula kimeshaanza kuleta madhara kwa baadhi ya watu ingawa sio makubwa. Hata hivyo inatarajiwa kuwepo kwa madhara makubwa hapo baadae ni vyema Wizara ikawaelimisha wananchi juu ya hatari na madhara yanayoweza kusababishwa na kutumia mpunga huo kwa chakula na pia kukosekana kwa lengo la upatikanaji wa mbegu hiyo.

Mhe. Spika, **k**atika utekelezaji wa bajeti ya mwaka uliopita unaonesha kuwa kuna vipindi 10 tu vimetayarishwa na kurushwa hewani kuhusu uzalishaji na uendelezaji wa mazao ya chakula, utunzaji na uhifadhi wa mazingira, na wakulima 80 tu wamepatiwa mafunzo ya udhibiti wa wadudu na maradhi ya mimea kwa kutumia dawa asilia. Kamati inaona Idadi hii ni ndogo sana na inajionesha wazi wazi kuwa kuna idadi kubwa ya wakulima waliopo vijijini ambao bado hawajafikiwa na taaluma hiyo.

Mhe. Spika, Kama tulivyotangulia kusema kuwa Idara ya kilimo ndio Idara mama katika Wizara hii ya kilimo idara hii, inahitaji kutengewa fungu maalum kwa ajili ya kazi zake na iangaliwe katika matazamo maalum . Wakulima wakishapewa mafunzo juu ya kutumia mbinu za kilimo bora au matumizi ya mbolea kunahitajika kufuatiliwa kuona ikiwa mkulima anaendelea vizuri au kuna kasoro fulani katika utendaji wake.

Mhe. Spika, kwa hivyo mabibi shamba na mabwana shamba huhitajika katika mashamba ya wakulima hao mara kwa mara, lakini jambo la kusikitisha ni kuwa wakulima hawa hawawezi kupitiwa mara kwa mara kwa vile hakuna usafiri wa uhakika wa kuwapeleka mabibi shamba na mabwana shamba katika mashamba ya wakulima. Hivyo, ni vyema Wizara ikawapatia wataalamu hawa usafiri ijapokuwa wa mapikipiki ili kuwarahisishia kazi zao.

Mhe. Spika, kuna haja kubwa ya kutengenezwa kwa miundombinu ya umwagiliaji maji katika shamba la Bambi ili liweze kutumika katika kilimo cha umwagiliaji maji kwani kwa hivi sasa zimeweza kutumika ekari 3 tu wakati shamba hili lina ekari 25 katika shamba la Bambi ambalo linazalisha mazao mbali mbali kama mtama mahindi na mboga mboga

KITUO CHA UTAFITI WA KILIMO KIZIMBANI

Mhe. Spika, Kituo cha Utafiti wa Kilimo Kizimbani kina historia ndefu na ni miongoni mwa vituo vikongwe sana katika ukanda huu wa Afrika Mashariki. Majukumu yake ni kufanya utafiti wa mazao ya biashara na pia mazao ya chakula na mkazo zaidi ni kwenye zao la mpunga. Tuanipongeza Serikali hii

ya awamu ya saba (7) kwa kutoa msukumo mkubwa katika sekta ya utafiti wa kilimo hapa Zanzibar kwa kunyanyua baadhi ya taasisi za utafiti wa kilimo Zanzibar.

Mhe. Spika, mafanikio ya utafiti katika miaka ya hivi karibuni yaliyopatikana ni pamoja na kugundulika kwa mbegu mpya za muhogo kama Kizimbani, Mahonda, Kama Machui na kupatikana kwa mbegu mpya za mpunga NERICA 1,10,12). Mafanikio hayo yanaweza kuwa endelevu ikiwa hatukuwa na changamoto za ukosefu wa wataalamu bingwa katika program mbali mbali za utafiti, uchakavu wa miundombinu ya majengo ya Ofisi, maabara za kufanyia uchunguzi maalum (screen house) na vile vile fedha za kutosha za kufanyia utafiti.

Mhe. Spika, nchi zote zilizoendelea katika sekta ya kilimo zimekuwa zikitoa kipaumbele katika masuala ya utafiti kwa kuwapatia nyenzo, vifaa na utaalamu wafanyakazi wa utafiti.Tukiangalia bajeti ya mwaka jana Taasisi imetengewa Shillingi Millioni Mia Nnne (Tsh 400,000,000) kwa kazi za maendeleo hata hivyo hadi kufikia Mwezi wa Juni,2013 Taasisi imepata Shillingi Millioni Arobaini na Moja (Tshs 41,000,000) sawa na asilimi 10.Tunapaswa kujiuliza asilimia kumi tu ya fedha za maendeleo inaweza kutekeleza malengo ya Taasisi?. Jambo la kushangaza zaidi ni kuwa katika mgao wa bajeti hii, fedha zilizotengwa ni Shillingi Mia Moja Arobaini Millioni tu (Tshs 140,000,000/-) hali hii ni ya kusikitisha sana.

Mhe. Spika**,** kituo cha utafiti cha Matangatuani Pemba kipo katika hali mbaya sana, katika kituo hicho hakuna kifaa hata kimoja cha kufanyia utafiti unaoweza kufanyika katika kituo kile ni utafiti wa kujua aina za udongo tu, kutokana na ukosefu wa vifaa vya kutendea kazi, ukweli wenyewe ni kuwa Matangatuani hakuna kituo cha utafiti, kuna ofisi tu. Hivyo.ikiwa Wizara imeamua kufanya utafiti basi ianze kukiimarisha kituo kile ambacho ni muhimu sana kwa maendeleo ya utafiti.

CHUO CHA KILIMO KIZIMBANI

Mhe. Spika, Chuo cha Kilimo Kizimbani ndicho tulichokipa dhamana ya kutoa mafunzo katika fani za kilimo na mifugo. Tuaamini kuwa wanafunzi wanaohitimu katika chuo hicho wanakuwa wana maarifa ya kutosha ya kuweza kuwasaidia wakulima wetu vijijini. Chuo kina uhaba wa walimu, vifaa pamoja na kukosekana huduma muhimu chuoni hapo kama vile maji na gari la kuchukulia wagonjwa pindi ikitokea dharura wakati wa usiku.Pamoja na kuwa Serikali haina uwezo lakini kwa suala la upatikanaji wa maji ya uhakika na gari la kuchukulia wagonjwa ni muhimu na Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo haitaweza kuvumila kuona wagonjwa na wanafunzi

wanahangaika kutafuta maji. Hivyo tunamuomba sana Mheshimiwa Waziri aje atupe maelezo yaliyotimia juu ya mpango wake wa kuwapatia maji na gari ya wagonjwa kaika Chuo cha Kilimo, Kizimbani.

Mhe. Spika**,** kuna wahitumu wengi ambao bado hawajapata ajira na wazurura mitaani, tunaishauri Serikali kuwapa kipaumbele wale wanafunzi ambao wamemaliza katika chuo hicho kwa kuwaajiri ili kupunguza suala la uhaba wa waalimu. Aidha kutokana na mahitaji mengi yanayohitajika katika kujiendesha chuo ikiwa ni pamoja na huduma mbali mbali zinazohitajika kutolewa kwa wanafunzi kama kuwapa huduma ya malazi chakula vifaa mbali mbali vya kujifunzia nakadhalika. Tunaishauri Serikali kuongeza ada kwa wanafunzi wanaojiunga hapa ili chuo kiweze kukidhi gharama za uendeshaji.

Mhe. Spika, Tarehe 14 Mei 2013 Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ilitembelea Chuo cha Kizimbani na kutembelea maktaba ya chuo,maktaba yake ni nzuri na ina vitabu vingi na muhimu kwa wakulima na wafugaji .Napenda kuchukua fursa hii kuwashajiisha Wawakilishi wote wa Baraza lako tukufu pamoja na Wananchi kwa ujumla kujenga utamaduni wa kujisomea hasa katika maktaba hiyo kwani kuna vijarida muhimu vinavyohusiana na mambo ya ufugaji na ukulima wa kisasa na ni miongozo mizuri kwa wakulima. Ni vizuri kama tutajenga tabia ya kujisomea kabla ya kuanza kufuga au kuanza shughuli yeyote ya ukulima.

IDARA YA MISITU NA MALIASILI ZISIZOREJESHEKA

Mhe. Spika, Idara hii ina jukumu la kulinda na kuhifadhi misitu ya asili na wanyama pori, hivyo ni wajibu wa idara hii pia kuhakikisha kuwa kuna udhibiti mzuri na utaratibu mzuri wa kukata miti na upandaji wa miti mwengine,suala la misumeno ya moto bado ni tatizo kubwa kwani watu wengi wanaitumia kwa njia za siri .Ushauri wetu ni kuwa pindi misumeno ya moto inapokamatwa basi ni busara zaidi misumeno hiyo ikatiwa moto ikiwa tumeshindwa katika kuizuia isiingizwe nchini, basi dawa yake ni kuiteketeza.

IDARA YA UHAKIKA WA CHAKULA NA LISHE

Mhe. Spika, Idara ya uhakika wa chakula na lishe inajukumu la kuratibu utekelezaji wa masuala ya uhakika wa chakula na lishe Nchini ikiwa ni pamoja na kuanzisha hifadhi ya chakula Zanzibar. Kamati yetu haijaridhishwa na utekelezaji wa mradi huu kwani bado jukumu la msingi la kuanzisha hifadhi ya chakula halijatekelezwa. Kutokana na umuhimu wa hifadhi hiyo hapa kwetu tulielezwa kuwa kuna baadhi ya mambo hayakutekelezwa kutokana na uhaba wa fedha hivyo Kamati yetu imeamua kupunguza fungu

katika mradi wa kuimarisha mikarafuu kiasi cha Shillingi Millioni Arobaini (Tshs 40,000,000/-) na kuongezea katika Idara hii ili waweze kutekeleza majumkumu yao ya msingi kwa wepesi zaidi.

Mhe. Spika, **m**wisho kabisa napenda kukushuruku wewe tena kwa kunipa nafasi hii na pia kuwashukuru wajumbe wako wote kwa kunisikiliza.

Mhe. Spika, **n**aomba kuwasilisha na pia naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe tunakwazwa na muda sana, tena na hapo mbele tunakaribia kumalizia mfungo mtukufu wa Ramadhan. Sasa shughuli zetu hizi tuziharakishe ili tuweze kurudi na kuungana na familia zetu tumalize mfungo huo na hatimae kukaa na familia kwa ajili ya siku kuu. Lakini pili fedha ambayo ilikuwa imetengwa kwa ajili ya mkutano huu imemalizika, kwa mujibu wa ratiba yetu bado kuna Wizara kama tatu na hii ambayo tunaanza leo ya nne inaweza ikachukua si chini ya wiki kwa utaratibu huu ambao tunakwenda. Hivyo Waheshimiwa Wajumbe tunaomba tuzingatie hilo katika mchango na nategemea tuje na utaratibu wa kuwezeshwa shughuli zetu hizi kufanywa kwa ufanisi lakini wakati huo huo kuzingatia muda tulionao, lakini pia zaidi kuzingatia matumizi ambayo yametengwa katika kumaliza mkutano huo wa bajeti. Tutakaa ili tuone na hatimae tutakuja kwenu Waheshimiwa Wajumbe ili mutusaidie ni namna gani tunamaliza shughuli zetu kwa ufanisi lakini kwa muda mfupi zaidi uliobaki lakini tumemaliza shughuli zetu zote.

Tuanze kuzingatia sasa kabla hatujaja na huo utaratibu ambao tutaomba Waheshimiwa Wajumbe muje kuunga mkono tuweze kufanya shughuli zetu na kumaliza ikiwa hatujazidi mno, tayari tumezidi lakini tusizidi mno na itatupunguzia uwezo wa mikutano mengine ya kawaida kuweza kwenda kwa ufanisi mzuri. Tuanze kuzingatia sasa kutokana na michango yetu kwa kupunguza muda, kujipanga vizuri kwenda kwenye *point* moja kwa moja ili kupata wachangiaji wastani wa kiasi kuchangia hotuba zilizobakia.

Mhe. Saleh Nassor Juma:Ahsante sana Mhe. Spika, kwa sababu ya muda niende moja kwa moja katika hoja lakini naomba nianze kwa usemi unaosema kwamba mapendeleo yakiachiliwa mbali uhuru wa mafanikio humulika kwenye ukweli siku zote kulikoni uongo. Nimelazimika kutoa nukuu hii baada ya kuliendesha vyema hili Baraza letu kwa kweli nimevutika sana na jinsi ulivyoi-*handle* ile hoja ya Mhe. Hamza, mpaka ilipofika na laiti ingelikuwa nina uwezo basi naamini kwamba hivi sasa ingelikuwa ninakwita *professor*. Baada ya dibaji hiyo naomba niendelee na hoja.

Mhe. Spika, nianze katika ukurasa wa 22 wa kitabu chetu hiki, ibara ya 6.2 ambapo kumezungumziwa suala zima la Taasisi ya Utafiti. Mhe. Spika, kama nchi inataka kupata maendeleo kupitia kilimo basi haina budi kuweza kuwa makini na kuiboresha sana Taasisi ya Utafiti. Mhe. Spika, taasisi hii ni muhimu sana katika maendeleo ya kilimo na wananchi wanaotegemea hicho kilimo, kwa kiasi hicho nchi nyingi hizi zilizoendelea ambazo tayari zinaendelea zilitegemea sana kilimo lakini ziliboresha sana taasisi za utafiti katika nchi zao.

Mhe. Spika, ninasikitishwa sana kwamba sisi tunasema kwamba kilimo ni uti wa mgongo wa taifa letu hili lakini huku bajeti yake iliyotengewa taasisi hii kama alivyosema yule msemaji wa hii kamati yetu kama ni shs.140,000,000/=, hawa watafiti achilia mbali kufanya tafiti zao pale ndani lakini hata kama wanataka kupata uzoefu wa nchi nyengine zinazofanya utafiti wanashindwa, shs.140,000,000/= kunipatia mimi nikaambiwa nizitumie kwa shughuli zangu binafsi kwa kipindi hiki cha mwaka mmoja basi nitalazimika uniongeze. Je, taasisi muhimu kama hii, kwa kweli Mhe. Spika, inaonekana serikali haiko *serious* katika kukiinua kilimo, haiko *serious* katika suala zima la kuinua maisha ya wananchi kupitia hichi kilimo.

Mhe. Spika, Japan kabla ya kujikita katika viwanda hawa walikuwa wanategemea kilimo kwa ajili ya uchumi wa nchi yao. Mhe. Spika, asilimia 45 ya bajeti ya Japan katika kipindi hicho waliisukuma katika kilimo hususan katika tafiti na katika miaka ile ya *1930s* Wajapan ndio waliokuwa wanaongoza kwa kuzalisha mchele kwa sababu walikuwa *serious*, ndio waliotuongoza katika kuzalisha matunda, ndio waliongoza katika kuzalisha mazao ya mizizi kwa sababu asilimia 45 ya bajeti yake ilijikita kwenye suala zima la kilimo tena katika utafiti.

Mhe. Spika, Wajapani natoe uzoefu kidogo wa nchi. Wajapani wakati wanafanya tafiti walikuwa wanazalisha kitu kinaitwa *Japanese peshori,* yaani mchele ule mrefu wa ki-Japani kama basmati, walitumia pesa nyingi wakaweza kuzalisha. Mnamo mwaka 1857 kuna *scientist* mmoja pale wa ki-Japani katika kufanya tafiti aliweza kugundua kichocheo cha ukuzi mti, hichi kikuzi mti kama utaukuza katika mche wa mti hasa mpunga basi mbegu moja ya mpunga ilikuwa inatoa miche karibu 60. Kwa hivyo walifanikiwa wa-Japani kumtumia huyu mtafiti kwa kuweza kuzalisha mpunga mwingi katika sehemu ndogo tu. Sasa sisi Wazanzibari katika hili tunatangaza sijui kilimo cha kufa na kupona, mapinduzi ya kilimo lakini hatuwawezeshi wenzetu, yaani katika sehemu yenye wataalamu wengi ni Wizara hii ya Kilimo, pale kuna madaktari katika masuala kadhaa, kuna watu wana *degree* mbili mbili. Mimi nawafahamu wana uwezo lakini elimu yao iko *statistics* haiko *dynamic* kwa sababu hawawezeshwi kufanya kazi.

Mhe. Spika, sasa mimi nadhani kama kweli tunataka tuwasaidie Wazanzibari, kama kweli tunataka tufanye mapinduzi ya kilimo katika nchi hii basi bajeti ya Wizara hii hasa sehemu ya utafiti kuna haja ya kupanuliwa sana kabisa kabisa.

Mhe. Spika, mimi katika kijiji changu cha pale Vitongoji mara nyingi tunategemea kilimo kwa ajili ya maisha, kilimo ndio chakula, kilimo ndio biashara, kilimo ndio tunawasomeshea watoto wetu, kilimo ndio tunaojengea nyumba zetu, kilimo ndio tunakwendea Mecca kabisa kabisa Mheshimiwa. Inasikitisha sana sasa hivi yaani kama utakwenda pale kwangu Vitongoji wale wazee walio na miaka kuanzia 70 ambao tulikwenda Mecca basi ni kupitia mazao ya kilimo, inasikitisha sasa kwamba hivi sasa achilia mbali kwenda Mecca kuhiji hatumudu hata kupata kula yetu ya miezi sita kutokana na kilimo kwa sababu kilimo sasa hivi ni tatizo.

Mhe. Spika, sisi tunalima njugu mawe pale na njugu nyasa kama mazao yetu ya biashara. Aidha tunalima mahindi pamoja na mpunga kama mazao ya chakula lakini inasikitisha Mhe. Spika, katika kipindi karibu cha miaka kumi na tano kunguni mgunda hatuwezi kumtibu pale, mahindi hatuyavuni vizuri kwa sababu ya kunguni mgunda. Maembe tunashindwa kusafirisha kwa sababu ya mafunza, tunayo miembe mingi, tunavuna sana maembe lakini bado tunashindwa. Sasa tatizo liko wapi, tatizo ni kwamba hawa watafiti wanashindwa kutupatia hata dawa. Sasa mimi ninadhani Mhe. Spika, tuwawezeshe wataalamu wetu hawa ili watuwezeshe sisi kuishi, watuwezeshe sisi wafanyabiashara wa mazao, watuwezeshe sisi kumudu maisha yetu, kinyume na hivyo Mhe. Spika, barabarani siku hizi unaona mashaka yaliyomo mule, ukipita huyu lete hichi, lakini akinamama pale walikuwa wakilima njugu wenyewe wanapungua mabarabarani kuomba. Sasa naomba Serikali itusaidie sana kuboresha kilimo kusudi kuweza ku-*create employment* kwa watu wetu.

Mhe. Spika, mabadiliko ya tabia nchi na kilimo, haya mpaka haya mabadiliko ya tabia nchi tutegemee sisi wakulima kwamba kuanza kuyarekebisha. Inasikitisha sana Mhe. Spika, kwamba nyie mnaleta mbegu ile ya Nerika, sasa ukileta mbegu hii ukiichukua ukiipanda Mkoani na ukanda huu wa Magharibi kwa Pemba utavuna vizuri tu, lakini njoo nayo sasa mbegu ile ile ya Nerika uianze Muwambe kwao Mhe. Hija kupita nayo humu Kengeja mpaka kufika Micheweni huwezi kuvuna, nyie mnatuletea mbegu ya Nerika, lakini angalieni sasa kwa nini Magharibi wavune Nerika, kwa nini sisi Mashariki tusivune vizuri. Mimi nadhani kuna *technical error* kwa hawa wataalamu na nadhani si kwa sababu ya taaluma zao ni kwa sababu hamuwawezeshi kufanya tafiti vizuri. Ukichukua Nerika ukiupanda huku Mkoani kwa sababu

infiltration of water ni ndogo lakini ina *grow well*, lakini Nerika ile ile njoo uilete kwangu Vitongoji ambapo *soil* ina *culcium carbonate* na *infiltration of water* ni kubwa huwezi kuvuna. Sasa mimi nadhani kuwe na *Nerika 1A* ambayo matumizi yake ni kwa ajili ya ukanda ule wenye *soil* nzuri. Kwa mfano kuanzia Makombeni hadi kufikia Konde. Sasa suala hili ili tuweze kuboresha tuwawezesheni hawa wataalamu hapo juu waweze kufanya tafiti kuona kwamba hichi kitu wanachokifanya kuona kwamba hichi kitu wanachokifanya katika sehemu za Zanzibar zenye kuleta mbegu zinazofaa sio walete tu mbegu. Mimi nadhani tuwawezesheni hawa wapatiwe bajeti watufanyie utafiti vizuri ili hayo mapinduzi ya kilimo yaweze kwenda ili sisi tuweze kujiajiri vizuri.

Mhe. Spika, suala jengine katika suala hili hili la kilimo sisi tuna tatizo jengine kubwa wakulima, mimi ni mkulima na mfugaji. Mhe. Spika, kama mkulima napata tabu, mazao ya kilimo unakuwa huna uwezo wa kuyahifadhi, ina maana kwamba lazima ukishavuna uyapeleke ukayauze, sasa *supply* ikiwa kubwa basi *demand* inapungua na *demand* ikipungua *price* nayo inakuja chini. Sasa tunalazimika sisi kuuza tungule zetu pale kwa bei ya chini kabisa kabisa kwa sababu kipindi kile cha mavuno *production* inakuwa kubwa bei lazima iteremke, hatuna mbinu za kuweza kupambana na bei za mazao kwa nini, halafu nyinyi wataalamu hamutusaidii kuweza kuona kwamba haya mazao yetu yanasubiri soko kwa nini.

Mhe. Spika, mimi nilitembelea katika nchi moja sitaki niitaje lakini katika kutembelea nilipelekwa kwa wakulima wenzangu. Mhe. Spika, kuna *gas* fulani wanatumia katika mazao, mazao yanavunwa yanakuwa *stable* sehemu wala hawaweki kwenye mabaridi, wanaweka kwenye *syntihetic gas* tu na wakishaweka mazao yale yanaweza yakakaa hapa mwaka mzima kwenye *store* hayajaoza wala hayawivi na wakitaka kuyawivisha wanakwenda kumwaga tena *syntihetic gas* nyengine wanamwaga basi baada ya dakika kumi tu ukiikamata ndizi imewiva. Sasa kwa bahati hiyo nchi tuliyokwenda sisi tulipata uhuru mwanzo kuliko wao, sasa sijui ni nini wao wakaweza kufanya mambo wakati wamepata uhuru juzi tu, sisi tunashindwa tatizo liko wapi, uchumi, sidhani. Kwa sababu wale na wao wakati huo walikuwa na mawe vile vile hawana mafuta sasa sisi tunayo tumeyakalia. Sisi tunataka tujue tu ni nini kinachosababisha hivi. Tunaomba msaada kwa sababu Mheshimiwa mimi ni mwananchi na nimesimama hapa kwa niaba ya wananchi tena wa chini kabisa wanaotegemea kilimo, hivi nyinyi miaka yote hii 50 tangu tupate uhuru mmeshindwa kweli kuwasaidia wakulima kwa kuweka *storage system* walizonazo wenzetu, mambo haya mpaka lini au serikali hii haikui ni kokoto?

Mimi nashangaa sana, nilikwenda kutembelea ile Majlisi Shuraa na Majlisi Dawlah nikapata nafasi baadae ya kutembea tembea mule. Mhe. Spika, inashangaza sana wao wanafanya *filling* kwenye majabali yale halafu wanapanda nyanya. Hivi sasa eti sisi tunatumia *tomato paste* kutoka Oman ambapo wao wenyewe ni majabali matupu. Sisi hapa tunapata mvua *twice a year* au *triple a year*, *we can't afford even to can our tomato, why*.

Mhe. Spika: Mheshimiwa rudi rudi kwenye Kiswahili zaidi, tena umalize hotuba yako katika muda wa dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante Mhe. Spika, unajua nilikuwa nazungumzia mambo ya utaalamu sana. Mhe. Spika, sawa nitajitahidi sana, lakini naiuliza serikali kwa nini sisi tununue *tomato paste* kutoka Oman ambapo ardhi yao kubwa ni mawe tu na sisi nyanya tunazo hapa kwa nini hatuzi-*canned* mkatusaidia kupata soko sisi wakulima wa tungule pale Vitongoji tukaja tukawauzia viwanda vyao, serikali hawana uwezo basi hata kuwaruhusu watu kwamba ekezeni katika viwanda msiwekeze katika kuku hawa wa paja nono na badala yake wekezeni kwenye viwanda vya kusindika tungule tukapata angalau soko, tunalazimika kuuza tungule sisi kwa bei ya kutupa tu kwa sababu hakuna *canning industry*, kwa nini huu si uhasada jamani dhidi yetu.

Mhe. Spika, mimi nadhani hii dakika 5 nimalizie kwa misitu. Mhe, Spika, wanasema watapanda miche milioni moja ya mikarafuu. Ona sasa tatizo liliopo, mikarafuu hii wanayotaka kupanda miche milioni moja imeingia hapa tangu *century* ya 17 ambapo aliingiza mfanyabiashara wa Ki-Oman anayeitwa Saleh Buhamirel. Mikarafuu hiyo haijabadilishwa kitu. Mimi nadhani kama wa-Japani walivyofanya mbegu moja ya mpunga kuweza kutoa miche karibu 20. Kwa hivyo nadhani na sisi tufanye maarifa hii miti yetu ya mikarafuu tuifanyie *modification* kidogo badala ya kuwa mirefu tangu ile aliyoipanda Saleh Buhamirel wanawake ndio wachumaji wakuu wa karafuu hawaiwezi tena. Sasa hebu tuifanyie *modification*.

Mimi ninachokuhakikishia juzi moja niliambiwa eti inapoteza *quality*. Mhe. Spika, katika kitu ambacho hakitapotea ni *quality*, sisi tunakwenda katika mambo ya *genetically* kuipandisha pandisha ikawa inazaa sana. Sasa mimi nadhani katika hili tusaidiwe kusudi tuweze kupata mkarafuu huu uliokuwa mzuri na ambao unazaa sana na unaochumika ili akinamama waweze kupanda.

Kwa mfano, pale pangu mimi Vitongoji huwa tunakwenda kupanda na wanawake sasa inabidi tuwakatie matawi ambapo tunaiuwa. Mimi nadhani

wao wenyewe mikarafuu midogo midogo akinamama wataweza kupanda tukii-*modify* hiyo mikarafuu au pia nalo hawaliwezi hilo.

Mhe. Spika, sasa katika suala zima la mambo haya ya misitu. Mhe. Spika, hivi sasa wana kazi kubwa hawa wizara. Hivi sasa kutokana na misitu mingi kuwa imepotea kama mivule, mikangazi, mibuyu jambao ambalo linaathiri sana *binomial* katika maeneo yetu.

Kwa mfano Mhe. Spika, hivi sasa ndege wengi wamepotea kwa sababu miti yao waliyokuwa wakiipenda na iliyokuwa ikizaa vyakula vyao haimo. Sasa hivi ukiangalia kuna *species* ya ndege wanaitwa Kwau, hawapatikani tena kwa sababu tu mibuyu hamna, hawapatikani tena kwa sababu mikangazi ambayo ilikuwa inazaa mafunza na ndio chakula chao haipo. Sasa wao wasifikirie tu kupanda miti ya kiajabu ajabu tu hivi, wafikirie miti ya zamani ambayo itaweza kurudisha vizuri *binomial* Mhe. Spika.

Nimalizie mwisho kabisa Mhe. Spika, na hili suala la utafiti ambao wanasema kwamba kufanya tathmini ya miti iliyopo. Mhe. Spika, hili siku zote nalisema na nitaendelea kulisema. Mheshimiwa hawa hawakutaja wao kwamba wanapanda mivinje lakini wanaruhusu kupanda mivinje, washaifanyia tafiti sana hii mivinje? Mimi nakwambia mivinje ina matatizo nilipouliza siku moja hapa niliambiwa haina tatizo, lakini mivinje ina tatizo, mivinje inaharibu sana ardhi kwa sababu ya kufyonza maji sana.

Mhe. Spika, kuna kitu kinaitwa *transpiration* katika mambo ya miti. Huu ni upotezaji wa maji yaani ni upoteaji wa maji kutoka katika ardhi kumwaga katika hewa, mvinje una tabia hiyo sana kwa sababu unazima tundu *stomatal pores* pamoja na *lent cells* kubwa haina majani, lakini ina *lent cells* na *stomatal pores* nyingi. Kwa hivyo *lenticular transpiration* yake ni kubwa. Matokeo yake maji yanafyonzwa kwenye ardhi inapoteza mbolea na matokeo yake tunapopanda vilimo vya chakula tunapata tabu sana. Sasa naomba Mhe. Spika, wataalamu wetu katika kufanya tafiti waone kwamba huu mvinje je, hauna tatizo, mbona sisi tunaona una tatizo.

Na mwisho kabisa wanapoziba mashimo yale katika viwanda maana tumeambiwa kuchimba kwenye viwanda vya kokoto, mawe. Kuna mashimo vibaya sana Mwambe, kuna mashimo katika viwanda vya Vitongoji, Micheweni. Sasa Mhe. Spika, wanapofukia hivi viwanda basi watupandie miti mizuri kama vile mikangazi, mibuyu, miembe hii na Kwau waje tena. Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru.

Mhe. Ussi Jecha Simai: Nakushukuru Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi ya pili leo kuweza kuchangia hotuba ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2013/2014 ya Wizara ya Kilimo na Maliasili.

Mhe. Spika, mimi moja kwa moja nitakwenda katika hoja ya michangio yetu. Mhe. Spika, la kwanza mimi naanza na Idara ya Kilimo hapa zaidi nitazungumzia suala la mabonde ya mpunga hasa yale ya bonde la Mbuzini.

Mhe. Spika, bonde la mpunga la Mbuzini ambalo kuna Mbuzini 'A', 'B' na 'C' ikiwemo Kibokwa na maeneo mengine limevamiwa na wakulima, wakulima ambao wanabadilisha ile dhamira ya bonde lile la upandaji mpunga badala yake sasa hivi limevamiwa kwa upandaji wa miti aina ya miembe. Mhe. Spika, zaidi ya ekari kumi tayari zimevamiwa na kupandwa miembe. Kwa hivyo, ile dhamira hasa iliyokusudiwa ya bonde hili basi imeondoka kabisa na wananchi wameanza kubadilisha huo mfumo. Kwa hivyo, hapa naiomba wizara inayohusika ifanye jitihada zake moja ya kuzuwia huo upandaji wa hiyo miembe lakini pia watupe hiyo tathmini iliyofanywa hivi karibuni juu ya eka ngapi hasa zilizovamiwa kwa upandaji wa hiyo miembe na ikisha wizara itueleze pengine ina mpango gani wa dharura wa kuweza kunusuru hili bonde ili lisiendelee kuvamiwa na wananchi wetu ambao wanapanda hii miembe.

Mhe. Spika, jengine katika idara hii kuna suala la madereva wa matrekta wale wakulima wetu kule. Kwa muda mrefu Mhe. Spika, madereva hawa hawana vifaa vya kujikinga na vumbi ama vifaa vyengine vya kuhifadhi afya zao. Kwa mujibu wa sheria ya kazi nataka kwamba wafanyakazi wawe na vyombo maalum ambavyo vitawalinda ili afya zao zisiharibike. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze kwa mwaka huu wa fedha wizara yake ina mpango gani wa kuweza kuwanusuru wafanyakazi wetu hasa hawa madereva ambao wanaathiriwa sana na lile vumbi ambalo wanakuwanalo kule bondeni.

Mhe. Spika, jengine katika hili suala la madereva hawa kuangaliwa afya zao, kwa kuwa watu hawa hawana kinga za vumbi inawezekana wameathiriwa na hili vumbi. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atwambie ni lini wizara yake itawafanyia *checking* hawa wakulima hasa hawa madereva ambao wanakuwemo katika vumbi kwa muda mrefu.

Jengine katika Idara ya Kilimo ni masuala ya fedha za *overtime* na fedha za likizo bado ni tatizo kubwa ambalo pamoja na yote kwamba wizara na idara nyingi tunaona hili tatizo lipo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri angeliangalia zaidi hasa *nature* ya kazi ya watu hawa ni ngumu mno, hivyo wanahitaji kupewa vile vijipesa vyao angalau kidogo wajisikie na wao.

Mhe. Spika, nikitoka hapo niingie katika Idara ya Misitu na Maliasili Zisizorejesheka. Katika hili Mhe. Spika, mara nyingi masuala yangu yamekuwa yakijibiwa na Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na namshukuru kwa kiasi kikubwa ananisaidia, lakini kuna wakati masuala yangu yanaelekezwa kwake na yeye amekuwa akilalamika kusema kwamba masuala hayo hayahusu moja kwa moja katika wizara yake, lakini leo moja kwa moja masuala yangu yatakwenda kwa wizara inayohusika.

La kwanza kipindi cha msimu wa masika uliomalizika katika bonde la Chaani imepandwa miti mingi sana, lakini kwa bahati mbaya miti hii mingi iliyopandwa na mingi yao imeng'olewa na kukatwa na baadhi ya wananchi ambao wanadai kwamba maeneo yaliyopandwa miti ile ni maeneo ya kwao wao. Kwa hivyo wana shida nayo maeneo yao walime. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze hatua gani za dharura ambazo idara yake inachukua kwa ajili ya kuinusuru hii miti ambapo serikali imekula hasara kubwa sana kwa upandaji wa miti hii lakini pia kwa kuishughulikia miti hiyo.

Chengine pengine idara imejipanga vipi katika kuwaelimisha wananchi hasa wa maeneo ya Chaani na Donge ambao wanatumia sana bonde hili la Chaani Masingini kwa ajili ya kuinusuru hii miti na kuwaeleza umuhimu wake katika uhifadhi wa mazingira lakini pia kwa kuwasaidia wananchi kiuchumi.

Mhe. Spika, nikitoka hapa naingia katika Chuo cha Kilimo Kizimbani. Hapa moja kwa moja nitaanza kuzungumzia juu ya shamba la kilimo la Makurunge. Mwaka uliopita Mhe. Rais wa Zanzibar, shamba hili alilielekeza kwamba lishughulikiwe na Chuo cha Kilimo Kizimbani, lakini hadi hivi sasa shamba hili kwa taarifa zilizopo halijapatiwa hati miliki ya umiliki wa hili shamba. Sasa Mhe. Waziri atakapokuja hapa atueleze wizara yake imefikia wapi katika kuhakikisha kwamba suala la hati miliki linapatikana ili shamba hili sasa tuweze kulitumia kwa uhuru zaidi. Lakini Mhe. Spika, pia kukosekana kwa hati miliki hii inapelekea kuwakosa wale wawekezaji ambao wako tayari kutaka kuwekeza katika shamba hili ili na sisi liweze kutupatia kipato.

Jengine katika chuo hiki kuna tatizo la mishahara ya wafanyakazi ambapo mishahara hii haifanani na baadhi ya vyuo vyengine vya serikali. Kwa muda mrefu serikali tulikuwa tukiiambia na waziri anayehusika na masuala ya utumishi wa umma anatwambia kwamba kunatakiwa kufanywe kitu kinachoitwa *harmonization*, yaani kuweka ule uwiano wa walimu ama wafanyakazi wa vyuo vyote vya serikali. Lakini sasa hivi ni mwaka wa tatu unaingia serikali bado haijafanya hiyo *harmonization* na walimu wetu hawa wa Chuo cha Kizimbani pamoja na wafanyakazi na wale wa Chuo cha Utumishi wa Umma bado wanaendelea kuhangaika na kukosa hizi haki zao za msingi. Kwa hivyo, hapa Mhe. Waziri aje atueleze pengine amejipanga vipi

kuiharakisha serikali ifanye hili suala la *harmonization* ili wafanyakazi wetu hawa nao waweze kupata hiyo haki yao.

Mhe. Spika, jengine katika Chuo cha Kilimo huu ujenzi wa bweni la wanafunzi wa chuo hicho cha kilimo. Mhe. Spika, Norway wako tayari kutusaidia katika hili kwa taarifa tulizonazo lakini bado serikali inasuasua katika kuziingiza fedha ili mabweni haya yajengwe yaweze kuwasaidia wanafunzi wetu hasa wale wanafunzi wa kike. Mhe. Spika, tunaiomba serikali kwa hili basi ingeliharakisha angalau tukaingiza hizo fedha hao wafadhili wasije wakatukimbia wakatusaidia ili tukaweza kulijenga bweni hili.

Jengine Mhe. Spika, nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri ushiriki wa Chuo cha Kilimo Kizimbani katika maonesho ya nane nane keshokutwa, nakusudia mwezi huo wa nane kwamba kwa muda mrefu tumekuwa tukipata taarifa kwamba Chuo cha Kilimo Kizimbani hakishiriki hata katika yale maonesho ya nane nane kule ambapo mwakani tunategemea kwamba tutafikia miaka 50 ya mapinduzi na tunatarajia kwamba Chuo cha Kilimo Kizimbani nacho kituoneshe mambo yake kiliyoyafanya tangu pengine nchi hii kupata uhuru wake hadi hivi sasa. Sijui Mhe. Waziri hapa atakapokuja atatwambia ushiriki wa Chuo cha Kilimo Kizimbani kinashiriki namna gani katika masuala ya nane nane au pengine walimu au wafanyakazi wangapi wa chuo hiki wameandaliwa kwa ajili ya kushiriki kwa mwaka huu.

Mhe. Spika, nikiendelea mbele na kumalizia malizia tatizo la maji katika hiki chuo. Ilipokuwa ikisomwa hotuba ya mwenyekiti wa kamati alizungumzia suala la matatizo ya maji pale chuoni, maji ni muhimu na ni uhai wa mwanadamu lakini hasa katika mazingira ya chuo Mhe. Spika, suala la maji ni muhimu sana. Kwa taarifa zilizopo hivi sasa pale kunachimbwa kisima tunashukuru lakini kisima kile kinatumia mikono wanazungusha yale mabomba yao. Hapa sijui ubora wa kisima hiki utakuwaje ambapo pale pana wanafunzi zaidi ya 210 sasa hivi wanataka kutumia huduma ile ya maji na huko nyuma kiliwahi kuchimbwa kisima kama hicho hakikufanya kazi zake vizuri. Kwa hivyo, Mhe. Waziri atakapokuja atueleze pengine wamehakikisha vipi katika suala hili la kuwapatia wanafunzi maji.

La mwisho kabisa Mhe. Spika, katika Chuo hiki cha Kilimo Kizimbani suala la vitendea kazi hapo chuoni, hakina vifaa vya kutendea kazi vyombo vya kutendea kazi zao wenyewe lakini hata vile vya kufundishia. Mfano mzuri Mhe. Spika, hapa hapana hata trekta moja lile la mfano la kujaribu tu liwepo lile mfano wa wa trekta basi hapana, ambalo hilo litasaidia katika kuwafundisha wanafunzi.

Mhe. Spika, chuo hiki hasa kinafundisha kwa vitendo lakini leo mwanafunzi anafundishwa trekta kwa nadharia anaambiwa kama lile linalopita kule Maruhubi hujaliona lile, lina maringi makubwa, hivi hatuwezi tukafika pahala pazuri katika masuala hayo. Kwa hivyo, Mhe. Waziri tunamuomba, tungeliomba Idara ya Kilimo nimeona kule katika maelezo kwamba kuna matrekta kama 46 yametengenezwa basi angalau tungeliwagaiya au tungewaazima hilo trekta moja watu wa Chuo cha Kilimo wakawa wanafanyia yale majaribio kwa ajili ya wale wanafunzi ambao wanasoma chuoni hapo.

Mhe. Spika, baada ya hayo nakushukuru sana naomba nifikie hapo ahsante sana, naunga mkono lakini mpaka nitapopata baadhi ya maelezo ya hoja zangu ambazo nimezitoa. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Spika, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu (*S.W)* kwa kuendelea kutukirimu neema zake tukabaki tukiwa hai na wazima katika dunia hii na katika Baraza hili tukawa tunaendelea na shughuli za kufanya kile ambacho wananchi wa Zanzibar wametutuma ni kusimamia maslahi yao.

Mhe. Spika, nikushukuru na wewe kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika bajeti hii ya Wizara muhimu sana ya Kilimo na Maliasili. Ni bajeti muhimu kwa sababu kwa mujibu watakwimu tulizopewa tunaambiwa inawezekana mchango wake katika pato la taifa si mkubwa sana na unashuka, lakini bado inashughulisha au inatoa ajira kwa takriban asilimia 70 ya wananchi wa Zanzibar. Kwa hivyo ni sekta muhimu sana.

Mhe. Spika, nimshukuru vile vile na kumpongeza Mhe. Kaimu Waziri wa Kilimo na Maliasili, Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban kwa kuwasilisha hotuba hii vizuri kwa ufasaha mkubwa kwa niaba ya waziri wa wizara hii. Mhe. Spika, kabla sijaingia katika mchango wangu nataka kusema kwamba tunapochangia hapa tunafanya hivi kwa nia ya kuwasaidia wananchi wa Zanzibar, nataka kutoa mfano mmoja tu.

Juzi siku ya Ijumaa tulipewa taarifa na wafanyakazi wa Wizara ya Afya kwamba pamoja na kelele zote tulizokuwa tumezipiga humu ndani wakati wa bajeti ya Wizara ya Afya juu ya mapungufu mbali mbali, moja wapo likiwemo hata gesi katika vyumba vya upasuaji kwamba ilifika operesheni siku tatu imesimama mtu anataka kupasuliwa kichwa kwa sababu hakuna gesi tukaambiwa limechukuliwa hatua.

Nikasema siku ile Mhe. Spika, kwamba hatua hizi za kuchukuliwa ili kuja kututhibitisha kinyume kwa siku ile ya kupitisha bajeti hapa hatusaidiani. Juzi

tukatoa maelezo kwamba tumepewa taarifa kutoka Hospitali ya Mnazi Mmoja kuwa kwa mara nyengine tena siku tano operesheni kubwa zote zimesimama kwa sababu hakuna gesi. Nashukuru nilimuandikia hili dokezo Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais akiwa ndio mratibu wa serikali na baadae Mhe. Jaku Hashim kwa sababu tulikuwa tumebadilishana taarifa akalizungumza hapa. Tumepiga kelele Ijumaa Mhe. Spika, na tumeona kupiga kelele si neno zuri lakini ndivyo inavyoonekana humu ndani. Leo ndio asubuhi kumeteremshwa mitungi ya gesi kwenda kusababisha operesheni zifanyike katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo Mhe. Spika, tunaposema tunasaidia lakini kusema kweli inachosha mara nyengine kurejea hayo kwa hayo ikawa watendaji kama vile hawasikii. Sasa tunaposema hapa tunasema kwa niaba ya wananchi kuwasaidia, tutegemee mambo kama haya yasitokee kila wakati Mhe. Spika.

Mhe. Spika, nimeanza na utangulizi huo kwa sababu nataka kusema kwamba nataka kuanza na bajeti hii kwa masikitiko na masikitiko haya nayaelekeza kwa Rais wangu Mhe. Ali Mohammed Shein, kwamba tunaizungumza sekta kubwa kama ya kilimo ambayo nimesema katika utangulizi inajumuisha takriban asilimia 70 ya wananchi wetu. Lakini leo unakaribia mwaka waziri wa wizara hii tumeona sote kutokana na hali yake hayawezi tena majukumu haya. Mhe. Spika, sote tunampenda kaka yetu Mhe. Suleiman Othman Nyanga, lakini ukweli kutokana na hali yake hayamudu tena majukumu haya na sidhani kama ni hali nzuri katika utendaji wa kiserikali kwamba kwa mwaka mzima inakaimiwa tu. Mimi ningemuomba sana Mhe. Rais hili alitazame.

Mhe. Spika, wizara hii hata hao makaimu wanabadilika, kulikuwa na wakati Mhe. Mohamed Aboud hapa alikuwa ndiye kaimu wa wizara hii, sasa kuna Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban. Hakuwezi kukawa na ufanisi ikiwa leo watu wanapasiana kama mnapasiana mipira tu watendaji wa wizara. Hili namuomba sana Mhe. Rais alitazame sana na sijui kama hiyo ndio sababu ya hili ninalotaka kulizungumza.

Mhe. Spika, baada ya kazi kubwa ambayo ilifanyika mwaka wa mwanzo wa kuingia madarakani kwa Serikali ya Awamu ya Saba mwaka 2011 ambapo serikali ilikuja na sera madhubuti sana na tukazipongeza sote katika mjadala ambao ulichukua muda mfupi sana, ulikuwa mjadala wa Wizara ya Kilimo mwaka 2011 wakati ule Waziri Mhe. Mansour Yussuf Himid kwa sababu serikali ilikuja na mpango ule wa kutoa ruzuku, ikakata gharama nyingi kwa wakulima, kwenye mbolea, mbegu, kwenye huduma za matrekta, umwagiliaji yote kusaidia sekta hii iweze kukua na watu wakashangiria sana. Mhe. Spika, wakulima wetu walifurahi kweli lakini leo tunaripotiwa katika ukurasa wa

nne wa hotuba hii kwamba ukuaji wa sekta ya kilimo umeshuka kwa asilimia 1.3 kutoka asilimia 2.7 ya mwaka 2011.

Mimi Mhe. Spika, nahoji zaidi hapo kwamba umakini wetu hata hayo maelezo yanapelekea kushuka kwa sekta hii. Hii hotuba ya bajeti inasema hali hii imetokana na ukame na kupungua kwa maeneo yaliyolimwa kwa baadhi ya mazao makuu ya chakula ikiwemo muhogo, ndizi na mahindi. Hii ndio hotuba lakini nahoji mimi umakini wetu nikilinganisha na kitabu hiki tulichopewa na Wizara ya Fedha siku ya mwanzo kabisa, mapitio ya hali ya uchumi na utekelezaji wa mpango wa maendeleo Zanzibar, 2012/2013.

Mhe. Spika, kwenye ukurasa wa 21 kunazungumziwa katika kitabu hiki sekta ya kilimo, kitabu kinasema hivi,

> "Sekta ya kilimo imejumuisha sekta ndogo ya mazao, uvuvi na mifugo. Katika kipindi cha mwaka 2012 kasi ya ukuaji wa sekta hii imepungua kufikia asilimia 1.3 kutoka asilimia 2.7 mwaka 2011. Hii imetokana na ukuaji mdogo wa sekta ndogo ya misitu na uwindaji iliyofikia asilimia 1.2 mwaka 2012 ikilinganishwa na asilimia 6.4 mwaka 2011 na sekta ndogo ya uvuvi iliyofikia asilimia 2.3 mwaka 2012 kutoka asilimia 11.9 mwaka 2011. Hata hivyo, ukuaji wa sekta ndogo ya mazao umepanda kufikia asilimia 0.6 mwaka 2012 ukilinganishwa na asilimia 0.5 mwaka 2011". Tazama maelezo ya hotuba hii.

Lakini kwenye kitabu hiki Mhe. Spika, tuondoke ukurasa wa 21 twende kwenye ukurasa wa 80 – 81 unazungumzia hiyo sekta ya kilimo kwa undani zaidi katika utekelezaji wake. Inasema Mhe. Spika,

> "Mchango wa sekta ya kilimo ukurasa wa 89 umeshuka kutoka asilimia 32.2 ya mwaka 2011 kufikia asilimia 30.2 mwaka 2012, kushuka huko kumesababishwa na kupungua kwa uzalishaji katika sekta ndogo ya mazao, mifugo, misitu na uwindaji".

Sasa najiuliza hawa waandishi wa kitabu hiki walikuwa wamesinzia, lugha nyengine si nzuri sitaki kusema Mwezi wa Ramadhani huu. Ningesema mimi wamepiga tembo maana yake huku ukurasa wa 21 Mhe. Spika, wanasema kwamba sekta ya mazao imekua kutoka asilimia 0.5 mpaka aslimia 0.6, iliyosababisha kushuka ni sekta ya uwindaji na sekta ya uvuvi. Lakini kitabu hicho hicho ukurasa wa 80 katika sababu za kushuka nadhani pia ni kushuka kwa sekta ndogo ya mazao. Sasa ni lipi Mhe. Spika, nahoji umakini wetu katika hata kutuandalia hizi ripoti seuze ukweli wa haya tunayoelezwa katika vitabu hivi.

Nimeona niseme hivyo Mhe. Spika, kwa sababu kama nilivyosema hii ni sekta muhimu sana, lakini sekta ambayo pengine pato lake katika uchumi linapungua lakini linatoa shughuli za uchumi kwa watu wetu kwa takriban asilimia 70 ya wananchi wetu. Sasa kama ni hivyo, tumefanya kitu gani kuunganisha sekta hii na sekta nyengine za uchumi. Mara nyingi nasema sijui kama sifahamiki kwamba huwezi Mhe. Spika, ukaendesha uchumi ikawa sekta moja iko mbali ya uchumi haihusiani kabisa na sekta nyengine za uchumi, lazima kuwe na *link sector* bainaya sekta moja ya uchumi na nyengine ya uchumi ili uchumi uweze kukua kwa pamoja.

Sasa leo tunazungumza sekta ya utalii na tunaambiwa ndio inachukua kwa kiasi kikubwa sehemu ya uchumi wetu, lakini kiasi gani tumehakikisha huduma zinazohudumia sekta ya utalii kutokana na kilimo, uvuvi na mifugo, asubuhi tumepigishana kelele vya kutosha kuhusu kuku kwamba zote hizi zitakwenda kupata nguvu kutokana na kukua kwa sekta ya utalii tunafanya vipi hivyo.

Mhe. Spika, sekta moja ambayo nataka nije nipate maelezo ni sekta hii ya benki ili sekta yoyote ikue lazima wahusika wasaidiwe na moja ni mikopo lakini tumesimamia vipi mabenki yetu na pengine kwa sababu Zanzibar hatudhibiti ndio hivyo tunavyozungumza hatudhibiti fedha zetu na uchumi.

Lakini kitabu hichi hichi ukurasa wa 57 cha mapitio ya hali ya uchumi. Ukenda ukurasa wa 57 utakuta maeneo yaliofaidika na mikopo katika mabenki ya kibiashara, kilimo ni asilimia 0.9. Sasa sekta zote hizo zinasimamiwa na serikali hiyo hiyo moja. Vipi tumeisaidia benki kuhakikisha kwamba katika sera zake na katika uendeshaji wake zinapewa nguvu ya kwamba zitoe msukumo katika kutoa misukumo kwenye mikopo katika maeneo ya kilimo. Mhe. Spika, yote hayo Serikali ije itujibu kwa sababu haiwezekani sekta moja ikawa inaendeshwa mbali na sekta nyengine tofauti halafu hazipati kusaidiana zile sekta.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naomba sasa kidogo nije katika wizara yenyewe. Mhe. Spika, naomba niende kwenye Idara ya Uhakika na Lishe ambayo katika kitabu cha Mhe. Waziri iko katika ukurasa wa 31. Mhe. Spika, mwaka juzi katika misaada ya mwanzo mwanzo kupitishwa katika Baraza hili ilikuwa ni Mswada wa Sheria kuhusu Uhakika wa Chakula na Lishe. Waheshimiwa Wawakilishi tulipokuwa tukichangia tulisema sana humu ndani kwamba je, tunaongeza tena taasisi au kweli tunajielekeza katika kupata huduma hiyo taasisi inayohusika na chakula na lishe.

Mhe. Spika, baada ya miaka miwili hakukuonekani dalili zozote kwamba zinaelekea huko na ripoti za idara hii bado inaonesha hayo kwamba bado tuko katika shughuli ya kujenga misingi ya utawala tu. Katika hili mimi ningeomba wizara ije inisaidie kwa sababu katika kukisoma kitabu chao kinachohusu *program* kisekta nimekitizama hapa kinasema, "Viashiria vya mafanikio ya sekta ndogo au programu ndogo ya uhakika wa chakula na lishe ni kuona kwamba tunahifadhi chakula kwa kuongezeka kwa maghala na tani za chakula zinazohifadhiwa".

Sasa hebu Serikali ije inambie mimi tangu tumepitisha sheria ile ikaunda tume hiyo kubwa inayoongozwa na Makamu wa Pili wa Rais kwa ukubwa wake na watu wengi ndani ya Serikali. Kumefanyika nini mpaka sasa hivi zaidi ya hivi vikao visivyokwisha. Naomba maelezo Mhe. Spika, katika hili.

Nikiondoka hapo Mhe. Spika, sasa naomba niende kwenye Idara ya Umwangiliaji. Mhe. Spika, wala sina kubwa nataka maelezo tu. Sisi ni Wawakilishi wa wananchi wa Zanzibar kwa ujumla wake sio majimbo tunayowakilisha tu hapa. Mhe. Spika, katika Idara hii ambayo imetajwa katika ukurasa wa 34 wa kitabu cha Mhe. Waziri cha bajeti kuna suala zima la uendezwaji wa miradi mbali mbali inayohusu umwagiliaji.

Ukurasa wa 36 pale pamezungumzwa katika mambo yaliyotelezwa ni:
Ununuzi wa ufungaji wa *surface motor* yenye *kilowatt 15* umefanyika sambamba na ukarabati wa *transformer* katika bonde la Bumbwisudi.

Sasa Mhe. Spika, mimi hapa kulikuwa na suala nimetumwa na wananchi naomba niliulize hapa. Wakulima wa Bumbwisudi wanasikitika kwamba katika kupatiwa huduma za umwagiliaji wametakiwa kila mmoja achangie kati ya shilingi ishirini elfu na shilingi thalathini elfu eti kuchangia umeme. Hebu naomba Mhe. Spika, hili akija Mhe. Waziri anisaidie.

Wanasema kuna bwana mmoja anaitwa Kadir Mkuu wa *zone*, huyu akishirikiana na Mkuu wa Kituo cha Umwagiliaji Bumbwisudi ndio waliokuwa wakichangisha na wametajwa katika kamati yao kwamba kuna hizi kamati za mabonde na kila *association* moja ina *plots* kati ya 80 na 100. Sasa wakulima hao maskini ya Mungu kila mmoja katika *plot* moja kaambiwa achangie kati ishirini elfu au thalathini elfu kama gharama ya umeme. Nimefanya hesabu ya haraka haraka tu Mhe. Spika, kama ukichukua kama hizo *association* walizosema wanazo katika bonde la Bumbwisudi na kama kila moja ina *plots* 100 basi ni *plots* 1000.

Kwa gharama za kuchangishwa kiwango cha chini cha ishirini elfu basi hawa wamechangishwa kama ishirini milioni. Sasa hebu tuje kuambiwa kuna sera

hii na hili naliuliza Mhe. Spika, kwa sababu nasikia wamefanya utafiti wenyewe katika maeneo mengine ya mabonde mengine suala hili halipo, liko kwao tu. Kwa hivyo, naomba hili tupewe maelezo na zaidi tumetiwa wasi wasi Mhe. Spika, kwa sababu wanasema walipofuatwa walimwambia huyu muhusika kwa sababu waliambiwa wachangie ili baade wizara kupitia Katibu Mkuu iweze kutia nguvu zake, wakamwambia basi hebu tupe barua ya Katibu Mkuu kuthibitisha hilo. Hiyo barua Mhe. Spika, hawakuipata, kwa hivyo matokeo yake wamechangishwa wanyonge hawa na wameshindwa kufikia hata malengo hawakupata kitu na fedha waliochangia nayo imepotea. Naomba akija Mhe. Waziri aje anipe maelezo ya kina.

Mhe. Spika, mwisho nna mambo madogo mawili tu kwa dakika chache chake kila moja. Moja kwenye miradi ya maendeleo, kutokana na zile hoja ambazo nimezitoa za serikali ambayo ilivyoingiza fedha nyingi katika mwaka 2011, lakini matokeo yake katika kiambatanisho nambari 1 cha hotuba ya Mhe. Waziri kinaonesha mazao yalivyopungua katika kila zao takribani.

Hii ni fedha za miradi ya maendeleo zilizokuwa zimeorodheshwa hapa katika kitabu hiki Mhe. Spika, ambazo ni jumla ya shilingi kumi na saba bilioni mia saba hamsini na moja milioni laki tisa tisini na nane elfu. Katika hizo mikopo inajumuisha kumi na nne bilioni ishirini na tatu milioni laki tano tisini na sita elfu. Hizi si pesa za msaada ni fedha ambazo zizokopwa zinaning'inia katika shingo za Wazanzibari zinaendelea kulipwa miaka mingi ijayo. Tuna haja ya kuendelea kuingiza fedha hizo ikiwa tija ni hii.

Mhe. Spika, naomba hususan maelezo kuhusu programu ya umwagiliaji maji na maelezo kama hayo nilikuwa nimezungumza kuhusu programu ya uhakika wa chakula na lishe kutokana na ahadi walizokuwa wamezitoa. Programu ya kukuza usarifu wa mazao ya kilimo ambapo kuna mia mbili na kumi milioni wakati sijaona mimi kama kuna usanifu wowote wa mazao uliokuwa unafanyika hapa Zanzibar. Programu ya kuendeleza sekta ya kilimo na mifugo (*ASDP- L)* kuna mia nane na sitini na tatu milioni laki moja hamsini na tano elfu.

Programu ya kuimairsha huduma za kilimo (*ASSP)* mia tano sabini na tatu milioni laki nane thamanini na moja elfu. programu ya miundo mbinu ya soko kuongeza thamani za bidhaa na misaada ya kifedha vijijini kuna shilingi bilioni tisa mia nne na nane milioni laki tano sitini elfu, niambiwe programu hii hasa inawafaidisha nani na imefanya nini mpaka hivi sasa. Mwisho programu ya mpango wa ulimwengu wa kusaidia kilimo na uhakika wa chakula kule iko na huku iko, kuna shilingi bilioni moja mia mbili arubaini milioni zinafanya nini fedha hizi Mhe. Spika, tuelezwe.

Katika fedha za mradi wa maendeleo nimeona kuna mradi wa kuangamiza adui kunguru ambao mradi huu umekuja kuripotiwa na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Sasa najiuliza kwa nini unakuwa na mradi mmoja umegawanywa katika wizara mbili. Uhakika wake utapatikana vipi Mhe. Spika, tutapima vipi mafanikio yake ikiwa kila mmoja anafanya kivyake, kwa nini mradi huu mmoja usiwekwe katika wizara moja, ikiwa kilimo uweko kwenye kilimo, ukiwa kwa Makamu wa Kwanza ubaki kwa Makamu wa Kwanza tukapata kupima vizuri.

La pili ninaloomba maelezo sekta ya kilimo si sekta ya muungano lakini wenzetu Tanganyika wanakwenda nje wakaomba fedha kwa ajili ya Jamhuri ya muungano. Nimeangalia kama nilivyoangalia miaka ya nyuma iliyopita kuna (*ASDP-L)* ambayo inaonekana kuna mfuko ulioanzishwa na nchi wahisani kwa ajili ya kusaidia kilimo. Hata katika taasisi zinazohusika Zanzibar hauhusishwi lakini hawa katika programu hii nzima kwa mujibu wa waraka huu ambao unapatikana katika mtandao Mhe. Spika, wala hauna kazi kubwa sana kuupata.

Wahisani peke yake wamechangia mia tatu kumi na moja bilioni mia moja sabini na mbili milioni. Sijui zimegaiwa vipi katika miaka. Lakini kwa mujibu wa bajeti ya wizara ya mwaka huu, Wizara ya Kilimo na Chakula ya Jamhuri ya Muungano kwa mujibu alivyoomba Waziri wake Mhe. Christopher Kajoro Chiza, kaomba katika zile hamsini na saba bilioni mia moja kumi na tatu milioni laki mbili thamanini elfu ni fedha za nje.

Nataka akija Mhe. Waziri aje anasaidie katika mradi huu na katika fedha hizi za nje zinazokuja katika sekta ya kilimo kwa jina la Jamhuri ya Muungano Zanzibar imepata kiasi gani. Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nakushukuru nitaunga mkono hoja baada ya kujibiwa hoja zangu. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*).

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Spika, naanza mchango wangu kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma kwa kuniwezesha kusimama hapa na mimi nikatoa maoni yangu kwenye Wizara ya Kilimo.

Mhe. Spika, vile vile nakushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii lakini pia naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa jitihada alioionesha kwenye kusoma kitabu chake kwa haraka haraka.

Mhe. Spika, sasa naomba nianze mchango wangu kwa kuzungumzia umwagiliaji maji. Mhe. Spika, kwa kweli jitihada wanazozifanya Wizara ya Kilimo katika kutafuta uwezekano wa kilimo cha umwagiliaji maji nawapongeza sana. Kwa kweli huo ni ukombozi kwa mkulima na mara nyingi

wizara ilikuwa ikisema kuwepo mpango mkuu wa umwagiliaji maji. Hili ni jambo zuri naona jitihada zinazofanywa hapa Unguja ambapo miundo mbinu imejengwa na visima vimechimbwa na miundo mbinu ya umeme imepelekwa kwenye mabonde ya Kibokwa na Cheju.

Mhe. Spika, lakini bado kuna mabonde makubwa kama vile bonde la Msaani, Pandani, Kitambuu, Mtambwe, Pujini, Chambani na bonde la Kwa Pweza katika jimbo la Wawi. Mhe. Spika, maeneo haya yana maji mengi katika ardhi lakini bado umwagiliaji haujapewa kipaumbele.

Mhe. Spika, miundombinu ya umeme katika maeneo haya ipo, tatizo ni kujengwa miundombinu ya umwagiliaji maji tu. Sasa namuomba Mhe. Waziri anieleze kwa nini Pemba kilimo cha umwagiliaji maji hakipewi msukumo na hata kikipewa msukumo, hupewa pale ambapo pana mabonde madogo madogo yanayotegemea mito midogo inayoingiza maji yanayotokana na mvua. Mhe. Spika, hapa naomba Mhe. Waziri anieleze huko Pemba kumechimbwa visima vingapi vya umwagiliaji maji.

Mhe. Spika, eneo jengine ambalo naomba nilizungumzie ni kuhusu huduma kwa wakulima. Mhe. Spika, eneo hili wizara haifanyi vizuri na nasema kwa sababu mimi mwenyewe nimetokana na wazazi wa wakulima na katika udogo wangu ilikuwa mara nyingi nakwenda bondeni na bibi yangu na nikiwaona mabwana shamba wakipita mabondeni na wakiwaelekeza wakulima jinsi ya kulima kutumia mbolea kupanda mbegu vizuri. Lakini hivi sasa Mhe. Spika, mabwana shamba wamekuwa mabwana hasa na mabibi shamba hawasemeki, hawaonekani mabondeni wamekuwa ni watu wa maofisini.

Sasa wakulima hawapati ushauri inapelekea wakulima kupanda mbegu zisizokuwa nzuri hawana ushauri wa kutumia mbolea na vile vile katika kilimo chao wanaharibu ardhi kwa sababu hawapati maelekezo ya mabwana shamba. Sasa na hapa namuomba Mhe. Waziri anieleze ana mpango gani au mkakati gani wa kupambana na suala hili na vile vile anambie katika Wilaya ya Chake Ckake kuna mabwana shamba wangapi na wakulima wangapi na hili Mhe. Spika, nataka nilijue kwa sababu nipate nilinganishe kila bwana shamba mmoja anahudumia wakulima wangapi.

Mhe. Spika, suala jengine nitakalotaka kulizungumza ni Karakana ya Matrekta Wawi. Mhe. Spika, ile taasisi ni muhimu kwa kushughulikia zana za kilimo. Lakini karakana ile haiendelezwi na wafanyakazi wake hawapewi motisha. Mhe. Spika, kwa kweli ni jambo la kusikitisha wafanyakazi wale wanavunjika moyo na nadhani Mhe. Waziri angelikaa na watu wake wakaangalia ile karakana itumike vipi vizuri zaidi kwa sababu kuiacha vile ni hasara.

Nashauri mafundi wa karakana waongezewe maslahi kwa sababu Mhe. Spika, haiwezekani fundi wa vespa wa wizara alipwe sawa sawa na fundi wa karakana ambaye anashughulika na kazi nzito. Nafikiria mipira ile yote tunayaona, nanga tunaiona na hakuna zana za kufanyia kazi isipokuwa wanatumia mikono yao na nguvu zao za kifua. Kwa hiyo, namuomba Mhe. Waziri aliangalie hili.

Mhe. Spika, suala jengine nataka nilizungumzie kidogo kwa sababu Mhe. Saleh Nassor Juma alilizungumza kwa kitaalamu kuhusu utafiti. Mhe. Spika, utafiti wa mbegu ni muhimu na nawaomba wizara ifanye utafiti wa mbegu kabla ya kuwagaiya wakulima na hili Mhe. Spika, nasema kwa sababu hivi karibuni nilisikia kwenye mawio kama kuna msimu uliopita wa Vuli, kuna bonde la Dobi na Kinyakuzi wamepelekewa mbegu mbovu ya mipunga na mipunga yao haikuchanua. Hili Mhe. Spika, ni tatizo na naomba wizara isigawe mbegu mpaka izifanyie utafiti na namuomba Mhe. Waziri anieleze baada ya hasara hii walioipata wakulima, Serikali kupitia wizara yake imewasaidia nini wakulima hawa.

Mhe. Spika, suala jengine ambalo ningependa nilizungumzie kidogo ni kuhusu pembejeo. Mhe. Spika, nawapongeza sana Wizara ya Kilimo kwa kuwafanyia mapunguzo makubwa wakulima wenye pembejeo. Lakini hapa Mhe. Spika, kuna manung'uniko kuhusu ugawaji wa dawa na mbolea kwa wakulima wanyonge wanasema dawa hizi haziwafikii zinabakia kwa wakubwa. Sasa Mhe. Spika, namuomba Mhe. Waziri anieleze ni utaratibu upi unaotumika katika ugawaji wa bembejeo, ili ikiwa kuna utaratibu wananchi wanauacha basi waweze kuufuata ili na wao waweze kupata haki yao hii na yale malalamiko yaondoke.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naomba nizungumze kidogo kwenye suala la kilimo cha chumvi. Mhe. Spika, suala la chumvi ni muhimu lakini wizara haijawa makini. Mhe. Spika, katika kisiwa cha Pemba kunazalishwa chumvi nyingi sana lakini wizara haitoi kipaumbele na kuwatafutia masoko wakulima.

Mhe. Spika, nasikia kuna nchi zisizo na bahari kama Congo, Zaire na nyenginezo. Chumvi ina bei nzuri lakini wakulima wa chumvi wa Pemba hubakia na magunia yao ya chumvi hawasaidiwi kuisarifu, kuisaga kuitia kwenye vifurushi na kuiuza.

Mhe. Spika, hapa naomba maelezo kwa Mhe. Waziri kwanza anambie katika Wizara yake ya Kilimo ni idara ipi inayoshughulika na chumvi na vile vile anambie afisa anayeshughulikia zao la chumvi Pemba anaitwaje na kazi yake

inayoifanya kwa wakulima wa chumvi ni ipi ni ushauri, utaalamu au ni nini naomba maelezo kwa Mhe. Waziri.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo nitaunga mkono bajeti hii baada ya kupewa majibu ya masuala ambayo nimeyauliza. Nakushukuru Mhe. Spika.

Mhe. Spika: kuna dakika 10 kama Mhe. Ali Salum Ali unaweza kuzitumia basi zitume hizo.

Mhe. Ali Salum Ali: Ahsante Mhe. Spika, kwa siku ya leo zinatosha sana. Mhe. Spika, nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa na afya njema na tuko hapa.

Pili nimuombe Mwenyezi Mungu *inshaalla* amjaalie afya njema Mhe. Waziri ili arudi katika Baraza hili kuja kujumuika na sisi katika kutekeleza majukumu ya taifa ya wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, mimi michango yangu sio mikubwa sana. Mimi nakwenda katika ukurasa wa 7 Mhe. Spika, katika suala zima la umwangiliaji maji. Hapa nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie bonde la Kibokwa ambapo linasemekana kwamba kwa muda mrefu mashine yake haifanyi kazi na huduma imekuwa haipatikani, kama ni hivyo ni lini huduma itapatikana na lini mashine itarudi ili wananchi wa Kibokwa waweze kulima kilimo chao.

Jengine ni eneo la umwagiliaji maji. Kumekuwa na utaratibu Mhe. Spika, wa kushiriki katika maonesho ya nane nane lakini kinachoonekana malengo makubwa yameelekezwa kwa maafisa wetu wa wizarani kwenda katika haya maonesho ya nane nane na miaka hadi miaka watendaji wanakuwa ndio hao kwa hao. Mimi nahisi Mhe. Waziri angeliangalia njia mbadala baada ya kuwapeleka watu hao kwa hao kila mwaka, basi tuanzishe utaratibu wa kuwapeleka wakulima wa chini kwenda kujifunza maendeleo ya wenzetu katika suala zima la umwagiliaji katika maeneo yetu ili na wao waweze kubadilika na tuone kwamba hali inakwenda vipi katika suala la umwagiliaji maji.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nililokuwa nataka kulichangia Mhe. Ismail Jussa Ladhu kalizungumza sana na mimi sitaki kwenda huko, kuhusu suala la kushuka kwa kilimo lakini mazao mengine kuwa ni finyu. Mimi Mhe. Waziri atakapokuja Mhe. Spika, naomba anisaidie nimekuwa napata kigugumizi hii tathmini ya kushuka au kupanda kwa kilimo au mazao hapa Zanzibar tunaipata wapi, kwa sababu sijapaona pahala ambapo tunakuwa tunaweza kupima mazao yetu si kwa wakulima si masokoni.

Mimi nafikiri Mhe. Waziri atakapokuja atanieleza kwamba tathmini hii tunaipata wapi na kwa vigezo gani, kwa sababu mazingira ya Wazanzibari kila mtu anakishamba chake na kijembe kongoroka analima ndizi zake anapandisha kwennye gari anapeleka sokoni. Sasa hii tathmini tunayoipata katika nchi yetu tunaipata kwa vigezo gani au tunachukua *reference* za miaka iliyopita, labda mwaka jana tungelima hivi, kwa hivyo mwaka huu tunakisia hali imekwenda hivi. Mhe. Waziri atakapokuja anieleze kwamba tathmini ya kilimo au mazao kwa nchi yetu tunaipata kupitia maeneo fulani na tunapima labda mazao haya kwa kujua hizi tani za uzalishaji tunazozipata katika misingi gani. Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie.

Jengine Mhe. Spika, ambalo nataka kulizungumzia ni suala la katika Kitengo cha Utabibu. Mhe. Spika, kuna malalamiko kwa watu wetu juu masuala mazima ya vikopo vya kuhifadhia nzi. Utaratibu uliokuwa umezoeleka sasa hivi haupo, zamani watu walikuwa wanakwenda kwa Masheha wanapata vikopo kwa wakati na sasa suala lile limeonekana kama lina ufinyu na watu wanakuwa wanakimbilia maofisini kuvifuata vile vikopo na inachukua muda mrefu na wakati mwengine usumbufu unakuwa mwingi mtu anatupa nauli, lakini akishafika wizara anakuwa hapati. Mimi niombe kwamba wizara ijitahidi kutumia utaratibu uliokuwa mzuri kufikisha vile vikopo vya kuhifadhia nzi kwa wakulima ili kuondosha usumbufu unaojitokeza.

Sehemu nyengine Mhe. Spika, ambayo nitazungumzia zaidi ni sehemu ya pembejeo. Bado kuna malalamiko wenzangu wamelizungumzia zaidi sana hili na kwa upeo mbali mbali na mimi sipendi kurejea humo kwa humo, wengine wametoa mifano kwamba wakubwa zaidi ndio wanaopata pembejeo lakini waliokuwa wanyonge hawapati. Nafikiri nimuombe Mhe. Waziri kutafuta njia mbadala iliyokuwa nzuri na sio pembejeo zenyewe kama kuletwa tu lakini pembejeo zenyewe mara nyingi zinaonekana kama hazina ubora baada kukuza mimea tatizo linaonekana kwamba ubora wa pembejeo zetu bado haujawa makini.

Sasa sijui zile sababu zinakuwa zinatoka wapi na kuna kipindi cha nyuma kulikuwa na historia refu ambayo tumeizungumza zililetwa pembejeo mbolea hapa baadae zikaunguza mipunga wakulima waliwahi kulalamika juu ya suala hili kuwa mbolea ile ilikuwa na saruji nyingi. Mimi nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja basi atusaidie ile utaratibu kama walivyosema wenzangu wa kutoa pembejeo na ule ubora wa pembejeo.

Mhe. Spika, nataka nimalizie dakika tatu zilizobakia kwa kwenda katika ukurasa wa 17, kinazungumza kuotesha miche milioni mbili aina tofauti ya miti katika eneo la hekta 450. Mhe. Spika, mara nyingi watendaji wetu wamekuwa na tabia ya kujisifu zaidi katika vitabu na ndio maana ukija

kuangalia unakuta mambo hayo kwa hayo kila siku. Lakini mabadiliko hasa unakuwa huyaoni kabisa.

Sasa mimi nataka tusaidiane tunaotesha miche hapa Mhe. Waziri nataka tusaidiane mawazo kwa sababu tunashiriki katika mambo mbali mbali ya kimataifa na maazimio mbali mbali ya kimataifa yanakuwa yanatoka na tunapoteza gharama kubwa sana kushiriki katika mambo yale ya kimataifa na hususan suala lile la upandaji wa miti. Lakini mtu unasikitika tu kwamba mwaka huu milioni mbili na mwaka juzi milioni moja na nusu lakini unakuwa huioni.

Sasa Mhe. Spika, huwa hatupendi kusema lakini inabidi tuseme kule China tumejifunza mambo makubwa sana. Nimuombe Mhe. Waziri ajaribu kushirikiana na wenzetu wa Halmashauri pamoja na Manispaa, wale wenzetu wanafanikiwa vipi ukipita katika ile miji unaikuta *green* kuanzia *airport* mpaka mji mzima. Sasa moja ambalo nimeliona na nimelidadisi pale wanasema kwamba mbinu ambazo wametumia wao hawapandi ile miche midogo midogo katika yale maeneo, unapofikia ule mwaka wa kuanzimisha upandaji wa miti, serikali inatoa gharama kubwa sana kupanda miti maeneo mbali mbali lakini ikimalizika tu miti iliyoota huioni.

Sasa wenzetu wana njia ambayo wanaipanda miti ambayo tayari imesimama na ina uwezo na wanaing'oa mizima mizima na wanatumia majiti kuweza kusimamia. Sasa inakuwa wepesi wa kuota unakuwa mkubwa tofauti na njia tunayotumia sisi ile ya kukurupuka, upandaji wa miti kila mtu na mti wake hata wewe Mhe. Spika, umeshapanda miti sana. Lakini tatizo tukija kuitafuta ile miti tuliopanda mwaka jana huioni. Mimi nafikiri tungejifunza kwa wenzetu njia ambazo wanatumia katika upandaji wa miti katika nchi zao na miti inavyoweza kukua na ikabadilisha mandhari ya nchi zao, kuliko zile njia tunazotumia sisi za kukurupuka na kutumia gharama kubwa pasipo na mafanikio.

Mhe. Spika, kwa sababu nilikuwa naenda haraka haraka zaidi kwa ajili ya kukwepa muda wako muda umemalizika. Kwa niaba yangu na kwa niaba ya Jimbo la Kwahani, mimi kwa wizara hii sina pingamizi naunga mkono hoja ya wizara hii kwa asilimia mia moja. Nakushukuru sana Mhe. Spika, ahsante sana.

Mhe. Spika: Mhe. Ali Salum Haji nakushukuru kwa kuzitumia vyema dakika kumi ukaweza kumaliza mchango wako.

Waheshimiwa Wajumbe narudia tena kusema kwamba tuko nyuma mno ya ratiba na sisi ndio ambao wa kuamua twende vipi sisi Waheshimiwa

Wajumbe. Hivyo naomba niseme kwamba Mwenyezi Mungu akipenda tutakuja na wazo na utaratibu wa kumaliza shughuli zetu na nitawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe mje kuniunga mkono.

Hali ya ratiba yetu iko ngumu nzito na muda tuliokwishatumia ni mkubwa mno kiasi cha kwamba ni historia ya chombo chetu hiki kuchukua muda mkubwa mwaka huu. Najua ni kwa madhumuni ya kuweka na kusimamia vizuri Serikali katika shughuli zake. Lakini vizuri vile vile kuzingatia ratiba na utaratibu wa shughuli hizi zinakwenda kwa ufanisi mzuri kwa muda ambao tunaupanga kwa sasa ni karibu tuko nyuma kwa siku nane za kazi.

Sasa hali hii itatuweka pahali pagumu sana kwa mujibu wa bajeti yetu namna itakavyomalizia kwa mwaka huu wa fedha 2013/2014, itakuwa si mfano wa kuigwa kimatumizi ambacho chombo hiki kilikuwa kinafaa sana iwe ni mfano wa kuigwa kimatumizi ili tuweze kuwa na nguvu ya kusimamia Serikali katika matumizi vile vile. Kwa hivyo, tutaanda utaratibu ili tuone tunamaliza shughuli zetu mapema iwezekanavyo kwa muda mfupi uliobaki ili tuweze kuungana na familia zetu kumaliza mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Baada ya machache hayo Waheshimiwa Wajumbe naahirisha kikao hichi hadi kesho tarehe 30/7/2013 saa 3:00 barabara asubuhi.

(Saa 8:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi tarehe 30/7/2013 saa 3:00 asubuhi)